

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Sita – Tarehe 4 Aprili, 2006

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwataarifu kwamba leo tunao wageni katika *Speakers Gallery* pale mtamwona Bwana na Bibi. Hao ni Bwana na Bibi Darbo ambapo Mr. Darbo yeye ni mtumishi mwandamizi katika *House of Commons*, Bunge la Uingereza, amekuja kututembelea.

WABUNGE FULANI: Hatuwaoni.

SPIKA: *Mr. and Mrs. Darbo, could you please stand up so that the MPs can acknowledge your presence.*

(Hapa Bwana na Bibi Darbo walismama ili Waheshimiwa Wabunge wawaone)

SPIKA: *Thank you, thank you very much Mr and Mrs. Darbo.*

Bado hajajifunza Kiswahili. *(Kicheko/Makofî)*

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: -

Taarifa ya Mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Mwaka 2002/2003.

SPIKA: Nimepokea ombi hapa ambalo naomba niliheshimu.

Mheshimiwa Godfrey Zambi anatuarifu kwamba kwenye upande wa kushoto nadhani wa *Gallery*, wapo Waheshimiwa Madiwani watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Ahsante sana. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Hatuwaoni.

SPIKA: Wako pale.

Waheshimiwa Wabunge, mnajua Waheshimiwa Madiwani ni muhimu sana, mkiwa na watu wa namna hii msisitie kumwarifu Spika ili waweze kutambuliwa. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu, kifungu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kifungu 32.

SPIKA: Haya Kifungu Namba 32.

MHE. HALIMA J. MDEE: Ndiyo Mheshimiwa. Spika.

SPIKA: Haya endelea Mheshimiwa Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, Hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na kujadiliwa kwa hii Hati, naomba nisome Kifungu cha 32 cha Kanuni za Bunge.

Kifungu husika kinasema: "Wakati wowote baada ya Hati yoyote kuwasilishwa Bungeni, kwa mujibu wa Kanuni ya 31, Waziri au Mbunge aliyewasilisha hati hiyo au Mbunge mwingine yeyote aweza kutoa hoja kwamba Bunge lijadili Hati hiyo. Hoja iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii haihitaji kutolewa taarifa na itaamuliwa bila mabadiliko au mjadala wowote. (*Makofi*)

Hoja ya kujadiliwa Hati zilizowasilishwa Bungeni ikikubaliwa itashughulikiwa kwa kufuata masharti ya Kanuni ya 23(iv) isipokuwa kwamba taarifa zinazowasilishwa Bungeni na Kamati yoyote ya Kudumu au Kamati Teule zitatengewa muda wa kujadiliwa Bungeni bila hoja kutolewa."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni, hii naomba kwa mujibu wa ratiba yako upange muda ambao Wabunge wataijadili hoja iliyoletwala na Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nitazingatia na nitawapeni uamuzi kabla ya mwisho wa Bunge hili linaloendelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA): Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu Utaratibu, endelea Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA): Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu, katika Hoja ya namna hii, lazima aungwe mkono. Lakini mpaka amekaa hakuna Mbunge yejote aliyeunga mkono Hoja hiyo. (*Makof/Kicheko*)

SPIKA: Nadhani sasa Mheshimiwa hukujandaa vizuri basi, maana kumbe hii Hoja haikuungwa mkono. (*Makof/Kicheko*)

Naomba utulivu. *Order, Order*, naomba utulivu. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita haji, swali la kwanza la leo.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 74

Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI aliuliza: -

Kwa kuwa lengo la Serikali si kubomoa majengo yaliyojengwa bila kupimwa rasmi katika sehemu zisizokuwa hatari bali ni katika harakati za kuimarisha miundombinu ya barabara katika sehemu hizo: -

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha miundombinu ya barabara huko Majohi Mji Mpya, Kata ya Chanika katika Manispaa ya Ilala, Jijini Dar es Salaam?
- (b) Je, Serikali inayatambua maeneo hayo na kama imeyatambua inaweza kunitajia maeneo machache kati ya hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, kama ifuatavyo: -

- (a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, lengo la Serikali si kubomoa majengo yaliyojengwa katika maeneo yasiyopimwa rasmi, bali lengo ni kutaka kuimarisha miundombinu ya barabara katika sehemu hizo ili wananchi hao waweze kupatiwa huduma muhimu zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa miundombinu huko Majphe Mji Mpya, Kata ya Chanika katika Manispaa ya Ilala, Serikali tayari imekwishaanza shughuli za uimarishaji wa miundombinu ya barabara mpya.

Kazi hiyo imeanza kwa kuchonga barabara hizo kwa greda la Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na kuziwekea kifusi cha changarawe ili kuziimarishe na kuweza kupitika kwa urahisi, ikizingatiwa kwamba eneo la Majphe Mji Mpya ni eneo lenye udongo wenge mchanga mwingi.

Mpaka sasa Manispaa imeishachonga barabara tano (5) zenye urefu wa jumla ya kilomita 24 na baadhi ya barabara hizo ni pamoja na: -

- (i) Chanika hadi Mji Mpya.
- (ii) Mji Mpya hadi Kivule kupitia kwa Dihume.
- (iii) Mji Mpya hadi Shule ya Msingi Kivule.
- (iv) Barabara inayotoka Shule ya Msingi ya Pugu hadi Majphe yenye urefu wa kilomita 4.

Gharama zilizotumika ni Shilingi milioni 4.5 ikiwa ni gharama za mafuta, kifusi pamoja na posho ya wasimamizi. Wakati wa utekelezaji wa kazi hiyo, hakuna jengo lililobomolewa ili kuruhusu uendelezaji wa miundombinu ya barabara katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, barabara za eneo la Majphe Mji Mpya zimeboreshwa kwa ushirikiano baina ya wananchi na viongozi wa mtaa wa eneo hilo hususan Mwenyekiti wa Mtaa wa Mji Mpya, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kivule na Katibu wa Mtaa wa Majphe. Ushiriki wa wananchi pamoja na viongozi umesaidia sana kubaini maeneo ya kupita barabara hizo, ikizingatiwa kwamba eneo lote la Majphe Mji Mpya halijapimwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inayatambua maeneo hayo yaliyojengwa bila kupimwa rasmi au ambayo yamejengwa kiholela. Maeneo hayo ni pamoja na: -

- (i) Eneo la Buyuni, Kata ya Chanika.
- (ii) Eneo la Machimbo, Kata ya Kitunda.
- (iii) Eneo la Mwakanga, Kata ya Pugu.

Maeneo yote hayo yapo nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam katika eneo la Wilaya ya Ilala kwenye kata za pembezoni.

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Katika maeneo hayo, kuna maeneo kwa mfano kama Jangwani pale Dar es Salaam. Je, Mheshimiwa Waziri ataniambia kwa wale watu kama wa Jangwani ambao wako hatarini Serikali inachukua hatua gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: - Mheshimiwa Spika, kabla ya kusema naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita, nilipoona ameuliza swali ambalo linahusu eneo la Ilala, lakini kwa kujua kwamba ni mtu wa Zanzibar nikasema huyu ni Mtanzania safi sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la Ilala, nadhani Mheshimiwa Mbunge, Dr. Mwita anajua juhudhi ambazo Serikali imefanya karibu kipindi chote, kutoa amri za hapa na pale kujaribu kuwaomba vile vile wananchi wasiishi katika maeneo yale, lakini bado hatukuweza kufanikiwa hadi hivi sasa. Kwa hiyo, tunachojaribu kufanya ni kufanya *upgrading* ya maeneo ambayo sasa yamepewa kipaumbele kwa eneo la Dar es Salaam. Kwa hiyo, naamini Ilala, Manzese na maeneo mengine ya aina hiyo yatakuwa katika mradi huo na tunatumaini itasaidia kidogo kuweza kuboresha mazingira katika eneo hilo.

Na. 75

Uhitaji wa Madaktari – Zahanati Zilizoko Sikonge

MHE. SAID J. NKUMBA aliuliza: -

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Sikonge wamejenga zahanati katika kata za Tutuo, Kipanga, Sikonge, Igigwa na Pangale, lakini tatizo hakuna wataalam wa kutoa huduma za afya kwenye zahanati hizo: -

Je, ni lini Serikali itaanzisha mpango kabambe wa kutoa nafasi nyingi za ajira kwa kada hii ili wataalam hao waende vijijini ambako zahanati nyingi kama zilivyo kwenye Jimbo la Sikonge zimekamilika lakini hazina wataalam wa kutosha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wilaya ya Sikonge ina upungufu mkubwa wa watumishi wa afya. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ina jumla ya zahanati 25, kituo cha afya kimoja na hospitali teule moja. Kati ya zahanati hizo 25, zahanati 20 ni za Serikali na tano ni za watu binafsi. Zahanati mbili bado hazijaanza kutoa huduma.

Aidha, zahanati nyingi zilijengwa chini ya mradi wa *TASAF*. Katika mwaka 2003 – 2006 Halmashauri iliomba na kukubaliwa kuajiri watumishi 17 katika kada mbalimbali. Nafasi zilizojazwa ni mbili tu kati ya zile nafasi 17. Aidha, kulingana na ikama ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, watumishi wa afya waliopo katika zahanati zote ni watano (5) tu kati ya watumishi 108 wanaohitajika katika zahanati na vituo vya afya.

Watumishi wawili wapo katika kituo cha afya ambapo kituo hicho kinahitaji watumishi 19.

Kwa kuelewa ugumu na upatikanaji wa watumishi kada ya afya, Wizara ya Afya kwa kutumia nafasi zilizotengwa mwaka 2004/2005 iliwapangia vituo Maafisa Tabibu watatu katika Wilaya ya Sikunge, lakini kati yao hao watatu aliyeripoti ni mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linalosababisha upungufu huo ni kutopatikana kwa watumishi hao katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikunge. Kwa mfano, kwa mwaka 2003/2004 kati ya nafasi tisa zilizotangazwa ni nafasi moja tu ndiyo ilijazwa na nafasi nane hazikupata watumishi. Mwaka 2004/2005 nafasi tano zilizotangazwa zote hazikujazwa kwa sababu watumishi hawakupatikana.

Kwa mwaka 2005/2006 Halmashauri imeamua kuomba watumishi Wizara ya Afya kwa kutumia utaratibu wa kuwapangia moja kwa moja katika vituo hivyo katoka vyuoni. (*Makofi*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Tatizo la watumishi katika Idara ya Afya ni kubwa sana katika nchi nzima na kinachosikitisha hasa ni kwa kiwango cha Madaktari wanaomaliza masomo katika Vyuo Vikuu (*intern students*). Madaktari hao wakimaliza huwa hawapangiwi kazi, wanahangaika kutafuta wenyewe na wengine wanafanya kazi kwenye maduka ya dawa.

Je, Waziri haoni kwamba kuna umuhimu hata hao kuwachukua moja kwa moja wakiwa bado vyuoni badala ya kuacha wakahangaika? (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza. Lakini kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli watumishi wa afya, wataalam ni wachache. Ni nusu ya ikama ambayo imeruhusiwa. Moja ya matatizo ni utaratibu ambao upo sasa hivi wa kuwataka Halmashauri watangaze kazi halafu watumishi wa afya waombe na utakuta maeneo mengine hayapendeki sana. Kwa hiyo, tumezungumza na wenzetu TAMISEMI pamoa na Utumishi tumekubaliana kwamba sasa Wizara ya Afya itakuwa inawapangia vituo moja kwa moja wakitoka shulenii, hakutakuwa na masuala ya usaili tena. (*Makofi*)

Ningependa niwapongeze wananchi wote ambao wamekuwa wakijenga vituo. Kwa mfano, nilitembelea Wilaya ya Urambo ambapo wamejenga dispensary 15, nane zimekamilika, lakini hazijaanza kufanya kazi kwa sababu hakuna watumishi. Ningeomba wananchi wengine waige mfano wa Jimbo la Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ningeomba Halmashauri zitenge mafungu ili tutakopopeleka watendakazi wasipate matatizo ya kupata mishahara. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa jibu zuri sana. (*Kicheko/Makofî*)

Na. 76

**Athari za Maji Machafu Yanayotoka Katika Kiwanda cha Bia
Dar es Salaam**

MHE. AMINA C. MPAKANJIA (k.n.y. MHE. ANIA S. CHAUREMBO
aliuliza: -

Kwa kuwa mfereji wa maji machafu utokao katika Kiwanda cha Bia cha Ilala, Dar es Salaam unapita kwenye makazi ya watu na kwa kuwa mfereji huo unasababisha kero na adha kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo ambamo unapita kwani unatoa harufu mbaya na kuacha takataka ambazo zinadhaniwa kuwa ni chanzo cha maradhi ya kipindupindu na malaria na kwa kuwa kiwanda hicho ni chanzo cha mapato ya Serikali: -

- (a) Je, Serikali imefanya utafiti ili kujua ni kwa kiasi gani wakazi wa eneo hilo wameathirika kiafya na kisaikolojia kutokana na mfereji huo?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iko haja ya kumshirikisha mmiliki wa kiwanda hicho pamoja na Serikali kuufunika mfereji huo ili kupunguza adha, kero na athari za kiafya kwa wakazi wa maeneo hayo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)
alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maji taka kutoka katika Kiwanda cha Bia Tanzania (*TBL*) hutirishwa kwenye mfereji wa maji ya mvua wa Mchikichini, eneo lenye wakazi wengi na ambalo halijapimwa. Maji hayo yana kiwango cha kemikali cha Ph. 6-7, kiwango ambacho hakina madhara na kinakubalika kuingiza maji taka kwenye mfumo wa mifereji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na sera ya *SAB Miller*, Kampuni Mama ya *TBL* ambayo ni kampuni ya pili duniani kwa ukubwa katika utengenezaji wa bia, *TBL* imelazimika kuangalia viwango vya juu zaidi vya mazingira, *ISO 14000*. *TBL* sasa inatekeleza mpango wa kusafisha maji taka kwa namna ambayo yanaweza kutumika tena kiwandani.

Awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji taka, mtambo ambao sasa unajengwa na unatarajiwa kuanza kutumika Agosti 2006. Awamu ya pili itakayotekelezwa mara tu baada ya awamu ya kwanza, itahusu kuongeza ubora wa maji hayo kufikia kiwango cha maji ya kunywa. *TBL* itatumia dola za Kimarekani milioni 3,400,000 kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na niliyoyaeleza hapo awali, athari za kiafya kwa wananchi wa Mchikichini zinasababishwa na kiwango kikubwa na taka yabisizinazotupwa kwenye mfereji wa maji taka yanayotiririshwa kwenye mfereji huo kutoka kwenye nyumba za wakazi na taasisi, mahoteli na migahawa iliyo katika eneo hilo. Hali hii husababisha maambukizi ya magonjwa ya kipindupindu, homa ya matumbo na malaria.

Mheshimiwa Spika, mfereji huu ni mmoja wa mifereji minne iliyopo katika eneo la Mchikichini, iliyochimbwa kwa madhumuni ya kuondoa maji ya mvua. Hivyo basi, kuufunika mfereji huo kunaweza kusababisha mafuriko katika eneo hilo. Ufumbuzi wa muda mfupi ni kwa uongozi na wakazi wa eneo la Mchikichini kufufua chama chao cha hiari (*NGO*) cha usafi wa mazingira. *TBL* wako tayari kukisaidia kikundi hicho kwa vifaa na fedha, kama walivyofanya mwaka 2001 na mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa kudumu ni kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Dar es Salaam (*DAWASCO*) kubuni mradi wa ukusanyaji na utupaji wa maji taka (*sewerage system*) kwa ajili ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, wastani wa asilimia 70 ya wakazi wa nchi yetu wanakaa katika maeneo ambayo hayajapimwa na hayana huduma za jamii na miundombinu. Mradi wa namna hiyo ukikamilika unawenza kuwa mfano wa namna ya kushughulikia tatizo la maji taka katika maeneo ya aina hiyo ya miji yetu. Serikali itakuwa tayari kuangalia uwezekano wa kusaidia utekelezaji wa mradi kama huo.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa ya kujibu swalii la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwa kulipokea vizuri tangazo la Serikali kuhusu hatua za kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji nchini.

Ninaamini Waheshimiwa Wabunge tutakuwa mstari wa mbele katika kusimamia utekelezaji wa hatua hizo katika maeneo yetu tukiazimia kuwaachia watoto wetu na wajukuu wetu urithi wa nchi ambayo haitofautiani sana na ile tuliyorithi kutoka kwa wazazi wetu, bibi zetu na babu zetu. (*Makofi*)

MHE. AMINA C. MPAKANJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swalii moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa eneo hili la Mchikichini lina wakazi wengi sana. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwakutanisha wakazi wa eneo hili la Mchikichini na mmiliki wa kiwanda hiki cha bia ili waweze kuweka utaratibu wa kutunza mazingira na kuweka hali nzuri ambayo inawatatiza wakazi wa eneo hili? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, niko tayari na ninamkaribisha tuandamane naye. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, maji taka sasa hivi Dar es Salaam imekuwa ni kero kubwa, si kutoka katika viwanda tu, lakini kutoka hata katika nyumba za watu binafsi. Zamani kulikuwa na watu wa Wizara ya Afya waliokuwa wakipitapita kuhakikisha kwamba wale wanaoacha maji taka wanachukuliwa hatua.

Pamoja na kusema kwamba anawaachia Jiji na Halmashauri, lakini Mheshimiwa Waziri haoni kwamba wakati umefika sasa wa Serikali kulishikilia suala hili ili kusudi watu wasalimike na maji taka ambapo sasa hivi watu wanatozwa fedha lakini maji taka hayashughulikiwi? Pia, Serikali inafanya nini ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondolewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la uchafu, tatizo la maji taka toka majumbani na maji taka toka viwandani ni kubwa sana Dar es Salaam, katika miji mingine na katika nchi yetu kwa ujumla. Tumejizatiti ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, sheria mpya ya usimamizi wa mazingira, sheria namba 20 ya mwaka 2004 ni kali sana na inatoa majukumu bayana kati ya Halmashauri za Miji, Halmashauri za Wilaya pamoja na Serikali Kuu na vile vile uteuzi wa Afisa Mazingira katika Halmashauri zetu.

Lakini vile vile katika Halmashauri kuna Mabwana Afya na sheria hii inatoa adhabu kali sana kwa uchafuzi wa mazingira. Kazi iliyopo sasa kwa kweli si kuongezea sheria, isipokuwa ni utekelezaji wa sheria zilizopo.

Serikali imeishatoa tangazo kuhusu hifadhi ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, basi tungoje tena tangazo lingine kuhusu uchafuzi wa mazingira katika maeneo mingine. Tangazo hilo litakuja tu, tunaomba tushirikiane katika kutekeleza sheria zilizopo.

Na. 77

Kiwanda cha Kusindika Matunda

MHE. RAMADHANI A. MANENO aliuliza: -

Kwa kuwa wakazi wa Chalinze ni wakulima wakubwa wa mananasi hapa nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea kiwanda cha kusindika matunda ili kuepuka unywaji wa juisi ya nanasi toka nje?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakazi wa Chalinze ni wakulima wakubwa wa mananasi hapa nchini na kwamba unywaji wa juisi ya nanasi toka nje unaendelea licha ya kuzalisha mananasi kwa wingi. Ni kweli vile vile kwamba ili kuikabili hali hiyo kuna haja ya Mji wa Chalinze kuwa na kiwanda chake cha kusindika matunda.

Kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu, Wizara yangu imepewa jukumu la kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji na kuhamasisha wawekezaji binafsi kujenga viwanda mbalimbali vikiwemo vya kusindika matunda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Wizara yangu kwa kupitia *SIDO* na kwa msaada wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*) na Jumuiya ya Madola (*COMSEC*), ilibuni mradi ambaao umetoa mafunzo kwa wajasiriamali 3,700 kote nchini. Pia, wakufunzi 150 wameandaliwa kwa ajili ya mafunzo ya usindikaji ambapo wawili kati yao wanatoka Mkoa wa Pwani.

Mwaka 2005 *SIDO* Mkoa wa Pwani ilitoa mafunzo ya usindikaji na masoko (*Processing and Marketing*) kwa awamu mbili Wilayani Bagamoyo (ambako ndiko Jimbo la Chalinze liliko). Jumla ya watu 60 walifaidika na mfunzo hayo. Pia, mwanzoni mwa mwezi Machi mwaka huu, mafunzo kama hayo yamefanyika kwa vijana kwa kushirikisha Jumuiya Endelevu Bagamoyo (*JEBA*).

Ni lengo la Serikali kuendeleza mafunzo ya usindikaji kote nchini ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wahitimu wa mafunzo hayo kuzingatia ubora wa bidhaa na ufungashaji.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa matunda ni zao muhimu sana kwa matumizi ya sisi binadamu. Je, Serikali ina mpango gani kuwatafutia masoko na chombo kitakachowenza kuwasaidia wakulima wa matunda hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, nafurahi kumueleza Mheshimiwa Maneno kwamba, Serikali imefanikiwa kupata mwekezaji wa kiwanda kikubwa cha kusindika matunda ambacho kinaitwa *UMNAT fruit processing* kitakachojengwa Mjini Morogoro. Kiwanda hiki kina uwezo wa kusindika tani 100 za matunda kwa siku na tayari kimeishaingia mkataba na wakulima 5,000 wa Mkoa wa Tanga, Pwani na Morogoro na mazao ambayo yatakuwa yananunuliwa ni mananasi na machungwa ambayo yanapatikana katika maeneo hayo. (*Makofî*)

Kiwanda hiki mitambo yake itaingia hivi karibuni na inategemea kusimikwa Juni mwaka huu na uzalishaji utaanza mwezi wa wa Julai. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge soko la matunda hayo limeishapatikana. Ahsante. (*Makofifi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu hayo mazuri, nadhani hakuna haja ya nyongeza. (*Makofifi*)

Na. 78

Soko la Kimataifa la Kigoma

MHE. PETER SELUKAMBA aliuliza: -

Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma ni kioo cha nchi yetu kwa nchi tunazopakana nazo za *Congo DRC*, Burundi, Rwanda na Zambia na kwa kuwa wafanyabiashara wa nchi hizo huja mkoani Kigoma kibiashara:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga soko kubwa la Kimataifa Mjini Kigoma?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa kipaumbele katika uendelezaji wa miundombinu ya masoko kama barabara za vijiji, masoko na maghala ili kukuza ushindani wa biashara na mazao ya kilimo na hivyo kuwezesha kuinua uchumi wa wakulima na wadau wengine wanaotegemea Sekta ya Kilimo.

Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa maeneo ya biashara yanayounganisha nchi yetu na nchi nyingine kama vile Mji wa Kigoma ambao ni kiungo cha biashara kati ya Tanzania na nchi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nafasi ya Mji wa Kigoma katika kuendeleza biashara ya mazao kati ya nchi yetu na nchi jirani, ninakubaliana na pendekeso la Mheshimiwa Selukamba la ujenzi wa soko la kimataifa katika mji huo. Hata hivyo, napenda kurudia maeleo ambayo nimewahi kuyatoa wakati nikijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge waliopendekeza ujenzi wa masoko ya kisasa katika maeneo yao kuwa, Halmashauri ya Mji wa Kigoma iingize katika mpango wake wa maendeleo ujenzi wa soko la Kimataifa na Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri hiyo kufanya tathmini ya ujenzi wa soko hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeweka mkakati wa kufanya tathmini ya kina ya maeneo mbalimbali (*strategic areas*) ambayo yanafaa kujenga masoko ya kisasa kwa

kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na miji husika hatimaye kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha zitakazotumika katika uendelezaji au ujenzi wa masoko hayo. Mkakati huo wa Wizara unaendelea na azma ya swali la Mheshimiwa Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini. (*Makofi*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kweli kwa kukubalia ombi langu bado naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

- (a) Ningependa kujua Bajeti ya ujenzi wa soko hilo itatoka kwenye *program* ipi na itakuwa *funded* na nani?
- (b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri mpaka sasa Wizara yake imejenga masoko mangapi ya kimataifa hapa nchini? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kwanza *program* ambayo inajenga masoko sasa hivi inaitwa (*Agricultural Marketing System Development Program*) ni mpango unaoendeleza mfumo wa masoko, Tanzania. Mfumo huu unafadhiliwa na watu wafuatao; Benki ya Afrika Maendeleo imechangia dola za Kimarekani Milioni 25, *International Fund for Agriculture Development (IFAD)* imechangia Dola za Kimarekani 19.3, Serikali ya Tanzania imechangia dola za Kimarekani milioni 7.5 na Serikali ya Ireland imechangia dola za Kimarekani milioni 1.13.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ambazo tayari zimeshajengwa masoko hayo ambayo yako sita ni hizi zifuatazo; soko la kwanza lipo Arusha linaloitwa Kikatiti ambalo limefikia asilimia 100, soko lingine lipo Babati linaitwa Galapo limefikia asilimia 80, soko lingine lipo Muheza limefikia asilimia 80 linaitwa Mtindira, soko lingine lipo Inyala Mbeya limefikia asilimia 80 na lingine liko Matai kule Sumbawanga limefikia asilimia 80. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Kawawa kweli swalii la nyongeza! Maana yake majibu yanaonekana kutosheleza lakini una nafasi. (*Kicheko*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya yetu ya Namtumbo inazalisha kwa wingi mazao ya mahindi, mpunga, karanga na ufuta, lakini bado tunapata shida ya masoko. Je, Wilaya ya Namtumbo imo katika Mikoa ambayo itafaidika na mpango maalum wa masoko ya mazao ya kilimo ya *AMSDP* na kama imo Serikali itatusaidiaje ili tuweze kufaidika na mpango huo? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante naona ni swalii zuri tu kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri uwahakikishie Namtumbo kama kuna chochote huko. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa kujali watu wake wa Namtumbo na soko la Tumbaku pamoja na mazao mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Namtumbo ni Wilaya ambayo ipo katika Mikoa 8 iliyoko kwenye mfumo huu wa *AMSDP*. Mikoa hiyo ikiwa ni Ruvuma, Mbeya, Iringa, Rukwa, Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Manyara, hiyo Mikoa 8 ilichaguliwa kutohama na kwamba inazalisha sana lakini hawana sehemu ya kuuzia.

Kwa hiyo, kwa kuwa Wilaya yake iko kwenye Mkao wa Ruvuma ninakubaliana na yeye kwamba kuna uwezekano wa kujengewa soko lakini Halmashauri ya Wilaya yake iende ikae na itathimini kwa vigezo ambavyo nilishavitoa. Nashukuru sana. (*Makofit*)

Na. 79

Awamu ya Pili ya Mradi wa *TASAF*

MHE. ALI AMEIR MOHAMED aliuliza:-

Kwa kuwa Rais, aliyepita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikwishazindua awamu ya pili ya mradi wa kusukuma maendeleo ya huduma za jamii kutoka pande zote mbili za Muungano;

- (a) Je, Serikali inaweza kueleza Zanzibar itafaidika vipi katika awamu hii ya pili?
- (b) Je, fomula ya utekelezaji itakayotumika katika awamu hiyo itakuwa ile ile ya asilimia 80 kwa 20 za wananchi au ni tofauti?

WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mbunge wa Donge, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Zanzibar itafaidika katika awamu ya pili ya *TASAF* kwa maeneo yafuatayo:-
 - (i) Visiwa vya Unguja na Pemba vitapatiwa fedha toka *TASAF* kwa ajili ya miradi itakayotekelzwa katika ngazi ya Sheha.
 - (ii) Wajumbe wa Kamati za Masheha na Makundi ya Walengwa katika ngazi ya Sheha watajengewa uwezo kupitia mafunzo yatakayotolewa kwa usimamizi wa miradi.
 - (iii) *TASAF* itatoa fedha kwa ajili ya kusaidia kuhamasisha kuanzisha na kujenga uwezo wa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza ili kupambana na umaskini kwa makini zaidi.
 - (iv) Watumishi katika Wizara husika, Mikoa na Wilaya, watajengewa uwezo ili kuwasaidia wananchi katika utekelezaji wa miradi yao.

(v) Asasi zisizokuwa za Kiserikali zitakazohusika kikamilifu kusaidia wananchi kwenye utekelezaji wa miradi zitajengewa uwezo wa kushughulikia masuala haya. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, mchango wa jamii katika utekelezaji utategemea aina ya malengo na aina ya mradi. *TASAF* itachangia miradi ya makundi ya walengwa wa aina tatu kama ifuatavyo:-

(i) Jamii maskini zisizokuwa na huduma za jamii na masoko. Kwa kundi hili mchango wa jamii ni kiasi kisichopungua asilimia 20 inajumuisha vifaa, nguvu kazi na/au fedha isipokuwa kwa miradi ya maji.

(ii) Makundi maalum katika jamii kama vile yatima, wagonjwa wa muda mrefu, wajane, wazee waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI na kadhalika mchango wa jamii ni kiasi kisichopungua asilimia 5 ya gharama yote ya mradi.

(iii) Kaya maskini zinazokabiliwa na uhaba wa chakula, lakini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Walengwa katika kundi hili hawatachangia badala yake watapatiwa ajira ya muda na kupewa stadi mbalimbali. Walengwa wa aina hii watafanya kazi na kulipwa ajira amba ni asilimia 90 ya ujira wa kawaida ili kutowavuta wale amba siyo wahitaji.

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa awamu ya kwanza imemalizika sasa tunaingia awamu ya pili, lakini baadhi ya Sheha hasa ndani ya jimbo langu la Jang'ombe hakuna Sheha hata moja iliyopata hata katika awamu ya kwanza.

Je, hii awamu ya pili itaanza kwa sisi ambao hatujapata kabisa, au itakuwa kama ule msemo wa Biblia kwamba “mwenye nacho ndiye anayeongezewa”? (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, nadhani katika ile semina ambayo tulishiriki tulisema ya kwamba awamu ya kwanza ilihuisha Wilaya 40 tu, sasa zitahusisha Wilaya zote nchini. Kwa hiyo, Jimbo la Jang'ombe nalo litafaidika. (*Makofi*)

Na. 80

Umaskini Uliokithiri kwa Wananchi wa Vijijini

MHE. AME PANDU AME aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi waishio Vijijini wana hali mbaya sana ya umaskini uliokithiri na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imekusudia kukuza uchumi endelevu nchini.

Je, Serikali ya Awamu ya Nne itafanya nini kwa wananchi walio Vijijini kuhakikisha kwamba wanajikwamua na umaskini walio nao?

WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Ame Pande Ame, Mbunge wa Nungwi, swali lake kama ifuatavyo:-

Serikali ya Awamu ya Nne, imeahidi kuleta Mapinduzi ya kilimo na kufanya kilimo kiwe cha kisasa zaidi kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya 2005 kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Katika kipindi hiki Serikali imepanga kutekeleza mikakati ifuatavyo kwa minajili ya kuboresha maisha ya wananchi wa Vijijini, ambako ndiko Watanzania wenzetu wengi wanaishi:-

Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini (MKUKUTA) ambao sera za sekta za kukuza uchumi ikiwemo sekta ya kilimo ambayo inagusa wananchi wengi wa Vijijini imepewa kipaumbele. Hii ni pamoja na kusimamia na kufuutilia kikamilifu utekelezaji wa mkakati wa maendeleo ya kilimo na mkakati wa maendeleo ya barabara pamoja na uanzishaji wa wakala wa nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini na Baraza la Taifa la Uwezeshaji na hatimaye uanzishaji wa Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, masuala makuu yaliyoainishwa na kupewa kipaumbele ni haya yafuatayo:-

- (i) Serikali itaendelea kuboresha miundombinu na hasa barabara za Vijijini na zile zinazounganisha Mikoa na Wilaya, ili kurahisisha njia za usafirishaji wa mazao na kufikika kwa urahisi vituo vya afya na huduma nyingine za jamii.
- (ii) Kuboresha njia za upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ili kuongeza mapato ya chakula na biashara.
- (iii) Kujenga uwezo wa wananchi katika viwanda na biashara ndogo na kati kama Sera ya Viwanda na Biashara Ndogo na za Kati ya 2003 inavyoelekeza, kuimarisha jitihada zinazoendelea za utafutaji wa masoko ya ndani na nje ili kuwarahisishia wananchi wa vijijini kuuza mazao yao.
- (iv) Kuboresha usimamizi wa ardhi na biashara za wananchi na kusaidia umilikaji halali wa mali hizo ili zisaidie kuwapatia mikopo katika Mabenki, hili linashughulikiwa vizuri katika utekelezaji na mkakati wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania maarufu kwa neno (MKURABITA).

- (v) Kupanua huduma ya mikopo yenyenye masharti nafuu.
- (vi) Kuendelea kuhimiza matumizi ya mipango shirikishi kwa njia ya kuwashirikisha wananchi katika shughuli za maendeleo. Hili linaenda sambamba na Sera ya CCM ya Madaraka ya wananchi kupitia Halmashauri zao za Wilaya n.k. kama vitovu vya maendeleo na ukuzaji wa demokrasia.
- (vii) Kuendeleza juhudhi za hifadhi ya mazingira na kuzuia kwa nguvu zaidi uharibifu wa mazingira ili tuwe na mazingira endelevu na hili Makamu wa Rais juzi amesema vizuri.
- (viii) Kutilia mkazo dhima ya kila kaya kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Serikali itaendeleza mkazo katika kutoa huduma bora za elimu, afya, maji safi na salama, pamoja na kuendeleza kasi ya mapambano dhidi ya Ukimwi ili kupata ufanisi mkubwa zaidi katika vita yetu dhidi ya umaskini. Hali kadhalika, Serikali itaendelea kuzingatia utawala bora na wa sheria kwa kuongeza mapambano ya vitendo dhidi ya rushwa na ujambazi mionganini mwa jamii yetu.

MHE. EZIKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, hasa jamii wa wafugaji wamejikuta ni maskini zaidi kutokana na janga la asili la ukame kwamba mifugo yao wamelazimika kuiuza kwa bei ya kutupa na mingine imekufa na mifugo hii ndiyo imekuwa ikitumika kama nyenzo muhimu kwa kilimo kwa hiyo, hawawezi kulima. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuwasaidia wananchi hawa kuwawezesha ili waweze kurudi kwenye hali ya umaskini walau waliyokuwa nayo kabla ya janga hili kutokea? (*Makofî*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali imekuwa ikihimiza kwamba wale ambao wana mifugo na hawana malisho ya kutosha wauze mifugo hiyo na waweke fedha hizo Benki ili wakati wa shida kama huu zitumike kuwasaidia. Kwa hiyo, tunaendelea kuhimiza hili lifanyike. (*Makofî*)

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ameleezea mikakati na utekezaji wa kuwakwamua wananchi wa Vijijini. Lakini mimi nataka kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Sehemu kubwa ya wananchi wa Vijijini ni wakulima, Mheshimiwa Waziri ametuelezea mikakati na utekelezaji je, kwa kiwango gani anaweza kutuambia atawawezesha wanawake na vijana ili wasiwe wanakimbilia Mijini waweze kuendelea kukaa Vijijini na kuzalisha na kuweza kupata kipato zaidi? (*Makofî*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza mikakati mbalimbali ambayo itawanufaisha wananchi wote bila kubagua. Namna ya kuwawezesha kwa mfano ukipeleka umeme kijijini mtu wa kwanza unayemwezesha kwa kweli ni mama, kwa sababu yeye badala ya

kukoboa mahindi yake kwa mawe, kinu au njia zizingine za kiasili, sasa atakoboa kwa kupitia mashine ambazo zinatumia umeme.

Lakini la pili, tumezungumza kwamba tutaanzisha mfuko wa taifa wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kama sehemu ya ile sheria ya uwezeshaji. Mfuko huo pia utahudumia wananchi wote pamoja na wanawake.

Lakini vile vile tuna mfuko maalum kwa ajili ya wanawake wa Shilingi milioni 500 shabaha yetu mbele ya safari mfuko huu tutautunisha zaidi ili uweze kuhudumia wanawake wengi zaidi na hasa Vijijini. (*Makofi*)

Na. 81

Miradi ya Maji

MHE. JACOB D. SHIBILITI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafahamu matatizo ya maji nchini na imekuwa na juhudzi ya kutatua matatizo ya maji kwa kutafuta wafadhili na pia pesa za hapa nchini na kwa kuwa Miji ya Misungwi, Musoma Mjini na Bukoba Mjini, ni katika ya miji iliyofanyiwa upembuzi yakinifu ili iweze kupata maji toka Ziwa Victoria ukizingatia Miji hii iko karibu na ziwa hilo:-

- (a) Je, upembuzi huo uko katika hatua gani?
- (b) Je, ni Shilingi ngapi miradi hiyo itagharimu na ni nani atafadhili?
- (c) Je, ujenzi wa miradi hiyo utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia shirika lake la maendeleo la *AFD* iligharamia mradi wa upembuzi yakinifu wa majisafi na majitaka kwa Miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi. Mradi huu uligharimu Shilingi milioni 226.1 sawa na (*Euro 166,160*) na ulikamilika Desemba 2004. Upembuzi yakinifu huo uliainisha hatua zifuatazo ambazo zinatakiwa zichukuliwe ili kuboresha huduma ya maji kwenye miji husika:-

(i) Ujenzi wa vyanzo vipyta vya maji kwenye Ziwa Victoria kwa ajili ya miji yote mitatu. Aidha kwa Mji wa Bukoba vyanzo mbadala vya chemichemi na mito vitaendelezwa pia.

(ii) Ujenzi wa mitambo ya kusafisha na kusukuma maji.

(iii) Ukarabati na upanuzi wa mifumo ya mabomba ya usambazaji majisafi.

(iv) Ujenzi wa mifumo ya uondoaji majitaka.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hatua hizo mradi uliopendekezwa utakaogharimu jumla ya Shilingi bilioni 95.5 ikiwa Bukoba Shilingi bilioni 31.7, Musoma Shilingi bilioni 48.8 na Misungwi Shilingi bilioni 15.0, utatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusu utekelezaji wa hatua za muda mfupi, usanifu wa mifumo ya majisafi na majitaka, utayarishaji wa vitabu vya zabuni, ukarabati na kuanza ujenzi wa mifumo mipya ya majisafi. Awamu ya pili itahusu kukamilisha ujenzi wa mifumo mipya ya majisafi na uondoaji majitaka.

SPIKA: Tunaendelea, ooh! Kama mnavyojuu Spika ana mambo ya kasi hapana kwenda taratibu

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, Mfadhili aliyegharama upembuzi yakinifu kwa sasa ana uwezo wa kugharimia utekelezaji wa hatua za muda mfupi tu katika miji ya Bukoba, Musoma na Misungwi kwa kiwango cha shilingi bilioni 9.6. Hivyo Wizara inaendelea kutafuta fedha za kugharamia hatua zilizobaki ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wafadhili wengine wakiwemo Shirika la Maendeleo la Ujerumani, Benki ya Uwezeshaji wa Nchi za Ulaya na Benki ya Dunia.

(c) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa hatua ya muda mfupi ambazo zitahusu ukarabati wa vyanzo vya maji vilivyopo, mifumo ya usambazaji majisafi na matanki ya kuhifadhia maji utaanza mwaka 2006/2007. Aidha sambamba na utekelezaji wa kazi hizo, usanifu na utayarishaji wa vitabu vya zabuni kwa ajili ya mradi wa upeo wa muda mrefu utafanyika.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa wafadhili wameweza kuonyesha upembuzi yakinifu wa Shilingi bilioni 15 kwa Misungwi je, iwapo kutakuwa na matatizo kwa wafadhili hao Serikali yetu iko tayari kutoa fedha zake za ndani ili kukamilisha mradi huo? (*Makofit*)

(b) Kwa vile wananchi wa Misungwi wamekuwa na matatizo makubwa sana hasa mwaka huu hususan akina mama na baada ya Bwawa la Misungwi kukauka je, katika bajeti ijayo Serikali iko tayari kutenga fedha ili kukarabati bwawa hili ili wananchi wa Misungwi waweze kupata maji mengi? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili yenye sehemu (a) na (b) ya Mheshimiwa Jacob Shibiliti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu jibu la msingi nimesema ya kwamba Serikali inaongea na wafadhili ambao wako watatu kwa ajili ya fedha zilizobakia. Nina

imani na nina uhakika kabisa kwamba fedha hizo zitapatikana kwani dalili siyo mbaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jibu la pili ni kweli kwamba naungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Bwawa la Misungwi, linakauka wakati wa kiangazi. Hali kadhalika Misungwi wana visima vifupi 16 na ambavyo pia maji yake siyo ya uhakika.

Lakini hapo hapo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika mradi wa Ziwa Victoria unaokwenda Shinyanga na Kahama ni kwamba Vijiji vyake vya Misungwi vingi vitapitiwa na mradi huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunaokoa muda Vijiji hivyo tunavifahamu na ninamwomba Mheshimiwa Mbunge baadaye aje nitampatia Vijiji vyote hivyo viko zaidi ya 20. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. TEDDY LOUSE KASELLA - BANTU: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi wa maji ya kutoka Ziwa Victoria, unafika Kahama kama mji na vile vile unafika Nzega na kwa kuwa jimbo la Bukene liko katikati ya Miji ya Kahama na Nzega na liko karibu zaidi na Kahama.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaonaje kwamba mradi huu uwanufaishe watu wa Bukene vile vile katika kata ya Igusule, Mwamala, Itobo au ipitie Sigiri, Mwangoye, Kasela na Itobo kwenda Nzega? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, mradi wa Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama, unapitia Vijiji vingi, jumla ya Vijiji 54 vitanufaika katika mradi huo.

Vijiji hivyo majina tunayo ningemwomba Mheshimiwa Teddy, aje tuangalie pamoa vile Vijiji kama Vijiji alivyovitaja na vyenyewe vimo humo. Lakini hata hivyo ni kwamba mradi huu baadaye ukishamalizika kutakuwa na mipango mingine ya kuangalia Vijiji vingine vitakavyonufaika ikiwa fedha zitaruhusu. Ahsante. (*Makofî*)

Na. 82

Chanzo cha Mto Ruaha Mdogo

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI aliuliza:-

Kwa kuwa Mto Ruaha Mkubwa hukauka wakati wa kiangazi na kuathiri sana upatikanaji wa umeme na kwa kuwa, mto Ruaha Mdogo unachangia kwa kiasi kikubwa maji yanayoendelea kuingia kwenye Bwawa la Mtera wakati wa kiangazi.

Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kutenga eneo la misitu ya Mufindi/Iringa ambalo ndicho chanzo cha Mto Ruaha mdogo na kulihifadhi kama *Ramsar Site*.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalí la Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo kwa kuanza na maelezo yafuatayo:-

Bwawa la Mtera, lina uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo milioni 3,200 na kiasi cha maji yanayoingia kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo milioni 3,650 kutoka katika mito mikuu mitatu ambayo ni Mto Ruaha Mkúu, unaochangia asilimia 56, Mto Ruaha Mdogo unaochangia asilimia 18 na Mto Kisigo unaochangia asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, Mto Kisigo hukauka kwa miezi minne hadi mitano wakati wa kiangazi ambapo ni Juni na Novemba. Kuanzia mwaka 1994 Mto Ruaha Mkúu umekuwa unakauka kwa mwezi mmoja hadi miezi mitatu wakati wa kiangazi.

Kabla ya mwaka 1994 Mto Ruaha Mkúu ulikuwa haukauki kabisa, ingawaje mtiririko wa maji wakati wa kiangazi unakuwa mdogo, kati ya meta za ujazo 0.5 hadi 3 kwa sekunde. Mto Ruaha mdogo haukauki kabisa na una mtiririko wa meta za ujazo 3 na 5 kwa sekunde wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, wastani wa asilimia 86 ya maji kutoka mito hiyo mitatu huingia Bwawa Mtera miezi ya Desemba hadi Mei na asilimia 14 huingia wakati wa kiangazi miezi ya Juni hadi Novemba.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha Ruaha Mdogo ni *permanent swamps* za Mufindi zenye eneo la kilomita za mraba 30 hadi 50. Eneo hili linaungana na eneo jingine lenye misitu ya *pines* ya *Sao Hill* ambayo sasa linavunwa na pia na mashamba ya chai makubwa yako katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Takwimu zinaonyesha kuwa mchango wa maji kutoka maeneo hayo ni asilimia 4 tu ya ujazo wa Bwawa la Mtera. Wakati wa miezi minne ya kiangazi Ruaha Ndogo huchangia asilimia 0.4 ya ujazo wa Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swalí la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchango wa maji katika Bwawa la Mtera, kutoka misitu ya *Sao Hill*, katika miezi ya kiangazi ni asilimia 0.4 na kwa kuwa haibainiki kuwa kutenga eneo la misitu ya *Sao Hill* na Mufindi kuwa *Ramsar Site* itabadilisha hali ya upatikanaji wa maji katika bwana la Mtera. Hivyo eneo hili halikidhi vigezo vinavyotumika kuanzisha *Ramsar Sites*.

Kwa hiyo, Serikali haioni umuhimu wa kutenga eneo hili kuwa *Ramsar Site* kwa kigezo cha upatikanaji wa maji kwa ajili ya Mtera peke yake. (*Makofi*)

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya kitaalam yaliyotolewa na Naibu Waziri. Nina swalí moja la nyongeza.

Nilipouliza swali hili nia haikuwa tu kuhifadhi maji ambayo ingekuwa *Ramsar Site* kwa ajili ya kutoa maji Mtera peke yake. Suala la *Ramsar Site* ni la kimataifa. Sisi Watanzania tunatakiwa ku-establish kuanzisha *Ramsar Sites* ambazo ni za aina tatu. Mojawapo ni *Ramsar Sites* zinazokuwa kwenye vyanzo vya maji au milimani *up land, wet lands* au *Ramsar Sites*.

Kwa vile Mheshimiwa Waziri wa Mazingira yupo ataungana na mimi kwamba kwa kweli eneo lile sasa hivi linaingiliwa sana na kilimo cha mahindi, ukiacha kilimo cha chai, lakini vile vile linaingiliwa na kilimo cha vinyungu kwa wananchi wanaotoka Wilaya za Kilolo, Iringa Vijiji na kadhalika na maji yale yasipoangaliwa yatakauka. Je, Mheshimiwa Waziri haoni ni vyema kuliangalia kwa undani zaidi kuhakikisha kwamba bado eneo hilo linahifadhiwa? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:
Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya swali la msingi kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Sheria Na. 20 ya mwaka 2004, Sheria ya Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira imeainisha jinsi ya kuanzisha na usimamizi wa maeneo ya ardhi oevu ambayo kimataifa inajulikana kama *Ramsar Sites*.

Sasa ni kweli kwamba maji kuingia Mtera haiwezi kuwa ni kigezo cha kuifanya *Samsar Site*, lakini tunaweza kuangalia vigezo vingine zaidi ili kuona kama tunaweza kuliangalia eneo hilo na kulitamka kama *Ramsar Site* kama taratibu za kimataifa zinavyotaka. Ahsante. (*Makofit*)

Na. 83

Kupanda kwa Bei ya Mafuta

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya mafuta ya petroli inazidi kupanda na kuwa Serikali iliwahi kutoa ahadi kuwa gesi ya asili ya Songo Songo itatumika kama mafuta ya magari na kama nishati ya kupikia na kwa kuwa gesi ya asili inazidi kupatikana kwa kiwango kikubwa pamoja na ile ya *Mnazi Bay*:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia gesi asilia kama mafuta ya magari pamoja na matumizi mengine?

(b) Je, kwa nini Serikali isihimize matumizi ya gesi hiyo kwa ajili ya Nishati ya kupikia badala ya kuruhusu uvunaji wa misitu kwa ajili ya kutengeneza mkaa wa kupikia hali ambayo imeleta ukame mkubwa hapa nchini?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha gesi hiyo kutumika kwenye viwanda vidogo kama vile vya kutengeneza vifaa vya plastiki na kadhalika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *TPDC* ilianza tathmini ya matumizi mbalimbali ya gesi asilia tangu miaka ya 1980 na 1990. tathmini hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kuzalisha kemikali/mbolea.
- Kuzalisha umeme.
- Kutumika kama nishati viwandani.
- Kutumika kama nishati ya kuendeshea magari badala ya mafuta na dizeli.

Kwa matumizi ya gesi kwenye magari badala ya petroli na dizeli, tathmini ilifanyika 1996. Tathmini hiyo ilikuwa ni pamoja na kupeleka ujumbe wa watalamu kutembelea nchi kama Malasyia ambayo kwa wakati huo ilikuwa kati ya nchi iliyopiga hatua kubwa katika teknolojia ya kutumia gesi iliyosindikwa (*compressed natural gas*) kwenye magari.

Haya yalikuwa ni matayarisho tu kwani uendelezaji wa gesi ya Songo Songo ulikuwa bado. Baada ya mradi wa Songo Songo wa kufikisha gesi asilia Dar es Salaam kukamilika mwaka 2004, *TPDC* kwa kushirikiana na mbia wake *Pan African Energy Tanzania Ltd*, wamechukua hatua za kuutekeleza mradi huo.

Mwaka 2004 ziliitishwa tenda za kumtafuta mwekezaji wa kuzalisha gesi iliosindikwa pamoja na kuweka mtandao wa kuiuzwa na Makampuni mawili yalijitokeza. Tenda hiyo haikuweza kukubalika kwa sababu ya masharti yaliyowekwa na mwekezaji mtarajiwa kwamba apewe ukiritimba yaani Kampuni nyingine zisihusike katika usambazaji wa gesi hiyo. Tenda za pili ziliitishwa mwezi Mei, 2005 na kufunguliwa Julai, 2005.

Ni Kampuni moja tu ilijitokeza ambayo nayo bado haijaleta mpango wa uwekezaji. Kwa sasa Serikali inaangalia uwezekano wa kushirikiana na Kampuni za Kichina. Nchi ya China imepiga hatua kubwa sana katika teknolojia hiyo. Na Ujumbe wa *TPDC* ulitembelea China Novemba 2005. (*Makofit*)

Hali kadhalika Serikali ya China imekubali kugharimia ujumbe mwingine mwezi Mei 2006 wa kujifunza kuhusu teknolojia na sera za China zilizowezesha mafanikio makubwa katika utumiaji wa gesi asilimia, sio tu kwenye magari, lakini pia utumiaji wa gesi asilia kwa ajili ya kupikia majumbani na kwenye Taasisi. Kwa sasa hivi *TPDC* inaendelea na tathmini ya matumizi ya esi asilia kwenye magari na majumbani Taasisi na viwanda hapa DSM, sehemu za Chuo Kikuu, Sinza na Mikocheni. Tathmini kama hiyo kwa viwanda na magari pia inafanyika Mjini Morogoro.

Ni mategemeo ya Serikali kuwa utekelezaji wa mradi huo, hasa kwa kushirikiana na wawekezaji wa China utaanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inawasiliana na Wizara ya Fedha ili kuweka vivutio kwa wawekezaji na watumiaji hasa kutokana na gharama kubwa za usambazaji wa gesi asilia. Sera nzuri na vivutio vitaiwezesha Serikali kuhimiza kwa ufanisi matumizi ya gesi asilia kwenye magari na kwa ajili ya kupikia na kuokoa fedha za kigeni kuagiza mafuta na vile vile kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Vile vile Wizara inakusudia kuleta hapa Bungeni Sheria ya Usimamizi wa masuala ya gesi.

(c) Mheshimiwa Spika, gesi asilia kama nishati, imekwishaanza kutumika viwandani. Mpaka sasa viwanda 10 vimeunganishwa kwenye mtandao wa usambazaji gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam na vinatumia gesi hiyo badala ya mafuta.

Viwanda vingine 21 vimo mbioni kuunganishwa katika mtandao wa gesi baada ya mipango ya upanuzi wa mtandao wa bomba la gesi kukamilika. Matumizi haya pamoja na yale ya kwenye umeme yanapunguza matumizi ya fedha za kigeni kiasi cha *US\$ 151.2* milioni kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, gesi asilia kama malighafi ya kuzalisha vitu vingine kama kemikali, mbolea, plastiki na kadhalika, bado haijaweza kutumika, kwani miradi kama hiyo ni mikubwa na inahitaji kiasi kikubwa cha gesi asilia. Endapo hazina ya gesi (*gas reserves*) zitaendelea kugunduliwa na kuthibitishwa kuwa zinatosheleza miradi mikubwa kama hiyo, basi miradi hiyo itaendelezwa.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutupa majibu ambayo yamepanua sana uwelewa wetu wa namna ya kutumia gesi hii. Kwa kuwa gesi hii ya *Mnazi Bay* ambayo itatumika zaidi katika kutengeneza nishati ya umeme kwa ajili ya Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi.

Je, Serikali inaweza kusema mradi huu hasa hasa utakamilika lini na hasa lini utafika Masasi?

Pili, katika matumizi bora ya nishati hii na hasa kwa sababu itasambazwa sehemu nyingi vijijini kutoka sehemu za Mtwara mpaka Masasi kupitia Mingoyo. Je, vijiji vilivyopo katika eneo hilo yaani vijiji vya Mkwera, Nanganga, Mumburu, Nangoo, Liputo na Ndanda vitafaidika namna gani itakapopatikana hiyo nishati?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu iko katika majadiliano na Kampuni ya *ATNAT* katika mpango mahusus wa kipeleka umeme Masasi na Mtwara. Tukifanikiwa kukamilisha majadiliano na Kampuni ya *ATNAT* kuhusu mradi huu mara baada ya hapo utekelezaji utanza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa mradi huu kuna *line* aina mbili za umeme ambazo zitapelekwa. Kati ya Mtwara hadi Mingoyo itapalekwa *line* ya kilovoti 132, kati ya Mingoyo na Ndanda itapalekwa *line* kilovoti 33. Ilivyo kawaida pale ambapo kuna *line* ya kilovoti 132 haitawezekana kwa haraka kipeleka umeme katika vijiji katika eneo

hilo mpaka pale ambapo *Sub-Station* itakapojengwa katika eneo hilo. Lakini katika vijiji vyote ambavyo viko kati ya Mingoyo na Ndanda pale ambapo kutakuwa na *line* ya kilovoti 33 pale fedha itakapopatikana itawafikishia umeme. (*Makofi*)

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba gesi ni moja katika masuala ya Muungano na kwa sababu Zanzibar kuna matatizo ya umeme. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gesi Zanzibar ili kusaidia umeme pamoja na shughuli za viwandani? Ahsante sana.

SPIKA: Linaonekana kama ni jipya. Lakini naona Mheshimiwa Waziri amesimama kulijibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza Zanzibar hakuna matatizo ya upatikanaji umeme kwa hivi sasa. Umeme unaopelekwa Zanzibar ni kama megawati 36 na *TANESCO* wanawauzia umeme Zanzibar, kama yapo yatakuwa ni matatizo ya usambazaji ndani ambayo Wizara yangu ya Serikali ya Muungano kwa kweli haihusiki. Lakini kadri tunavyojua ni kwamba umeme unapelekwa Zanzibar kwa kiwango hicho pamoja na kwamba sisi tuna mgao huku lakini Zanzibar wanapata megawati wanazozihitaji za umeme. (*Makofi*)

Na kwa maana hiyo, suala la matatizo ya usambazaji au upatikanaji umeme Zanzibar halipo. Lakini napenda niongeze pia kutokana na kutambua umuhimu wa umeme kwa maendeleo ya Tanzania kama nchi nzima ikiwemo Zanzibar, hivi karibuni tu Mheshimiwa Waziri wa Nishati Zanzibar alikutana nami na kukubaliana juu ya umuhimu wa *TANESCO* kupeleka umeme Pemba pale watakapokuwa wamepata mradi wa kufikishia umeme Pemba. (*Makofi*)

Na. 84

Uchimbaji wa Madini ya Vito Korogwe

MHE. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa katika maeneo mengi ya tambarare na milima yanayoizunguka Wilaya ya Korogwe kuna hazina kubwa ya madini ya vito ambayo hayapatikanikatika maeneo mengi nchini na kwa kuwa uchimbaji wa madini hayo katika maeneo hayo hufanyika kienyeji na hivyo kusababisha athari mbalimbali za mazingira:-

Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati muafaka sasa wa kuwakusanya na kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Kalalani/Kigwasi ili wachimbe katika njia bora zaidi badala ya uchafuzi wa mazingira unaofanywa hivi sasa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, napenda nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo mengi ya Wilaya ya Korogwe yanayo hazina kubwa ya madini hususan yale ya vito, hasa *sapphire, ruby, garnets, tourmaline, zircon na acquamarine*.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini Na. 5 ya mwaka 1998 na Kanuni zake za mwaka 1999 zimeweka bayana taratibu za hifadhi ya mazingira kwa wachimbaji wakubwa pamoja na wadogo. Uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo ya Kalalani na Kigwasi umekuwa ukisababishwa kwa kiasi kikubwa na wachimbaji wadogo wasio na leseni za uchimbaji ambao wamekuwa wakivamia maeneo mbalimbali na kuchimba madini bila kuzingatia Sheria na Kanuni za nchi. Wavamizi hawa wameingia hata ndani ya maeneo yenye leseni halali za wachimbaji wadogo pamoja na wakubwa. Eneo la Kalalani/Kigwasi lina wachimbaji wadogo wenye hati miliki halali za kuchimbia madini, yaani *Primary Mining License* zaidi ya 170.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuwakusanya na kuwawezesha wachimbaji hawa wa Kalalani/Kigwasi ili wachimbe vito kwa njia bora zaidi. Njia mojawapo ya kutekeleza hili ni Wizara yangu tukishirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wachimbaji hawa wadogo popote walipo kuanzisha ushirika au *SACCOS* zao, ili iwe rahisi kukopesheka na vyombo vyya fedha na iwe rahisi kwa Wataalam wa Wizara yangu kuwapa mafunzo ya pamoja ya namna ya kuchimba madini kwa tija. Sera ya Madini ya mwaka 1997 inahimiza wachimbaji wadogo kuanzisha ushirika au vikundi vidogo vidogo kwa lengo hilo hilo, kwa kuwa itakuwa rahisi kupata misaada wakiwa kama Taasisi.

Kwa eneo la Kalalani/Kigwasi, kama nilivyosema awali wapo wachimbaji waodgo wenye hati halali zaidi ya 170, kwa hiyo kazi ya kuwahamasisha inaweza kuwa rahisi, na tunamwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane naye katika kutekeleza uhamasishaji wa kuwawezesha wachimbaji hawa kuanzisha chombo chao cha kuwawezesha kupata mikopo au mafunzo kwa pamoja.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa kuna wanawake wachimbaji wadogo wadogo walioko kama wa Muheza wa Mgusu na Nyarugusu. Je, Serikali sasa haioni haja kutenga fungu la kuwasaidia akina mama hawa ili wajiwzeshe katika kuchimba madini hayo? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini inaona umuhimu wa kuwawezesha akina mama, vijana, wachimbaji wote wadogo wadogo ndani ya nchi yetu Tanzania na kutokana na hivyo, Wizara ya Nishati na Madini imeshaandaa mipango ili kuhakikisha kwamba wachimbaji wote wadogo wadogo wanafaidika na rasilimali tuliyonayo hapa nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ameshaunda Kamati chini ya Uwenyekiti wa Mwenyekiti Mtendaji wa *STAMICO* ambayo imeanza kazi yake tarehe 10 Machi, 2006 na hiyo Kamati imeundwa rasmi ili kuunda mikakati ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo Tanzania nzima. Ahsante. (*Makofî*)

Na. 85

Mjusi aina ya Dinasoria

MHE. FATUMA A. MIKIDADI aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha miaka iliyopita katika ya Wilaya ya Lindi Vijijini, kulikuwa na mjusi mkubwa aina ya Dinasoria ambaye baadaye alitoweka na mwingine ikakutwa skeletoni yake ambayo ukubwa wake ni sawa na nyumba, skeletoni hiyo ilichukuliwa na Wajerumani na kuiweka katika jengo lao la Makumbusho ya Sanaa hadi leo hii:-

- (a) Je, Serikali ya Tanzania inafaidika vipi kutokana na skeletoni ya mjusi kuwapo huko aliko?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa sasa wakati muafaka kufanya makubaliano na Ujerumanî ili kurudisha skeletoni ya mjusi huyo hapa nchini ili nasi tujipatî fedha za kuinua uchumi wetu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali haifaidiki kimapato au kifedha kutokana na skeletoni ya mjusi huyo aliyeko Ujerumanî. Fedha iliyopo ni kwamba masalia hayo yamehifadhiwa kitaalamu na katika mazingira salama kisayansi na hivyo kuwzesha masalia hayo kuendelea kuwepo kwa muda mrefu bila kuharibika. Aidha, jina la Tanzania linatangazwa kwa kuwa masalia hayo yanaonyesha kuwa yamegunduliwa nchini Tanzania. Kufahamika huku kwa nchi yetu duniani kuna sababisha nchi ijulikane na ipate watafiti wengi kutoka nchi mbalimbali duniani kuja kufanya utafiti wa urithi wa utamaduni pamoja na kuvutia watalii.
- (b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kurejesha masalio au vifaa vya utamaduni kutoka nje ya nchi moja kwenda nchi husika, umefafanوليwa na mkataba wa *UNESCO*

wa mwaka 1970. Mkataba huo, pamoja na mambo mengine unaelekeza nchi mwanachama kuweka sheria zinazozua kumiliki masalio ya kitamaduni ambayo yanaingizwa bila vibali stahili kutoka nchi nyingine na pia kuzuia uingizaji wa masalio ya kiutamaduni yaliyoibowi au kuporwa kutoka nchi nyingine. Aidha, mkataba huo unaelekeza nchi mwanachama kurejesha masalio ya utamaduni ambayo yapo nchini mwao ambayo yatakuwa yameingizwa baada ya mkataba huu kupitishwa kama nchi inayoomba itatekeleza masharti yafuatavyo. Masharti yenye ni kama ifuatavyo:-

- Kugharamia usafiri na usafirishaji wa masalio hayo;
- Kugharamia utunzaji na uhifadhi wa masalio hayo kwa kipindi chote cha kuwepo masalio hayo katika nchi husika;
- Kuwepo na mazingira sahihi kitaalamu ili masalio hayo yasiharibike yawapo hapo nchini; na
- Vile vile kuwepo na utaalamu sahihi katika kutunza na kuhifadhi masalio hayo.

Mheshimiwa Spika, kutohana na maelezo hayo na kwa kutumia mkataba huo ambao Tanzania imeridhia Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba huu ni wakati muafaka kuanza mchakato wa urejeshwaji wa masalio hayo kwa mujibu wa maelekezo ya mkataba huo. (*Makofi*)

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mhusi huyu ni mgeni machoni pa watu wengi, hata mimi mwenyewe sijamwona. Ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri atuelezee alivyo livyo akizingatia uzito wake, urefu wake, na upana wake. La kwanza. (*Kicheko*)

La pili, kwa kuwa kuna uwezekano wa kurejeshwa mhusi huyu wa kihistoria nchini Tanzania kwa nini asirejeshwe Mkoani Lindi, Wilayani Lindi Vijijini kwa sababu ana historia ya Mkoa wa Lindi, ana utamaduni wa Mkoa wa Lindi na ana asili ya Mkoa wa Lindi? Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mimi nadhani tusubiri jitihada za kumrudisha mhusi zizae matunda, hapo ndiyo tutajua lihifadhiwe wapi au tani ngapi. (*Kicheko*)

Na. 86

Ongezeko la Mamba katika Ziwa Rukwa

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la mamba upande wa Kusini mwa Ziwa Rukwa na kwa kuwa, tishio kubwa kwa maisha ya wananchi wanaoishi na kutegemea ziwa hilo kwa kupata mafao ya rasilimali itokanayo na ziwa hilo:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza mamba hao?
- (b) Je, Serikali inaweza kuruhusu mamba hao wakawindwa na kutumika kama kitoweo hasa kwa kuwa hivi sasa yapo baadhi ya makabila hapa nchini wanakula nyama yake?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILII NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Sigonda, Mbunge wa Songwe lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwinda mamba waharibifu ili kuwaondolea wananchi kero zinazosababishwa na wanyama hao. Aidha, vibali vyaa uwindaji wa mamba hutolewa kila mwaka kwenye maeneo yaliyotolewa taarifa ya kuwa na matukio ya uharibifu huo. Hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Ziwa Rukwa ni mionganoni mwa maeneo ambayo tayari yamekwishatolewa taarifa ya kua na matukio ya uharibifu wa mamba.

Mwaka 2005 Wizara yangu iliruhusu kampuni ya *Mwasi Multi-business Enterprises Co.* ya Sumbawanga kuwinda mambo 62 katika Ziwa Rukwa na Mto Mombo. Hata hivyo kampuni hii haikuweza kutekeleza lengo la kuwinda katika Ziwa Rukwa kama ilivyopangwa. Kutokana na hayo mwaka 2006 Wizara yangu imepanga kutoa leseni kwa kampuni mbili kuwinda mamba 145 katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wanyamaporini ya mwaka 1974 hairuhusu mamba kuwindwa kwa ajili ya kitoweo, hivyo hakuna leseni inayotolewa kwa madhumuni hayo. Hata hivyo, Sheria hii inaruhusu wananchi kutumia nyama itokanayo na wanyama wanaouawa, ikiwa ni pamoja na mamba, chini ya mpango wa kudhibiti wanyama waharibifu.

Aidha, Wizara yangu inatambua kwamba yapo makabila yenyeye desturi ya kula aina fulani ya wanyama ambayo pengine makabila mengine hawatumii. Kwa kuzingatia haya, Wizara yangu haina kipingamizi kwa wananchi watakaoamua kutumia nyama ya mamba watakaowindwa chini ya mpango wa kudhibiti wanyama waharibifu kwa ajili ya kitoweo, kama mila na desturi zao zinaruhusu hivyo, ili mradi wafuate sheria na taratibu zilizopo.

Na. 87

Uendelezwaji wa Wakulima wa Kisasa

MHE. JUMA H. KILLIMBAH aliuliza:-

Kwa kuwa Serikai Awamu ya Nne imeelezwa bayana juu ya dhamira yake kuhusu kumwendeleza mkulima kwa kilimo cha kisasa kwa msingi wa uchumi wa kisasa

na kwa kuwa, mwaka huu 2005/2006 nchi yetu haijapata mvua za kutosha ili kukidhi kilimo:-

- (a) Je, Serikai ina mpango gani madhubuti wa kuokoa wananchi katika janga la njaa linalowakabili kwa kuwa ni dhahiri kuwa Watanzania walio wengi wanategemea kilimo?
- (b) Je, ni maandalizi gani yameandaliwa hasa juu ya upatikanani wa mbegu bora na mbolea za kisasa kwa ajili ya mazao ya muda mfupi bila urasimu ili pindi mvua za msimu 2006/2007 zitakapoanza wakulima waanze kilimo?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa harubu juu ya matumizi ya jembe la mkono hasa kwa wanawake walioko vijijini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatia hali ya ukame iliyoyakumba maeneo mengi nchini katika msimu wa 2005/2006 na kusababisha upungufu mkubwa wa chakula, Serikali imekwishachukua na kutekeleza hatua za kukabiliana na janga la njaa linalowakabili wananchi kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na tathmini iliyofanyika mwezi Agosti/Septemba, 2005 na Novemba 2005 Serikali imetoa tani 21,499 za mahindi ya kuuzwa kwa bei nafuu ya sh.50 kwa kilo kwa watu 613,405 waliobainika kuwa na upungufu wa chakula kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Novemba, 2005 hadi Januari 2006.

Aidha, kutokana na tathmini nyingine iliyofanyika mwezi wa Januari na Februari, 2006 jumla ya tani 56,774 za mahindi zimetolewa kwa ajili ya maeneo yaliyobainishwa yana upungufu wa chakula kwa kipindi cha miezi miwili ya kuanzia Machi hadi Aprili, 2006.

(ii) Baada ya kuainishwa na tathmini ya Januari/Februari 2006 kuwa akiba ya chakula iliyopo katika maghala ya Serikali haitoshi kukidhi mahitaji ya chakula kwa watu walioathirika na upungufu wa chakula hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2006 Serikali imenunua tani 42,000 za mahindi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuziba pengo lililojitekeza.

Aidha, Serikali imeomba wahisani kutoa jumla ya tani 100,000 za mahindi ambapo Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*WFP*) wameombwa kuratibu upatikanaji wa msaada huo.

(iii) Ili kuepusha upandaji holela wa bei za vyakula, Serikali iliondoa ushuru kwa kuingiza mahindi kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi mitatu kutoka Januari hadi Aprili, 2006 ili kuwahamasisha wafanyabiashara kuagiza mahindi kwa wingi kwa ajili ya kuwauzua wananchi wenye uwezo wa kununua chakula.

Aidha, Serikali imepunguza ushuru kwa kuingiza mchele kutoka nje ya nchi kutoka kiwango cha asilimia 75 hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Machi, 2006.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mbegu bora zinawafikia wakulima kwa wakati uliopangwa. Wizara imeendelea kuzalisha mbegu bora kupitia katika mashamba yake ya mbegu yaliyopo Arusha, Kilangali, Msimba (Morogoro), Dabaga (Iringa) na Mwele (Tanga). Katika msimu wa 2005/2006, jumla ya hekta 1,000 zimelimwa na zinategemewa kuzalisha jumla ya tani 1,500 za mbegu za mazao mbalimbali. Kati ya hizo, tani 373.5 zitakuwa ni mbegu bora za mahindi, tani 103.5 za mtama na tani 393 za mikunde. Serikali pia imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha na kuagiza mbegu bora za mazao na kuzisambaza katika maeneo ya kilimo ili wakulima wazinunue.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mbolea Wizara imeandaa mkakati wa kuzifikisha mbolea mapema kwa wakulima kwa kuhusisha sekta binafsi, wafanya biashara na Halmashauri za Wilaya. Mkakati huo unaainisha majukumu ya Wizara na Halmashauri za Wilaya katika kusimamia usambazaji wa mbolea itakayosambazwa chini ya utaratibu wa ruzuku ili kuongeza ufanisi na kuondoa mapungufu yaliyojitekeza katika misimu iliyopita. Wizara hivi sasa inakamilisha kuandaa taratibu muhimu za ununuzi na usambazaji wa aina zote za mbolea zitakazohitajika katika msimu wa 2006/2007.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mipango na mikakati yenyе lengo la kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo ikiwa ni pamoja na matumizi ya matrekta na wanyamakazi kuondoa harubu ya matumizi ya jembe la mkono. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya maonesho na mafunzo ya matumizi ya zana za kilimo zinazokokotwa na wanyama. Wizara inashirikiana na Halmashauri za Wilaya kuwahamasisha wakulima kuibua miradi itakayowawezesha kuendeleza matumizi ya wanyamakazi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Pembejeo inaendelea kutoa mikopo yenyе masharti nafuu kwa wakulima ili waweze kukarabati matrekta mabovu na kununua matrekta mapya na zana zake.

Wizara vile vile inahamasisha sekta binafsi kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta kwa kutoa mikopo yenyе masharti nafuu kwa ajili ya kununua matrekta na zana zake ili hatimaye wakulima wengi wasio na uwezo wa kununua matrekta waweze kuyakodisha kulimia mashamba yao. Aidha utaratibu wa kutumia Vyama vya Akiba na Mikopo *SACCOS* ambao umeanza kuwawezesha baadhi ya wakulima nchini kutumia matrekta kwa kukodishiwa na *SACCOS* zao unahimizwa na Serikali.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda wetu wa kuanza maswali ulichukuliwa na matangazo na pia Hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee, naongeza dakika kadhaa, lakini siyo nyingi sana tukizingatia umuhimu wa Maswali na Majibu. (*Makofii*)

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda pia nishukuru Serikali kwa juhudhi zake ilizozifanya kwa kuweza kutoa chakula cha msaada hasa kwa wananchi wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi, ila nina swali dogo la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa, jimbo langu la uchaguzi hali ya mazingira yake ni kame na hasa ukiangalia mkoaa mzima wa Singida inategemea sana mvua za kubahatisha. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri hasa kupitia Wizara yake anawashauri nini wananchi wa jimbo langu walime zao gani ambalo linaweza likahimili ukame na ili hapo panapojitokeza uhaba wa mvua hilo zao hilo liweze kuwaokoa wananchi na tatizo la njaa.

(b) Je, Serikali kupitia Wizara inasema nini kuhusiana na miradi hasa ya *PADEM* hii miradi ya umwagiliaji ambayo sasa inaonekana kwamba ipo jimboni kwangu lakini ipo kwa namna ya kinadharia?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la wilaya ya Iramba pamoja na maeneo yote ni kanda ya kati ni ya ukame na kwa hiyo Serikali inashauri tu kwamba wakulima katika maeneo hayo yote wajitahidi kulima mazao yanastamili ukame, yakiwemo mazao ya mtama mfupi kwa jina la mesia, muhogo na mazao madogo madogo ya kundekunde ambayo yanaweza yakaiva upesi kwa kutumia mvua chache.

Mheshimiwa Spika, la pili juu ya miradi ya umwagiliaji ambayo iko kwenye jimbo lake na haijashughulikiwa kikamilifu ningependa tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa Serikali imekwisha kuandaa mpango mkubwa wa umwagiliaji yaani *Irrigation Master Plan* ambayo itaombewa fedha toka Serikalini na endapo fedha zitapatikana basi na miradi hii iliyoko katika wilaya ya Iramba, itaweza kushughulikiwa.

Na. 88

Mahitaji ya Benki ya Tandahimba

MHE. JUMA A. NJWAYO aliuliza:-

Kwa kuwa taasisi za fedha kama vile benki ni moja ya vitu vinavyochochea kukua kwa uchumi na kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM imetamkwa wazi juu ya kujenga uchumi wa kisasa na imara:-

- (a) Je, Serikali inayo taarifa kuwa Wilaya ya Tandahimba, pamoja na kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa kuitia zao la korosho lakini haina benki?
- (b) Je, Serikali inafahamu kwamba, baadhi ya wananchi wa Wilaya hiyo wamepata kuumizwa na kuibwa fedha zao wakiwa njiani wakipeleka fedha kwenye Benki Newala ambako ni mbali?
- (c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuwapunguzia wananchi wa Tandahimba shida na hatari wanazokutana nazo wakiwa wanapeleka fedha benki Newala?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo taarifa kuwa wilaya ya Tandahimba haina benki pamoja na mchango mkubwa wa kiuchumi unaotolewa na wialaya hiyo.
- (b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina taarifa ya matukio ya wananchi kuibwa au kuumizwa wanapokuwa njiani au kutoka Benki ya Newala. Hata hivyo, matukio kama hayo yanaweza kujitokeza popote hata pale ambapo benki ipo karibu na wananchi.
- (c) Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kifedha nchini yaani *Financial Sector Reforms* unaoteklezwa kuanzia mwaka 1991, ni azma ya Serikali kujitoa katika kuhusika moja kwa moja na biashara ikiwemo biashara ya kibenki. Sera iliyopo ni kuwawezesha wananchi kuanzisha na kusimamia shughuli hizo wao wenyewe. Kwa kuwa wawekezaji wanao uhuru wa kuwekeza katika maeneo wanayochagua, Serikali inafanya jitihada za kuwashamasisha wananchi kuanzisha huduma kama benki hususan pale ambapo wawekezaji wameshindwa kufika.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imekwisha pokea na kukubali maombi ya kuanzishwa kwa benki ya wananchi wa Tandahimba yaani *Tandahimba Community Bank* ikiwa ni mwitikio wa hatua za Serikali za kuweka mazingira na sheria zinazohamasisha jamii na wananchi kujiunga pamoja na kuanzisha benki au taasisi za fedha katika maeneo yao. (*Makofî*)

Na. 89

Msamaha wa Kodi ya Magari kwa Wabunge

MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHANI aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge, Wawakilishi na baadhi ya watumishi wa asasi nyingine kama vile Madaktari wanapata msamaha wa kodi ya magari kwa mujibu wa Sheria za

nchi, lakini jambo la kushangaza ni kwamba msamaha wa kodi wa wawakilishi hautambuliwi Tanzania Bara wakati msamaha wa kodi ya magari kwa Waheshimiwa Wabunge wanatambuliwa huko Tanzania Zanzibar:-

- (a) Je, ni kwa msingi gani msamaha wa kodi ya magari kwa Waheshimiwa Wabunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar hautambuliwi Tanzania Bara?
- (b) Je, kero hii ni ya nini kwa Taifa moja?
- (c) Kwa nini gari zenye namba za usajili Zanzibar haziruhusiwi kutembelea Bara wakati zile za Bara zinaruhusiwa kutembea huko Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Utaratibu unaotoa msamaha wa kodi ya magari kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar hautumiki Tanzania Bara kwa sababu Wawakilishi wanapewa msamaha chini ya utaratibu wa Sheria ya Zanzibar ambayo haitumiki Tanzania Bara na hivyo kupelekea msamaha wa kodi ya magari ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutotambuliwa Tanzania Bara.
- (b) Kimsingi Sheria hii si kero, kwa kuwa Sheria inayotoa msamaha wa kodi ya magari kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar inatumika Zanzibar peke yake, na si kodi ya Muungano.
- (c) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayofanya magari yenye namba za usajili za Zanzibar yasiruhusiwe kutembea Bara ni kutohakana na kuwepo kwa sheria tofauti zinazosimamia usajili wa magari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Hali hii imejitokeza kwa sababu suala la uandikishaji wa magari si suala la Muungano. Hata hivyo, magari hayo yanaweza kuruhusiwa kutembea Tanzania Bara iwapo wenye magari wako tayari kutimiza masharti yaliyo kwenye Sheria ya usajili ya Tanzanuia Bara.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, sasa ni matangazo, taarifa ya kikao Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ushirika, wajumbe wakutane saa tano na nusu asubuhi hii chumba Na. 219. Kamati ya Bunge na Kilimo na Ushirika saa tano na nusu ukumbi Na. 219, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itafanya ziara ya ukumbi mpya wa Bunge leo mara baada ya kipindi cha maswali. Wajumbe ya Kamati ya hesabu za Serikali, wanaombwa kukutana saa tano chumba Na. 428 jengo la utawala.

Wabunge wote mnataarifiwa kwamba nyuma ya jengo la utawala pale ambapo mara nyingine tunaweka viti ama uwanja wa gwaride wa Bunge kuna maonyesho mahususi kwa ajili yetu yanayoendeshwa na taasisi zisizo za kiserikali *Civil Society*

Organizations ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge mkachukua fursa kwa wakati wenu kwenda kuona kinachoendelea hapo kuanzia saa saba, yataendelea kwa siku mbili, leo na kesho. Kamati ya Ulinzi na Usalama itakutana leo kwenye chumba Na. 231 baada ya kipindi cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge jana Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama Mwenyekiti, alisimamia kikao chetu saa sita hadi ilipositishwa Bunge kwa saa zile za asubuhi. Sasa *Presiding Officer* mwagine ni Mheshimiwa Job Ndugai.

Kwa taarifa yenu tu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Bunge linaendeshwa sasa kwa viwango vya hali ya juu *Presiding Officers* wote wawili walipelekwa Uingereza *House of Commons* ndio kama wiki nne zilizopita walikuwa London wamefanya mafunzo ya wiki mbili kwa hiyo ninapowaleta hapa sio kwamba na kubahatisha. Kwa hiyo, wote wawili wamepitia mafunzo hayo na matunda mtaendelea kuyaona hasa wakati wa bajeti *session*. (*Makofî*)

Sasa ninalo tatizo wachaangiaji katika hoja inayofuata, ni wawili tu. Kwa hiyo, nikisema kwamba nisubiri hadi saa sita, Mheshimiwa Job Ndugai, atashindwa kuja hata ku-*preside* kwa hiyo naomba mambo mawili kwanza nimruhusu sasa hivi baada ya maswali aweze kuja hapa ili aendeshe kikao na pili aendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wanayo nafasi nzuri tu kwa Muswada huu wa fedha kuweza kuomba nafasi ili waweze kuchangia. Baada ya kusema hivyo basi sasa namwomba Mheshimiwa Ndugai aje tubadilishane. (*Makofî*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Taasisi za Fedha wa Mwaka 2006 (The Banking and Financial Institutions Bill, 2006)

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Tunawaomba Waheshimiwa muondoke kwa utulivu na kwa haraka kidogo ili mambo mengine yaweze kuendelea, Mheshimiwa Waziri subiri kidogo.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 yaani *The Banking and Financial Institutions Act 2006* pamoja na marekebisho yake ambayo nina amini mmekwisha kabidhiwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti, wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mbunge wa Handeni kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa Dr. Mwinyi Haji Makame mwakilishi wa

jimbo la Dimani, pamoja na baadhi Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ambao kama nilivyoeleza wakati tunawasilisha Muswada wa Benki Kuu walishiriki pia katika kuujadili na kutoa ushauri kuhusu Muswada mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi ilipokutana mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo imesaidia sana kuuboresha Muswada huu. Vile vile nawashukuru sana wadau mbalimbali katika sekta ya Mabenki, ambao wametoa ushauri wao ambao kwa kiwango kikubwa tumezingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Sheria ya sasa ya Mabenki na Taasisi za Fedha sura Na. 432 ya mwaka 1991 ilitungwa takriban miaka kumi na tano iliyopita. Ni dhahiri tangu kutungwa kwa sheria hii yametokea mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kitaifa na duniani kote.

Mabadiliko hayo kwa upande wa kitaifa ni pamoja na ongezeko la Mabenki na Taasisi za Fedha ambapo idadi ya mabenki yameongezeka kutoka benki mbili mwaka 1990 hadi 32 hivi sasa.

Matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kibenki ikiwemo *Credit Cards* marekebisho manyopendekezoa kuwasilishwa katika Muswada huu yanalenga kuimirisha usimamizi wa mabenki na taasisi za fedha kutohana na mabadiliko haya yanayoendelea kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Muswada huu ninawaleta mbele yenu ya kutunga sheria mpya ya Mabenki na Taasisi za Fedha yamefanywa ili kwenda sambamba na mabadiliko mbalimbali ya sera za kiuchumi na kimataifa kwa lengo la kuwezesha wasimamizi wa mabenki na vyombo vya fedha.

Kabla sijaelezea kwa kirefu maudhui ya Muswada, naomba kutoa maeleo ya maeneo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu kama ifuatavyo.

(i) Kuwezesha usimamizi wa karibu wa Mabenki na Taasisi za Fedha na kuhakikisha zinajiendesha kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha usalama wa fedha za wananchi.

(ii) Kuweka mazingira bora ya usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa awamu ya pili ya mageuzi ya sekta ya fedha yaani *Second Generation of Financial Sector Reform*.

(iii) Kutoa idhini kwa Mabenki na Taasisi za Fedha kuanzisha kampuni tanzu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali za kibenki ili kuwafikia wananchi wa kawaida. Huduma hizo ni pamoja na mikopo ya kukodisha mitambo na vitendea kazi yaani *lease finance* mikopo ya muda mrefu, yaani *development finance* na mikopo ya nyumba yaani *mortgage finance*. Kifungu cha 24 (n) na (o) kwenye mabano cha Muswada kama kilivyorekebishwa.

(iv) Kuwezesha kuchukuliwa kwa hatua za tahadhari, yaani *prompt collective action* pale ambapo benki au taasisi ya fedha inashiria kulegalega ili kuokoa fedha za wananchi. Hatua hizi ni pamoja na kuziweka benki na taasisi za fedha chini ya wasimamizi wa Benki Kuu yaani *statutory Management*.

(v) Kulinda fedha za wateja wa Benki na taasisi za fedha kwa kuanzisha mfuko ujulikanao kama *Deposit Insurance Fund* kama kinga kwa wateja.

Aidha, mfuko huu utakuwa na bodi yenyewe wajumbe sita, watatu kati yao watakuwa Gavana wa Benki Kuu na Makatibu Wakuu wa Wizara za Fedha ya Serikali ya Mapinduzi na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe wengine watatu watatoka nje ya Benki Kuu na Serikali ambapo Sheria imeweka masharti kwamba mmoja wao atatoka baina ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maudhui ya Muswada, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kumi na moja. Sehemu ya kwanza yenyewe ibara ya 1 hadi 3 inahusu mambo ya utangulizi kama vile jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii na ufanuzi wa maneno yalijotumika katika Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inajuhumisha ibara ya 4 na 5 na zinaipa Benki ya Kuu ya Tanzania madaraka na uhuru zaidi katika utoaji wa leseni za shughuli za kibenki, na usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha. Sehemu hii pia inafafanua misingi ya usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, ya Muswada huu inahusu ibara 6 hadi 15 ambazo zinakusudia kuweka utaratibu wa utoaji na usimamizi wa leseni za shughuli za kibenki na mambo yanayoweza kusababisha kufutwa kwa leseni hizo. Masharti juu ya umilikaji wa Mabenki na Taasisi za Fedha yameahinishwa katika sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inajumuisha ibara 16 hadi 23 na zinaweka masharti juu ya mtaji unaohitaji kwa shughuli za kibenki. Muswada unapendekeza kuongeza kiwango cha chini cha mtaji kutoka shilingi bilioni moja ya sasa hadi shilingi bilioni tano.

Inapendekezwa vilevile kuipa Benki Kuu uwezo wa kuzigawa taasisi za fedha katika makundi na kuweka masharti ya upatikanaji wa huduma za kibenki katika maeneo yasiyopata huduma hiyo kwa urahisi, pamoja na kuweka taratibu thabiti za usimamizi wa vikundi vyta kuweka na kukopa visivyo vya ushirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu ibara 24 hadi 30 sehemu hii inaahisha shughuli ambazo Mabenki na Taasisi za Fedha yanaweza kuruhusiwa kufanya.

Pia inaweka masharti juu ya kiwango cha mkopo, ambacho mteja mmoja anaweza kupata kikomo cha mikopo kwa watu wenyewe uhusiano wa karibu na benki husika, uwekezaji wa taasisi za fedha na taratibu za kuungana na makampuni mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu sita yenye ibara 31 hadi 35 zinaipa Benki Kuu mamlaka ya kusimamia na kuzingatia ukaguzi wa taasisi za fedha pia inaipa uwezo Benki Kuu wa kupeana taarifa na mamlaka nyingine za usimamizi wa taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mweykeiti, sehemu ya saba ambayo inajumuisha ibara 36 hadi 42 zinahusu mfuko wa bima ya amana na vigezo vya uteuzi wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa mfuko wa bima ya amana. Mambo yanayohusu uwendeshaji wa mfuko wa Bima ya Amana yameainishwa katika sehemu hii ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane yenye ibara ya 43 hadi 49 zaweka masharti kuhusu mali inayotelekezwa, utoaji wa mikopo na ufuataliaji wa marejesho ya mikopo, utoaji wa taarifa zinazohusu wateja wa taasisi za fedha, uonyeshaji leseni za kibenki na taarifa za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa yenye ibara za 50 hadi 62 zinaainisha majukumu ya benki au taasisi ya fedha pale inapofilisika. Haki za wateja na wadai na mazingira yanayoweza kusababisha Benki Kuu kuiweka benki au taasisi yoyote ya fedha chini ya usimamizi wake yaani *Statutory Management*. Aidha, Muswada unafafanua mamlaka na majukumu ya Benki Kuu inapoiweka taasisi ya fedha chini ya usimamizi wake. Utaratibu wa ufilisi wa lazima na ulipaji wa mali mbalimbali wakati wa ufilisi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 10 yenye ibara 63 inaweka masharti ya ufunguaji wa ofisi zinazowakilisha taasisi za fedha zilizosajiliwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti sehemu ya 11 na ya mwisho yenye ibara ya 64 hadi 72 zinahusu masuala mengineyo kama mamlaka ya Benki ya Kuu ya kutoa adhabu kwa taasisi ya fedha, kinga ya kisheria dhidi ya mashtaka kwa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa Benki Kuu na wafanyakazi wake wanapotekeleza majukumu waliyopewa chini ya sheria hii na utungaji wa sheria ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada ulioko mbele yenu na hatimaye likubali kuupitisha kuwa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili tena nitoe maoni Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya

kuchambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha kwa mwaka 2006, *Banking and Financial Institutions Bill* 2006. Inayokusudia kufuta sheria ya sasa ya Mabenki na Taasisi za Fedha, sura Na. 342 ya mwaka 1991 kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya Benki Kuu hususani kusimamia mabenki haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee tena kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kwa kazi nzuri waliyoifanya na masaa mengi kuuchambua Muswada huu pamoja na uwakilishi mzito kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wamechangia mawazo mazuri wakati wa kuwasilisha mjadala wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wataalam wake wote kwa kutupa ushirikiano katika kuuchambua Muswada huu. Utaratibu huu ni mzuri kwa sababu moja ya mkakati unaoanza katika Kamati za Bunge letu Tukufu katika kuangalia jinsi ya kupunguza kero zetu hasa katika masuala yanayohusu pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada, naomba nitumie fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa na Mheshimiwa Kilontsi M. Mpologomyi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mzee N. Zubeir, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Ndugu Anselm Mrema Katibu na Pia Ndugu Helen Mbeba, Katibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 70(2) toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Muswada huu yanalenga kufuta Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991 na kutunga Sheria mpya. Aidha, Muswada unapendekeza kuoanisha vipengele vya Sheria na mahitaji ya wakati wa sasa ya Sekta ya Fedha nchini na taratibu bora za usimamizi wa Taasisi za Fedha zinazokubalika Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulifahamu hili wakati Bunge lako Tukufu lilipokuwa linatunga Sheria ya sasa ya mwaka 1991 Sekta ya Fedha ya Taifa ilikuwa na uwakilishi mdogo sana wa Taasisi mbili ama tatu *NBC, CRDB, TID* na *THB* ambazo pamoa na mtandao uliokuwa unafika maeneo mengi ya Tanzania, lakini ubora na ufanisi wa uendeshaji na utendaji ulikuwa umezifanya Taasisi hizi kuwa mahututi. Sheria hiyo iliweka mazingira ambayo historia sasa inaturuhusu kukubali kwamba ubinafsishaji wa Sekta ya Fedha umechangia katika kupanua utendaji na uwezo wa Mabenki na Taasisi nyingine za fedha hali ambayo imepelekea Bunge lako Tukufu kuanzia jana kuridhia marekebisho ya Sheria mpya ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 na sasa linajadili marekebisho ya Muswada huu wa Sheria ya Taasisi za Fedha na Mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa Sheria mpya ya Mabenki na Taasisi za Fedha umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, kuweka utaratibu maadhubuti wa usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha nchini ili kukidhi haja ya kuwa na mfumo wa fedha amba ni bora na salama. Pili, kuipa Benki Kuu ya Tanzania madaraka na uhuru zaidi katika utoaji wa leseni za shughuli za Kibenki na usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha. Tatu, kufafanua madhumuni ya msingi ya usimamizi wa Mabenki na Taasisi za Fedha.

Nne, kuweka utaratibu wa utoaji na usimamizi wa leseni za shughuli za kibenki na mambo yanayoweza kusababisha kufutwa kwa leseni hili; Tano, kuweka masharti mapya juu ya mtaji unaotakiwa kwa shughuli za kibenki ambapo inapendekezwa kuongeza kiwango cha chini cha mtaji kwa mabenki kutoka Shilingi bilioni moja hadi Shilingi bilioni tano; Kuipa Benki Kuu uwezo wa kuzigawa Taasisi za Fedha katika makundi na kuweka masharti mahsusii juu ya viwango vya mtaji kwa kila kundi ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za kibenki katika maeneo yasiyopata huduma hiyo kwa urahisi hususani Vijiji.

Kuainisha shughuli ambazo Benki Kuu inaweza kuyaruhusu Mabenki na Taasisi za Fedha kuweka masharti ya kiwango cha mkopo ambacho mteja mmoja anaweza kupata; Utoaji wa mikopo kwa watu wenye uhusianowa karibu na Benki husika; Uwekezaji wa Taasisi za Fedha na taratibu za kuungana na makampuni mengine; Kuipa uwezo Benki Kuu kwa kupeana taarifa na mamlaka nyingine za usimamizi wa Taasisi za Fedha katika nchi nyingine hususan nchi jirani; Kuweka vigezo kwa ajili ya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Bima ya Amana.

Kuweka wazi majukumu ya Benki au Taasisi ya Fedha pale inapofilisika; Haki za wateja na wadai na mazingira yanayowawezesha kusababisha Benki Kuu kuiweka Taasisi yoyote ya Fedha chini ya usimamizi wake.

Mwisho, kufafanua mamlaka na majukumu ya Benki Kuu inapoiweka Taasisi ya Fedha chini ya usimamizi wake, utaratibu wa ufilisi wa lazima (*Compulsory Liquidation*) na ulipaji wa madai mbalimbali wakati wa ufilisi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Kamati kilichohudhuriwa na Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Zakhia Meghji, Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Katibu Mkuu Hazina na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kilichofanyika tarehe 23 - 25 Machi, 2006 Kamati ilipitia vifungu vya Muswada huu.

Baada ya majadiliano, Kamati ilipendekeza marekebisho pamoja na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha Muswada huu ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri ameyakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na Muswada ule wa Benki Kuu, Kamati yangu imetambua umuhimu wa Muswada huu hasa tukizingatia kuwa unahusu Benki na Taasisi za Fedha ambazo zina mahusiano ya moja kwa moja na makundi mbalimbali ya jamii katika uchumi wetu. Maana yake ni kuwa Benki na Taasisi hizi ndizo zinazopasa kuwahudumia Watanzania wenyewe kipato cha juu, cha kati na kile cha chini hasa wanaoishi Vijijini.

Eneo kubwa linalijitokeza hivi sasa, kama tatizo kubwa ni mazingira ya kibenki ambayo bado hayajatoa fursa kamilifu ya matumizi ya huduma zake kwa wananchi walio wengi hasa kule Vijijini. Jitihada za Serikali za kuanzisha Sera ya mikopo midogo kwa biashara ndogo na za kati na ile ya MKURABITA pamoja na mpango mzima wa MKUKUTA haina budi kusaidiana na utendaji kazi na uendeshaji wa shughuli hizi za Benki na Taasisi za Fedha. Hapo ndiyo umuhimu wa Muswada huu unapodhihirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni lile la riba kubwa ambazo bado zinatozwa na Mabenki yetu na Taasisi zetu za Fedha kwenye mikopo. Uwezeshaji wa Sekta ya Fedha katika kusaidia kuendesha uchumi wetu unakwazwa na ukubwa wa viwango vya riba za mikopo ikilinganishwa na riba za amana zinazowekwa. Eneo hili ni muhimu likaangaliwa hasa na Benki Kuu baada ya kupewa uwezo zaidi wa usimamizi na Sheria mpya ili kuhakikisha kuwa idadi ya wanaofaidi huduma za kibenki inakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia kwa kipindi kirefu kuwa Mabenki na Taasisi zetu kuwa zina fedha nyingi zaidi ambazo zinabakia katika vyombo hivyo *Excess Liquidity* bila ya kutoa huduma zinazolengwa. Hili ni tatizo ambalo nalo limegusiwa katika Muswada huu. Kamati yangu imeshauri kuwa Benki Kuu sasa ijaribu kurekebisha kasoro hizi katika mazingira ya Sekta ya Kifedha ili mchango wa Benki na Taasisi za Fedha katika kukuza uchumi wa nchi uwe mkubwa zaidi kuliko hivi sasa.

Benki Kuu imeelekezwa itoe mwongozo wa kisera ambazo utahamasisha Benki na Taasisi za Fedha zilizo chini ya usimamizi wake kuona umuhimu wa kipekee wa kufikisha huduma za Taasisi hizo kwa Watanzania wote badala ya kuweka mkazo kwa wakazi na shughuli za Biashara na Uchumi za Mijini tu. Maendeleo ya Tanzania yanategemea mchango wa kila Mtanzania na hivyo Sekta ya Fedha inashauriwa sasa

iangalie kwa makini zaidi namna ya kuwaingiza Watanzania wengine na shughuli zao za kiuchumi katika mtandao wa huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba hata kama idadi ya Mabenki nchini inaendelea kuongezeka, haiwezi kuwa na *impact* kubwa katika uchumi kama huduma zake zitakuwa ni *selective* na *stratified* kwa maana ya kuhudumia sehemu ndogo ya wateja na kuacha sehemu kubwa ya wahitaji hususani wakulima wetu kule Vijiji. Ni matumaini ya Kamati yangu kwamba Benki Kuu itaendelea kuhakikisha kuwa huduma za Benki na Taasisi za fedha hususan hizi zinazowagusa Watanzania moja kwa moja, zinapanua shughuli zake na kuwafikia walio wengi, pamoja na uvezeshaji wa zile Taasisi ndogo za fedha ambazo zinaendelea kutoa mikopo midogo kwa Watanzania wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa katika maelezo ya Muswada wa Sheria ya Benki Kuu, ni matumaini ya Kamati yangu kuwa Muswada huu wa Benki na Taasisi za Fedha utaongezea nguvu ya dhana ya uvezeshaji ambayo hivi sasa ni kipaumbele cha kwanza katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imebaini kwamba mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika uwekezaji kutoka nje na ndani ya nchi na pia ongezeko la mapato katika biashara za nje, utalii na kadhalika yametokana kwa kiasi kikubwa na imani ya wawekezaji kwamba Sekta ya Fedha ya Tanzania ina uwezo wa kiutendaji na kiteknolojia ya kushiriki katika mfumo wa kibenki wa Kimataifa, *International Banking System*. Hali hii inatoa motisha kubwa kwa wafanyabiashara na watu wengine ambao wanahitaji kufanya malipo kuweka na kuhamisha fedha mionganoni mwa Mabenki ya sehemu mbalimbali kwa usalama bila usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhia kuwa sehemu hii ya Sheria ya mwaka 1991 inahitaji kuboreshwa ili ikidhi mahitaji ya mazingira ya kiuchumi ya Tanzania na dunia inayotuzunguka kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati yangu kukubali kimsingi mapendekezo ya Muswada huu, natoa ushauri ufuatao:-

(a) Mapendekezo ya kuongeza masuala ya *Development Banking* na *Mortgage Banking* katika Muswada hususan katika kifungu 24(1)(n) na (o) yazingatiwe. Kamati inaamini kuziongezea shughuli za uwekezaji mitaji katika maeneo haya Benki na Taasisi zetu za Fedha zitaboresha zaidi uchumi wa nchi yetu.

(b) Uwakilishi wa Serikali zote mbili, yaani ile ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar uzingatiwe.

(c) Kamati inashauri Serikali kuweka adhabu kali kwa mtu au Shirika au chombo kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 48 cha Sheria kinachohusu uaminifu na usiri hasa katika kuhifadhi taarifa za habari za wateja wanaotumia huduma za kibenki. Utoaji wa siri wa viwango vya fedha vya mteja ni kosa kubwa sana.

Kamati yangu inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kifungu cha 16 na 17 (1) - (3) vinavyohusu masharti ya mitaji, akiba na mahesabu ya kihasibu katika uanzishwaji wa Benki au Taasisi ya Fedha unatayarishiwa kanuni ambazo zitawezesha kila kundi au jamii inayohitaji Benki au Taasisi ya Fedha inapata fursa hiyo kutokana na hali halisi ya mazingira na uchumi wa eneo hilo. Hii itasaidia sana katika kupanua huduma za kibenki na za kifedha katika nchi yetu bila kujali maeneo na vile vile kuepukana na tatizo la kupatikana kwa huduma za vyombo hivi katika maeneo fulani tu na mengine kuachwa.

Benki za jamii (*Community Banks*), Benki za Kuweka na Kukopa zipate fursa ya kuanzishwa bila ya kuathiriwa na masharti makubwa yaliyowekwa katika vifungu viliviyotajwa ambavyo ni maalum kwa ajili ya Taasisi zinazohitaji mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakhia Hamdan Meghji, Naibu wake Mheshimiwa Abdisalaam Khatib, Gavana wa Benki Kuu, Ndugu Daud Balali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na Maafisa wote wa Benki Kuu. Aidha, shukrani za pekee zinatolewa kwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Mwinyihija Makame, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Maafisa wao na Wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kuisaidia Kamati kufanikisha kujadili ili hatimaye tupitishe Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. HAMAD R. MOHAMED - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANIA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naomba nichukue fursa hii kuwasilisha maombi ya Kambi rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada huu wa *The Bank and Financial Institution Bill, 2006* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 (5)(b) na (c) na pia kifungu cha 81 (1)toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu, Gavana na pia Ndugu zetu kutoka Zanzibar, Waziri pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Uchumi na Fedha ambao kwa bahati mbaya waliwakilishwa kutoka upande mmoja tu wa Chama Tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba Kambi ya Upinzani kwanza inaunga mkono Muswada huu mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kama unavyosomeka katika *long title* yake ni kuwa na madhumuni ya kutoa miongozo na udhibiti kuhusu shughuli zote za Benki na Taasisi za Fedha pamoja na Vyama vya Kuweka na Kukopa, yaani *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoileweka, ni ukweli usiopingika kuwa Benki na Asasi za Fedha kazi yake kuu ni kuinua uchumi wa nchi kwa kuwawezesha wananchi kuwatunzia fedha zao na kuwakopesha ili kukamilisha mzungumko wa fedha katika kuuza na kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu na ule wa Benki Kuu uliopitishwa na Bunge lako Tukufu punde hivi, unatoa fursa kwa Benki Kuu kuratibu na kusimamia vyema mabenki na vyombo nya fedha nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vyombo vyote nya fedha vinajitahidi katika mipango yake kuhakikisha kuwa vina uwezo wa kujiendesha na hatimaye viweze kutoa huduma. Hivyo, ni ukweli usiofichika kwamba vyombo hivyo vitajitahidi kukusanya mapato kwa njia ya riba, *Bank Charges*, kununua hisa na *bonds* ili hatimaye viwe na uwezo wa kutoa mikopo ya muda mfupi na hatimaye muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii haitofautiani na ile ya mfugaji, ni lazima ampe ng'ombe malisho na maji ya kutosha ili apate maziwa. Njia rahisi ya kuvifanya vyombo nya fedha vikopeshe bila wasiwasi ni kwa raia kuwa na tabia ya kuweka akiba hata kama ndogo kiasi gani, *Banker* akiona mteja ana tabia ya kuweka kila wakati, anapopata mapato hujenga imani kuwa mteja huyo anaweza kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi sana, maana sote tunafikiria kuanzisha Benki kwa ajili ya kukopa tu, tena kwa riba ndogo. Mawazo haya yataua hata hizo Benki zetu za Jumuiya tunazozianzisha ambazo ni *Microfinance Institutions*. Ni vyema kwanza tujenge tabia ya kuelimishaja umuhimi wa kuweka, umuhimu wa kukopa kwa ajili ya kuzalisha ili uwe na uwezo wa kulipa unachokikopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa *Microfinance* zinaendela kutoa huduma, nchi kama Bangladesh wameweza kukusanya rasimali kwa kuanzisha namna mbalimbali za akiba na mikopo, yaani *Various Servings and Credit Products* kwa mfano kuweka akiba kila siku, yaani *Daily Service*, kuweka kwa lazima, kuweka kwa hiari, kuweka kwa mikataba na kuweka kwa muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali, Benki Kuu na Taasisi zote za fedha zizidishe elimu ya kuelimisha watu kuweka fedha na kukopa kwa madhumuni maalum yatakayomwezesha mkopaji kurudisha mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii inahitajika sana Vijijini kwani ndiko hasa kwenye mahitaji makubwa ya mikopo midogo midogo na hatimaye mikopo ya kati, yaani *Small na Medium Microfinance Credits*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu uliopatikana katika nchi zinazoendelea ambazo zimeijengea uzoefu mkubwa *Microfinance* kukopa kwenye zaidi ya Taasisi moja, yaani *overlapping*, hii inatokana na mkopaji kutokutimiziwa mahitaji kutokana na mtaji mdogo wa Taasisi aliyokopa na mahitaji yake ni makubwa au pengine wakopaji ni wengi kuliko uwezo wa chombo kinachohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanywa juu ya matokeo baada ya maskini kupatiwa mikopo na mabadiliko ya maisha yao, imeonekana kuwa mikopo midogo husaidia zaidi katika kutoa huduma, yaani *services* kuliko kwa kichocheo cha kupunguza umaskini. Kwa mfano, utafiti uliofanywa Bangladesh katika *Household* 1798 ni asilimia moja tu (1) ya watu wote ndiyo walioondokana na umaskini kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri kuwa Benki Kuu na Taasisi nyingine zisaidie *NGO* na *Microfinance Institutions* kuunda aina za mikopo, yaani *Products or portfolios* zitakazowawezesha wakopaji kujikwamua katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa ujumla wake imeundwa na jamii maskini. Kwa hiyo basi, dhana nzima ya *Microfinance* inatakiwa ifanye kazi yake kwa makini na nguvu zote za Serikali zielekezwe katika Sekta hii ili kumkomboa Mtanzania na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Microfinance* kwa lugha ya kawaida ni kwa chombo kinachohusika na shughuli zote za kibenki lakini kwa makundi ya wale wenye kipato cha chini, yaani *Low Income Clients* wakati *Micro Credit* ni utoaji wa mikopo midogo ambayo inaweza kutolewa na Benki na Asasi zote za Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio kikubwa cha Watanzania ni kuitaka Serikali kupitia Benki Kuu kutoa upendeleo maalum wa kisera kwa nia ya kuziinua jamii zote ambazo kwa njia moja au nyingine zinaishi katika mazingira magumu na kuona kama Serikali yao hajiali, yaani *to make policy which offer subside oriented programmes to serve marginal Communities and poor household and control interest rates*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaamini kuwa pindi Serikali na Benki Kuu wakiishapitisha sera hizo za upendeleo maalum itaviwezesha vikundi vya jamii, yaani *self help groups* katika maeneo mbalimbali ya Tanzania kuanza kufanya shughuli zake za kuinua uchumi na kujiongezea kipato katika ngazi ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu kama chombo mama katika Asasi zote zinazotoa huduma za kifedha, inayo dhamana ya kuhakikisha kuwa *Microfinance Institutions* nazo zinakuwa na uwezo wa kupata mikopo yenye masharti yanayoendana na hali halisi sehemu ambazo Asasi hizo zinafanyiwa kazi. Hivyo basi, ni jukumu la Benki Kuu kutoa mwelekeo wa riba ambazo Mabenki makubwa ya Biashara yanatakiwa kuzipa Asasi hizo, vilevile kutoa mwongozi juu ya utendaji kazi wa wamiliki wa Benki hizo za *Microfinance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tafiti mbalimbali nilizofanya, inawezekana kabisa ni rahisi kutoa mikopo Kilimanjaro kwa sababu ya uelewa wa watu na kadhalika, lakini ikawa ni taabu sana kutoa mikopo Kibondo ambapo uelewa wa watu ni mdogo. Kwa hiyo, Benki Kuu inatakiwa ifanye utafiti wa kutosha kuangalia hali halisi za watu zilivyo ili kuzisaidia zile *institutions* zinazotoa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *BoT* inaratibu na kusimamia vyombo vinavyohusika na utoaji huduma ya fedha, itakuwa ni muhimu kwanza ifanye utafiti nchi nzima kuangalia mahitaji ya vikundi na watu binafsi wanaohitaji huduma ya mikopo midogo midogo na waangalie hali halisi ya uwezo, yaani *purchasing power* katika maeneo husika. Wakishakuwa na uelewa wa mitaji nchi nzima, itakuwa ni rahisi kwao kuratibu ratiba, riba na mikopo itakayotolewa na *Microfinance Institutions* na Mabenki makubwa, yaani wanaita *Area Subside Oriented Credit Programmes*, itaweza kufanikiwa kwa sasa. Naamini kabisa kuwa Serikali haina takwimu ya mahitaji kujua ni asilimia ngapi ya wananchi wanahitaji huduma ya mikopo midogo midogo, ya kati na mikubwa na ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inashindwa kuona kama kweli Serikali ina dhamira ya kweli ya kuwainua wananchi wake kwa kipato kwa kupitia Mabenki na Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *Balance Sheet* ya *NMB*, inaonyesha kuwa Benki hiyo imeikopesha Serikali kwa kununua *Treasury Bills* kwa asilimia 84 ya mgao waliouweka kwa ajili ya kukopesha na kwa kutoa mikopo na kwa sababu kubwa wanayoitumia kwamba hii ni *risk free* na asilimia 16 iliyobaki ndiyo wamekopeshwa wateja wao pamoja na kwamba wateja hao huweka dhamana ambayo mkopaji hawezi kuitumia mahali pengine ili kuipunguzia Benki *risk*, lakini bado Benki zinatoza riba kubwa kwa wateja wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *trend* ya Serikali kwa Mabenki yetu ndiyo kama hiyo, maana yake ni kuwa fedha zote za Mabenki zimelundikana humo kwa kungoja kuikopesha Serikali. Je, Benki zitakuwa na haja ya kuwakopesha wateja wake wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa lipo tatizo la mfumo wa mgawanyo wa mtaji katika kuelekeza kwenye uwekezaji, yaani *allocation of capital for investment*. Tunaiomba Benki Kuu baada ya kupita kwa Miswada hii miwili na kuwa Sheria iangalie mfumo mzima wa kutumia fedha nyingi walizonazo Benki zetu na namna fedha hizo zitakavyoweza kuingizwa katika mzunguko wa kuwakopesha wateja kwa asilimia isiyopungua 50 badala ya asilimia 16 ya sasa na kuzikopesha *NGO* na hizo *Small and Medium Microfinance Enterprises* ili nazo ziweze kutoa mikopo inayoweza kubadilisha hali ya maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wateja kuweka dhamana na kuwazuia wateja kuzitumia dhamana hizo kwa shughuli nyingine, riba ya mikopo bado siyo chini ya asilimia 16 na riba ya kuweka inayotolewa na Benki haizidi asilimia 2.5, 3 mpaka 3.5. Kwa hiyo, ukitoa asilimia 16 na asilimia 2.5, wao wanapata faida ya asilimia 13.5. Hii ni mbali na *Bank Charges* wanazotoza. Hivyo *Banks* kutoakutoa mikopo kwa kisingizio cha *high risks* hakipo, kwa nini faida wanayoitengeneza kwa kuikopesha Serikali na riba kubwa wanazozitoza kwa wakopaji wengine ni dhahiri kuwa Mabenki yatakuwa na fedha nyingi ambazo wangeliweza kuwakopesha wateja wao kwa asilimia isiyopungua 50.

Microfinance, SACCOS na SCALT hata Vyama vya Ushirika vya Mazao na Wafugaji, tunaishauri Serikali kuangalia upya utaratibu huu wa Mabenki kuikopesha Serikali kwa asilimia kubwa na kushindwa kutoa mikopo kwa wananchi, eti kuikopesha Serikali ni *risk free* wakati wananchi wanakopeshwa baada ya Benki kuridhika na dhamana za wakopaji kitu kinachoondoa *risks* katika fedha wanazokopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii kubwa ya Watanzania ni ile inayoishi Vijijini na jamii hiyo ndiyo inayochangia sehemu kubwa ya pato la Taifa. Kama Sheria ya Vyama vya Ushirika inavyosema kuwa Msajili wa Vyama vya Ushirika kupitia Idara ya Ushirika, Mikoa na Wilaya ndiyo mwenye mamlaka ya kuweka taratibu za usimamizi wa shughuli zote zinazofanya na Vyama hivyo kama vya kuweka na kukopa kama *SACCOS* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na hali halisi ya utendaji wa kazi na mazingira ya Vyama hivyo vinavyofanya kazi na ukweli kuwa vinahudumia sehemu kubwa ya Watanzania, tunashauri Benki Kuu iwe kiungo baina ya Msajili wa Vyama vya Ushirika na Mabenki ili kuweka mfumo utakaolazimisha Mabenki hayo kusaidia Vyama vya Kuweka na Kukopa na Vyama vingine vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Benki Kuu itilie maanani ni jinsi gani itasaidia *informal financial institutions* kuwa *formal* ambazo ndizo hasa zinazolengwa katika Muswada huu ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Benki ya Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha pili cha Muswada kinazungumzia Mamlaka ya Benki Kuu ya kutoa leseni na kifungu cha nane na cha kumi kinazungumzia Taasisi ya Fedha kupewa au kutokupewa leseni. Kutokana na uzoefu tuliuopata huko nyuma, ni vyema tukawa na muda maalum ambaa mwombaji anaweza kupatiwa leseni au kukataliwa. Hivyo, Kambi rasmi ya Upinzani inashauri kuwa ama ndani ya Sheria hii au katika Kanuni, utamkwe muda wa tokea ombi linapopokelewa na kujibiwa ili kuondoa usumbufu wa kungojea hadi kukata tamaa. Pia Waziri atakapojobu hoja za Wabunge, ni vyema akatueleza *standard practice* inachukua muda gani hadi chombo husika kupata leseni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 11 (4) cha Muswada, kinatoa mamlaka kwa Benki Kuu kusimamisha au kufuta leseni kwa Tawi la Benki lililopewa leseni au Kampuni tanzu kama chombo chenyewe chenye mamlaka cha nchi iliyoko. Asasi hiyo imesimamisha au kufuta leseni ya asasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inaomba ufanuzi wa mambo yafuatayo:-

Kwanza: Je, kama Asasi hiyo inafanya vizuri sana Tanzania na ikiwa wenyе hisa hapa Tanzania ni tofauti na wale wa nje: Je nayo itafutwa?

Pili, inapotokea Asasi hiyo huko kwao imeuza hisa zote kwa Kampuni nyingine, lakini uuzaaji huo haukuathiri umiliki wa *Tanzania Branch*, nayo pia itafutwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatoa ushauri kuwa kama kweli nchi yetu imedhamiria kwa dhati kuwainua wananchi wake, wakulima, wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati, ni lazima iondoe sera zinazomnyima mkulima na mfugaji wa kawaida haki ya mali zake kutokutambulika kama dhamana katika Asasi za Fedha hizo rasmi.

Aidha, Serikali iimarishe Asasi zisizo rasmi zinazotoa mikopo kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati na wakati huo huo na ufuatilaji kuhusu utendaji wa Asasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Muswada huu wa Taasisi za fedha na Mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanafalsafa mmoja aliwahi kusema kwamba “*the highest good in life is happiness*” na mimi nasema kwa sababu hiyo ndiyo maana Ilani ya Chama cha Mapinduzi imekusudia kwa dhati kabisa kuondoa umaskini wa watu wake na hasa wale wanaoishi katika mazingira ya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kuwa sikuanza kumshukuru Waziri kwa kuleta Muswada huu mzuri katika kipindi hiki muafaka, Muswada ambao kwa kweli umekuja kwa wakati ambao wananchi wanasubiri nini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya katika kipindi hiki cha miaka mitano, basi naomba nifanye hivyo kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu mzuri katika kipindi hiki muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu moja kwa moja kwa kupongeza Muswada huu hasa katika namna ambavyo umeeleza hizi *Microfinance Company na Housing Finance Company* katika ile sehemu ya tatu ya Muswada section Na.14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *section* hii kwa hakika ndiyo hasa imejikita pale kwenye shida kubwa ya Watanzania. Mimi nilipokuwa nje ya Bunge nikiwa mwananchi wa kawaida sikuamini kwamba ni rahisi sana kupata mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba, hali hii ndiyo inayowakuta wananchi wetu wengi. Nilipoingia humu juzi naambiwa Mabenki yana fedha, lakini zile fedha hazina wakopaji. Mimi nilishangaal! Hali ilivyo kwa wananchi wetu wa kawaida kupata mkopo ni kitu kigumu kweli kweli. Binafsi nimewahi kukumbwa na tatizo hilo, kutafuta mkopo wa Shilingi milioni mbili. Ilinichukua karibu miezi nane na nina nyumba yenye thamani ya Shilingi milioni 20 tena siyo moja. Lakini vyote hivi havikutosha kunifanya mimi kuweza ku-*secure* mkopo kutoka Benki.

Lakini humu pengine ni taarifa na maneno ya wazi kabisa kwamba Mabenki yana fedha, lakini zinakosa wakopaji. Hii mimi nasema kweli kwa kipindi kirefu tumewanyanyasa watu wetu kwa sababu kama kweli Sheria hii tutaitunga na ikatumika kwa mantiki na kwa maelezo yake kama ilivyo, nina hakika hakuna Mtanzania hata mmoja atakayekuwa maskini katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wako tayari, utayari kwao umefika, wana nia ya kujikomboa na umaskini, lakini wanashindwa mahali pa kupata mitaji. Lakini sasa kwa sababu Sheria hii inaeleza kwa uwazi dhamira yake ya kuwasaidia wananchi hawa na hasa wanaoishi Vijijini, basi dhamira hii kwa kadri ya tafsiri ya sheria yenye we iweze kuwa kama ambavyo imedhamiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sayansi ya Sheria, kila sheria inapotungwa huwa ina *spirit* yake na *spirit* ya Sheria yoyote inatokana na mazingira ya wakati huo. Sababu ya Sheria kutungwa, lazima iwe wazi sana, basi sababu ya Sheria hii ya Mabenki isiwe tu peke yake kwamba imetungwa ili tuweze kudhibiti haya Mabenki katika *operations* zake kwa sababu tumeshapata shida mbalimbali, tumeshaiona ile *Greenland Bank* ilivyoanguka na vipi na vipi isiwe tu inaishia hapo, lakini iende zaidi ya hapo na kuzifikiria zile *functions* kwa maslahi ya maendeleo ya wananchi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Hapo ndipo tunapoweza tukawa tumetunga Sheria ambayo kwa dhati kabisa inaweza kumsaidia mwananchi wa Tanzania na kwa sababu wameona Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inayowasaidia, basi tunaweza tukawa tumetoa majibu kwa matatizo yao ya muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii, unaweza ukamkuta mtu hana kazi, lakini mtu huyu ambaye hana kazi anajenga nyumba ya ghorofa, yenyе ghorofa 12 Karikoo. Hii ni ajabu! Hakuna nchi yoyote duniani watu wanajenga nyumba kwa fedha yao kutoka mfukoni. Sheria hii nadhani inajibu kwamba wakati wa kubabaisha na wakati sasa wa kufanya vitu kwa kubabaisha kwa vyanzo vya mapato ambavyo havifahamiki umepita. Kwa sababu huyu mtu anayejenga ghorofa ya milioni 600, milioni 800 hadi bilioni moja unaweza ukamkuta hana hata *registered business*, hata kwenye orodha ya walipa kodi huyu mtu hayupo. Hii ni ajabu sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nasema, kwa Sheria hii sasa kwamba tutakuwa na utaratibu wa *Housing Finance Company's* ambazo nina hakika zitatoa mikopo kwa nia ya kuwafanya watu wakajenga nyumba zao za kuishi, lakini pia hata biashara itakuwa ni msaada mkubwa.

Nadhani kutokuwepo kwa uaminifu mkubwa katika Watendaji wa Sekta rasmi na zisizo rasmi na Watendaji wakubwa au Watumishi wa Serikali kutokuwa waaminifu ni kutokana na wao kupenda kuwa na mahali ambapo wanaweza wakaishi kwa raha. Hakuna mtu hapendi kuwa na nyumba yake ya kuishi. Mimi ninaamini kama tungeundiana Tume humu tukachunguzana kila mtu amejenga nyumba kwa utaratibu gani, basi hapa tungeweza kuona maajabu. Unaweza kumkuta karani ana nyumba ya Shilingi milioni 100. Sasa tukianza kuhojiana hapa, kila mmoja aseme ye ye ameipataje. Tutakuta kuna vichekesho huko ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nasema, umefika wakati sasa *we must be open*. Tuwe wazi, watu wafanye vitu kwa uwazi, watu wamiliki mali kwa uwazi na kwa utaratibu unaoeleweka ambao nina hakika utawekwa vizuri kwa kutumia Sheria hii ya Mabenki na Taasisi za Fedha. Kwa sababu hapa ninaona kuna *Housing Company's* ambayo nafikiri itatoa mikopo kwa ajili ya watu kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba ninafurahishwa pia katika *section* hiyo hiyo ya 14 namna ya tafsiri ya *Microfinance Company* ambapo imejaribu kuchukua karibu watu wa aina zote, lakini zaidi sana inapozungumzia yule mkulima ndogo kabisa wa Vijijini. Mimi nasema, kwa sababu hii *phenomena* ya *Microfinance* hasa ni kwa ajili ya mtu mdogo, basi kwa kutumia Sheria hii na pengine kungekuwa na *expressed provision*, Sheria hii iseme kwa uwazi kabisa namna ambavyo itamsaidia yule mtu wa Kijijini kabisa. Watu wetu wa Vijijini, tunajua, nchi yetu ni maskini, lakini ule umaskini tunaozungumza humu haileti ile *image* halisi ya umaskini halisi ambao wananchi wetu kule Vijijini wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini wa wananchi wetu kule Vijijini ni mkubwa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulijua hili amelisema sana kwamba umaskini wa watu wetu ni mkubwa sana tofauti na hali ambayo pengine tunaiona kwa juu juu. Wako watu hawana vitanda vya kulalia. Siyo nyumba, kitanda cha kulalia hana! Wako watu wetu hawana viatu, wako watu wetu hawana hata choo. Huu ni umaskini mkubwa tunawatoaje huko? Imani yangu kubwa ni kwamba tutawatoa huko kama tutafanya kilimo kikawa ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hii. Kilimo hiki hakiwezi kikakua, hakiwezi kikawa ndiyo kipaumbele kama hakutakuwa na makusudi ya kuwasaidia wakulima wale wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vitu vingi vinaweza kufanyika ili kuwasaidia hawa wananchi. Tunazo zile Benki zetu za Ushirika ambazo tumesema sisi, Ushirika wetu katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi utakuwa wa Kuweka na Kukopa. Zile *SACCOS* ni Benki za Kata. Hizi zisiachwe na pengine Benki hizi zitakazokuja, *Microfinance* na nini zijaribu *ku-inject* hiyo power yake kwenye hizo Benki ili kutokuharibu na *ku-twist mind* ya wananchi wetu wa Kijijini. Kwa sababu Vijijini watu wakishafahamu kitu fulani, basi ukiwaleta kitu kipyra wana-*twist mind* na hivyo tunaweza tukakuta *tuna-end with nothing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa kweli mkazo mkubwa ungekuwa ni kuzisaidia zile Benki Kata kwa sababu nia yao ni kukopa Sh.200,000/=, Sh.150,000/=, Sh.300,000/= mikopo midogo midogo ambayo ikienda kule kwenye Benki Kata, ninaamini uwezekano wa wengi kupata na kupungua kwa urasimu kutakuwepo. Kwa sababu Benki wanaiona iko pale, inaendeshwa na ndugu zao, jamaa zao wanaowafahamu kuliko ukisema mtu atoke kule Kibakwe aje achukue mkopo *NMB Mpwapwa*, huu ni mgogoro mkubwa sana.

Kwanza, ile nauli yenye we atakayo itumia mpaka afike na aweze kupata mkopo itamchukua muda mrefu. Lakini pia urasimu na mambo mengine yanaweza yakasababisha akate tamaa na hivyo kubaki hivyo hivyo maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niende zaidi ya hapo na niipongeze hii Sheria kwamba katika *section 49* wamejaribu kueleza namna ambavyo watadhibiti haya Mabenki na kwa kweli hii Sheria inakusudia kwa dhati kabisa kudhibiti haya Mabenki na mimi niseme kabisa, hii ni njia nzuri ya kuweza kuyadhibiti. Maana wamesema kwamba zile Benki ambazo zitakuja kutoka nje, basi zitajaribu kuangaliwa kutoka huko zilikotoka na zimeweza kuendeshwa kule kwa ufanisi wa kiasi gani kabla hatujaweza kuzisajili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kwa kumalizia mazungumzo kwamba nia ya Muswada huu wa Sheria iwe kweli kabisa kwenda kumwokoa mwananchi wa Kijiji. *Financial Institutions* hizi zipo, tuna Mabenki mengi sana yamejazana Dar es Salaam ambayo yanazungusha tu kukopesha hapo hapo tu na hakuna kinachoendelea. Lakini Vijijini kwetu watu wana shida na wanabiri waone sasa Serikali hii inawafanya nini. Kwa kutumia sheria hii, mimi naamini tutakuwa na namna nzuri ya kuweza kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nikupongeze pia kwa kukalia Kiti hicho kwa mara ya kwanza na ulivyokaa tu ni dalili kwamba unakiweza sawa sawa kama mwenzako aliyekutangulia jana Mheshimiwa Jenista Mhagama alivyokimudu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza na Muswada huu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, timu yake, Gavana wa Benki na timu yake. Ni kweli huu ni Muswada wa muhimu na ni Muswada ambao unaweza ukatusaidia kututoa katika umaskini kama utakuwa umewekwa kwa umakini inavyotakiwa. Mimi nataka kulenga hapo kwenye sura hiyo ya kututoa kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema tu kwamba kwa bahati mbaya kama alivyosema mwenzangu na mimi nianze hapo hapo kwamba *spirit* ya Muswada huu haina tofauti na *spirit* ya Muswada Na. 342 tunaoufuta, tena umekwenda kwenye *spirit* kali zaidi kwa maana ya udhibiti. Lakini sio kwa maana ya kusukuma na kusaidia Taasisi zetu ambazo tungependa ziende zaidi Vijijini. Sasa mimi nilitegemea kwamba baada ya kazi nzuri iliyofanywa na mtaalam De Soto ambayo kazi hiyo nadhani imeendelea vizuri pia kwa Kamati ya dada yangu Mheshimiwa Anna Makinda, nilitegemea kuona kwamba *spirit* ya sheria hii inakwenda zaidi katika *facilitation* kuliko udhibiti. Lakini dhana ninayoiona zaidi ni ya udhibiti kuliko kusukuma, kusaidia, kuhamasisha na kushawishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kazi ya Benki Kuu daima ni udhibiti. Lakini ninarudi pia kwenye historia na kwa bahati nzuri nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge hili, miaka zaidi ya 10 iliyopita tulipata nafasi ya kutembelea nchi kadhaa ikiwemo Ujerumani, Sweden na Denmark. Wenzetu walikotoka miaka zaidi ya 100 iliyopita Benki Kuu zao kazi zilizofanywa ni *facilitation* kuliko udhibiti. Sasa sisi tunadharau lengo na nia ya *facilitation* tunakimbilia zaidi waliko wenzetu leo ambayo ni *control* ambapo wao wanahitaji *control* kwa sababu hawahitaji kwenda kwa wananchi, wananchi wanaelewa Taasisi za fedha zimeenea kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa wenzetu, dhana ya Shipakase Ujerumani, *Saving Bank* tunayo sisi kwenye Posta, lakini Posta ziko wapi? Ziko Makao Makuu ya Wilaya zaidi. Tena kama ni zote, huwezi kupata *saving* na huwezi kuwa na Benki kama huna *saving*. Mmoja alisema hata kama ni senti kumi lakini *ana-save*. Tena huko nyuma tulianza vizuri, tuliweka masanduku yale madogo, unaweka kufuli, unafundisha mtu huko nyumbani afanye *saving*, ile hela hawezi kuitoa. Ule usfunguo unawekwa mahali! Hapa tuliwashawishi watu! *Spirit* tuliyonayo haitupeleki kule na huyu ni mtu pekee tu anayeweza kutufikisha katika dhana hiyo kwa sababu Benki Kuu inapaswa kuleta uwiano kati ya udhibiti ili fedha kidogo ya wananchi iweze kulindwa, lakini pia iweze kuhamasisha Taasisi za wananchi ziweze kujiwezesha vizuri. Hii *balance* isipokuwepo hatuwezi kupiga vita umaskini hata siku moja. Tutaendelea kuimba kupiga vita umaskini lakini tutabaki kuwa na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio jambo la ajabu, wananchi walio wengi leo wanaona Benki ni Taasisi ya miujiza, ni kitu cha ajabu. Wananchi walio wengi hawawezi kuingia kwenye Benki, tena wanapita mita 50 kutoka Benki. Tena siku hizi ni mbaya zaidi, kwa sababu na Askari yupo pale ana bunduki, wananchi wanaikimbia Benki. Wakati wenzetu wanahamasisha hata Polisi wa wenzetu wanakuwa ni *friendly*, lakini wananchi wetu wakiona ile bunduki wanakimbia. Ni kwa sababu dhana hii hajaingia kwa wananchi wetu.

Nilitegemea katika vipengele vya sheria hii, tungkuwa hata tunaweka *emphasis* kwa mfano kwenye *public relations*. Hata mimi Mbunge naogopa kuingia kwenye Benki Kuu, tena sasa baada ya *twin tower* ndiyo kabisa, naogopa hata kuingia sijui naingilia wapi! Sasa kama mimi naogopa: Je, wananchi wa kawaida wanafanya nini? Yule anayetaka kuanzisha Taasisi ameanzisha *SACCOS* yake, inataka kwenda kwenye *Financial Institution* anafanya nini? Hawezi kwenda kwenye yale majengo. Hatuna namna yoyote ya urahisishaji wa kwenda kwa Taasisi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linanipa wasiwasi, ningependa kama sio leo lakini mapema iwezekanavyo tufanye kazi ya kuona ni namna gani tunaweza ku-*facilitate* Benki Kuu ikawa ni *facilitator* kama zilivyoanza Benki za wenzetu. Nina mfano wa *RABO* Benki kule Uhulanzi. *RABO* Benki hata leo ndiyo inayo-*facilitate* Tanzania. Sasa inawezekanaje *RABO* kwenda mpaka Vijijini! Ndiyo inayosukuma *SACCOS* zetu ziweze kupata msaada, lakini Benki za kwetu hazifanyi kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufanyi kujifunza kutoka kwetu. Tuna *TIRDOS* Benki, nayo ni ya Uholanzi inafanya kazi kwetu leo hii. Ina-*facilitate* kwenye Vijiji vyetu na ndivyo walivyofanya huko kwao miaka mia moja na kitu iliyopita na wamewezesha kuwaweka watu na *spirit* ile ile wanaiendeleza leo kusaidia wale watu wadogo wadogo waweze kupata msaada kutoka kwenye *Financial Institutions*. Ni kwa msingi huo Ulaya hakuna mtu hata mmoja anayejenga nyumba kwa hela ya mfukoni mwake. Ni kwa msingi huo, hakuna mkulima anayekwenda kulima shamba kwa trekta aliyonunua yeye kwa sababu hawezি kununua trekta, anajua anakwenda kukopa hela Benki. Ni kwa msingi huo huo hata usafiri, wenzetu hakuna mtu anayekwenda dukani anatoa hela kutoka mfukoni, sisi tunabeba hela na magunia tunakwenda kununua gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kutoka kwenye hali hii kama hatutabadilisha mawazo. Kinachotakiwa ni *mindset* yetu ibadilike ili tuweze kuingia kwenye mfumo mzima, tunapozungumza kupiga vita umaskini tuanze kwenye Taasisi ambazo ni silaha muhimu (*tools*) katika kuleta haya mabadiliko.

Ninashukuru sana Gavana amekaa Marekani, tena Gavana wetu amekaa kule, nina hakika katika uchumi aliojifunza aliona wenzetu Wamarekani walifanya nini. Ningependa kuona zile *spirit* za wenzetu zinasaidia. Wenzetu sasa hivi wanakwenda kwenye *cards*, lakini *cards* hizo tutakuwa nazo sisi Wabunge. Mimi naweza kwenda mahali popote leo nikachukua hela kwa kutumia *ATM*, mwananchi hajui kitu kinaitwa *ATM*. Mwananchi anahitaji kutoka kwenye *sequence* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea katika kifungu hiki kikubwa kidogo kinachozungumzia *limit* ya fedha kwa *Financial Institutions*, nadhani ni kifungu cha 17(1) na 17(2) tunazungumzia bilioni tano kama *minimum*. Wenzetu walianza na viwango vya chini ili wananchi waweze kujiunga. *SACCOS* inapaswa kwenda kwenye *principle* ya aina hiyo iweze ku-*facilitate transactions* zile muhimu za kibenki zifanyike hata na *SACCOS*.

Katika Wilaya, *SACCOS* inaweza ikajiunga ikawa na *apex* ya *SACCOS*, lakini wakaunda Benki yao. Lakini ukiwawekea *limit* hawawezi kwenda kufanya *transaction*. Kitu muhimu katika *Financial Institution* ni uwezo wao kukopeshana, lakini vilevile ku-*facilitate transaction* za fedha ziweze kufanyika bila kuwezesha. Hii haiwezekani na tumeweka bilioni tano. Ni *limiting* kwa wengi wa *SACCOS* zetu ambazo pamoja na nia njema lakini hatutaki kuziwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashtuka zaidi ninapokuta kwa mfano, kwenye kifungu 17(2), pale tuna nia ya kuzungumza inasema: “*For the purpose of encouraging provision of banking services to underserved communities whether rural or urban.*” Lakini hatukuweka mazingira ya *rural*, tunaweka sentensi moja katika sheria nzima yenye vifungu zaidi ya 50, lakini tuna kifungu hiki kimoja kinakwenda zaidi kwenye *rural*. Mimi nilitegemea hapa tungekwenda kwa *details* zaidi, tunasaidia vipi hao watu tuliowaita wa *rural* yaani wa Vijiji ambao wanahudumia asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania! Benki zetu leo zinasaidia watu tulioko Mjini na Mjini ni asilimia ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa wakati wa kujibu, Mheshimiwa Waziri anisaidie nijue ni watu wangapi Watanzania wanatumia huduma za Benki. Hiyo ndiyo itatuonyesha kama sheria tunayotunga, tunaitunga kwa nchi nzima au tunatunga kwa ajili ya kikundi cha watu wachache kama akina Dr. Slaa na sisi tuliookaa hapa ndani.

Tunapotunga Sheria, ni vyema ilekee zaidi kuwawezesha kutoa nguvu, kutoa uwezo kwa watu walio wengi ambao ndiyo wanazalisha sehemu kubwa. Wakulima wanazalisha zaidi ya asilimia 50 na kuleta kwenye *GDP* ya nchi hii. Lakini hatuna *facilitation* hapa ambayo inawaelekea. Wako mmoja mmoja, wana matatizo, hawawezi *ku-access* hizo fedha, wanaogopa zile Taasisi kwa sababu haziendani na wao. Benki zetu usipokuwa na tai nina mashaka, tumerudi kule tulipokuwa. Usipoingia na tai kwenye Benki nafikiri hata unawenza ukaondolewa ndani ya jengo la Benki. Sasa hapo tunajenga watu wa aina gani? Tunajenga Taasisi ya aina gani? Kwa hiyo, nilitegemea kifungu hiki kingesaadia kwa kwenda ndani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa na *debate* juu ya Shilingi bilioni 200 au inayokaribiana na bilioni 200 za kujenga *twin tower*. Nilitegemea hizi fedha ndiyo zingeelekezwa huko kwenye Taasisi hizi za chini ziweze kujikwamua. Mtanzania hahitaji majengo makubwa, *security*, unaweza kuijenga kwa namna nyingi tu. Hata nyumba ya tembe ukiweka mashine zako za kisasa ukalinda zile fedha, lakini ukapeleka huduma zikawa katika nchi nzima na baadaye ukajenga maghorofa makubwa kutokana na hao hao watu wadogo. Hizi fedha zingeelekezwa zingesaidia kunyanya hata *provision*, hakuna mfuko, hakuna chombo ambacho tunakiunda. Tumeunda chombo ambacho kitakwenda wakati wa ufilisi (*liquidation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nilitegemea chombo kizuri zaidi ambacho kazi yake ni kwenda *ku-facilitate* hizo Taasisi ndogo ndogo, hizi *SACCOS*, hizi Taasisi ndogo watu wamejiunga pamoja, wanaunda Benki yao. Nilitegemea tuna mfuko mzuri na mkubwa ambao unawenza kutusaidia tukaelekea sasa kwenda kuondoa umaskini kutoka kwa watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma ile *draft* ya Kamati ya Mheshimiwa Anne Makinda, tuna fedha nyingi zimezagaa huko Mitaani, kuna watu wetu wengi wanafanya kazi nzuri hawana hata *Bank Account*, lakini hawana *Bank Account* kwa sababu hizi zilizoko siyo *accessible* kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninadhani kwa sasa tutakuwa tumechelewa, lakini ningependa kama tunafuta Sheria 342 na kuweka hii mpya, tufikirie mapema iwezekanavyo wakati wa utekelezaji ni namna gani tutaunda sasa vyombo vipyta ndani ya Sheria hii *by way of amendment* ambazo zitakuja mapema haraka iwezekanavyo ili tuweze kuona ni namna gani tutaleta *spirit* mpya, tutaleta mawazo mpya, tutaona kazi kama ile ya *De Soto* ya *informal sector* zinakuwa *translated* kwa kiwango gani katika kumsaidia Mtanzania kwa njia ya *Institutions* tunazotengeneza na Benki yetu ikaacha tu kuwa chombo cha kudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti ni muhimu. Napenda usalama wa fedha zangu! Nakumbuka huko nyuma tumekuwa na Taasisi kama *Caravan* imechukua fedha ya watu. Nakumbuka kuna Upatu umechukua fedha za watu, fedha zimepotea, tumelalamika sana na wengine ni watu wa Ikulu pia walihusika na ile *Caravan*, nilikumbana nao wakati ule. Ni kweli udhibiti ni muhimu, lakini udhibiti usiwe lengo pekee tunapokuwa na vita kubwa zaidi kama vita vya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani kwamba hilo niliseme na niliseme kwa uchungu kwa kiwango hiki kwa sababu nilipata manufaa ya kupelekwa nje nikaona wenzetu walikoanza, nikaona walifanya nini na sisi leo tunataka kufanya nini na nini kinaweza kuleta manufaa kwa mtindo ambao tunautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo sana na Muswada kama ulivyo, lakini ningependa niseme kile kifungu cha 24(4) ambapo Benki zinaweza kwa kibali cha Benki Kuu kuingia kwenye *commercial operations*. Mimi sina tatizo na kifungu jinsi kilivyo, lazima kibali kipatikane kwa sababu tunahitaji kulinda pia. Lakini ningependa iwe zaidi na *facilitation*, kuwe na *aspect* ya *promotion* katika hili kwamba biashara peke yake ndiyo itakayotusaidia hatimaye. Kama kuna biashara kati ya mkulima wa Mpanda aliyelima mahindi yake hana soko, anayaweka kwenye *godown* yanaozea huko na huko kwingine kuna mwenye nyanya hatujaangalia namna gani tuta-*facilitate* hizi kwa kutumia *Financial Institutions* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa *aspect* hii tu-*develop* vizuri na labda kungekuwa na *branch* katika Benki Kuu kwa kuwa ndiyo *monitor* ambayo ingelisaidia. Nimeiona hiyo kwenye *Reiffelsen Bank* kule Ujeruman. Wao wana kitengo kabisa, kazi yake ni kwenda kuzunguka Vijijini. Sasa Benki Kuu ya kwetu wataaka kwenye *twin tower* lakini wenzetu wanazunguka Vijijini, kitengo kabisa kimepewa na magari kinaitwa *promotion service* kwa kijerumani. Kinakwenda kwa wakulima kinaangalia ng'ombe, kinaangalia mazao ya yule mkulima na wanawahamasisha namna gani wajijunge pamoja ili waweze kutumia ile Benki yao ndogo, hiyo *Reiffelsen* iweze kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *of course* sio kazi ya Benki kufanya biashara, lakini ina-*facilitate* biashara. *Ita-create* namna ya wale watu kuweza kuwa na *business commercial relations*. Watanzania hawajui biashara. Watu wetu hatuna namna ya kuweza kuwafundisha biashara! Sio kazi ya Benki Kuu, lakini Benki Kuu ina nafasi kubwa katika ku-*facilitate* hao watu wakaingia kwenye biashara kwa kutumia mtindo wa fedha zinavyosafirishwa, malipo yanavyofanyika, watu wanavyohakikishiwa kwamba hakuna kinachoharibika kwenye biashara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tuna kitu kikubwa cha kujifunza kwa wenzetu na sielewi ni kwa nini tulipelekwa Ujeruman kwa sababu wale ni *very much advanced*. Lakini tulipofika kitu kikubwa walichotuambia, walituambia kwamba mwaka 1990 sisi tunapotatembelea, kiasi cha maziwa tunachopata kwa ng'ombe Tanzania ni kiasi ambacho Mjerumani alikipata mwaka 1870. Hili ni jambo la ajabu sana. Sisi leo tuko karne ya Sayansi na Teknolojia *we don't need to re-invent the wheel*, lakini toka walivyokuwa mwaka 1870.

Lakini yote haya ni kwa sababu gani walituonyesha *facilitation* zinavyokwenda, yule mkulima ana chombo cha kukamulia maziwa ya ng'ombe wake, chombo hicho hakununua kwa fedha yake ya mfukoni, amekwenda kwenye Benki yake hiyo ya wakulima. Benki ile imeweza kum-*facilitate*. Benki hizi tukiziunda zitaleta maajabu! Zitaleta mabadiliko makubwa, zitasaidia watu wetu kuachana na kutegemea fedha zinatoka mfukoni. Nadhani hata ujambazi, wizi, ubadhirifu unaweza kupungua sana kwa sababu watu watajua kwamba nikienda mahali fulani nitapata fedha halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *spirit* hii tusipoi-*develop* na sheria kama hii isipolinda sheria hizi, zitabaki kwenye vitabu, zitawasaidia watu wenye uwezo na hazitasaidia mtu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie athari wakati mwingine tunayoipata. Tumefanya *propaganda* kubwa sana, tumewahimiza Watanzania wanunue hisa, kwenye *TBL*, kwenye Sigara, hisa hizi ni watu wangapi zinawanufaisha? Mtanzania kama Mbunge, mimi nimeweza kununua hisa 300 na kwa mwaka naweza kupata Sh.11,000/= tu kutoka kwenye hisa zangu. Mtanzania wa kawaida ambaye hata Sh. 300,000/= hawezি kununua, atapata nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kwenda mbele zaidi, tunahitaji kujitoa kutoka kwenye usisi tushuke kwa mtu wa kawaida na tujiweke kwenye nafasi yao tuone tunataka kumsaidiaje katika karne ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ni imani yangu kwamba Waziri atanisaidia tuone wanaotumia hizi Benki ni wangapi na hizi Benki kama zinatumika *percent* zilizoko Mijini je tutawasaidia kwa kiwango gani hao wananchi walio wengi amba wako Vijijini na hatuna hata ndoto ya kuwafikia labda kwa miaka mingine labda 20 ijayo. (*Makofii*)

MHE. CHARLES N. KEENJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwa ufupi kabisa katika Muswada huu. Nitangulie kwa kusema kwamba naiunga mkono hoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuiwasilisha vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze na wewe kwa kukalia Kiti hicho. Kimekukaa vizuri kweli kweli! Unastahili, maana tulipotembelea Kongwa tulikutana na wale wananchi amba walikuwa wamenunua matrekta 29 katika mwaka mmoja Kijiji kimoja kwa kweli maendeleo tuliona yanaridhisha. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tujitawale ni miaka 45, lakini bado tunatafuta ni jinsi gani tumwezeshe Mtanzania aweze kupata mkopo aendeshe shughuli zake. Katika nchi hii ukitaka kujenga nyumba lazima uwe na fedha taslimu, ukitaka kununua gari uwe na fedha taslimu, ukitaka kufanya biashara lazima uwe na fedha taslimu. Kwa hiyo, mambo mengi tunayoona ni mambo ambayo yanatokana na watu kuchukua fedha kutoka mifukoni mwao kufanya mambo hayo. Huna, huwezi kufanya na kwa hiyo, unakwama.

Mabenki haya yaliyopo yatakwambia yanakopesha kilimo. Ukienda kuangalia wanakopesha nini, wanakopesha ununuzi wa mazao na uuzaji wa mazao nje na sio kulima mazao yale.

Kwa hiyo, wale wananchi 29 ambao mwaka jana walinunua matrektu mapya walinunua kutokana na akiba zao na wala sio kutokana na mikopo waliyopata kutoka Benki. Kwa hiyo, tunachozungumzia hapa ni nini tufanye sasa tupate utaratibu wa kuaminika utakaomwezesha Mtanzania kupata mkopo ili aweze kufanya shughuli zake ili tuweze kufikia kile tulichowaahidi wananchi wa Tanzania, “maisha bora kwa kila Mtanzania.” Haya maisha bora hayatatokana na Mabenki kuweka *liquidity* kubwa au kununua *government bonds* kwa ajili ya kujipatia faida. Itatokana na akiba za wananchi kuwekezwa katika uchumi ili zituwezeshe kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhishwa sana na huu utaratibu unaowekwa wa kusimamia Mabenki. Lakini naomba nipate usafanuzi maana huku nyuma tulianzisha vyombo ambavyo tuliviita Mabenki ambavyo huenda sasa vikaitwa majina tofauti. Tulikuwa na *Community Banks* na Mufindi ni maarufu, Dar es Salaam iko moja Kilimanjaro nafikiri na Kagera, tuna *Community Banks*.

Mheshimiwa Mramba alipokuwa Mbeya alianzisha Benki Kata, halafu tuna *SACCOS* na *SACCAS*. Hizi tunapenda tujue zina-fit VIP katika mfumo huu tunaouzungumzia katika Muswada huu. Mimi ningekuwa nimefurahishwa sana kama kungekuwa na sehemu maalum ambayo ingezungumzia hivi vyombo ambavyo vinakuja chini ya hili jina *Financial Institution* ili kufafanua masuala mbali mbali na masharti na utaratibu wa usimamizi ambao ungekuwa maalum kwa vyombo hivi. Lakini tunaambiwa kwenye kifungu cha 17 kwamba Benki itaweza kuweka masharti maalum ya kusimamia vyombo hivi. Natarajia masharti hayo yatakuwa katika kanuni ambazo na sisi tutapata nakala ili tuweze kuona ni nini kinachowekwa katika kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo kubwa tunahitaji mfumo wa kumwezesha mwananchi kupata mikopo ili tuweze kupambana na umaskini. Huyu mwananchi hatumtarajii kwamba atapata mikopo kuitia kwenye Mabenki yenyewe, tunatarajia kwamba atapitia katika *Financial Institutions* mbalimbali ambazo zipo na zile ambazo zitaanzishwa.

Katika hili ningeomba kwa kweli uwepo utaratibu mzuri sana wa kuangalia ni masharti gani tuweke kuhusiana na hizi *Community Bank*, Benki Kata, *SACCOS* na *SACCAS* ili kuziwezesha zitekeleze majukumu haya. Ninapopita kwenye Jimbo langu la Ubungo, ninakutana na akina mama wanaojitahidi kutafuta mapato ya kuendeleza familia zao, wanatafuta mikopo. Wameahidiwa kwamba watapata mikopo, sasa wanasema Mbunge sasa mikopo hiyo iko wapi? Wakati mwengine wanafikiri Mbunge ana uwezo wa kuwapa mikopo kutokana na kile alichonacho, wanakuta Mbunge mwenyewe kumbe ni maskini kama wao, kwa hiyo, ni maskini anajaribu kukopa kwa maskini.

Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na mfumo utakaowawezesha akina mama wale waweze kupata mikopo, kuwawezesha vijana wapate mikopo ya kuendesha biashara zao

ndogo ndogo, kuendesha viwanda vyao vidogo vidogo na kuendesha shughuli zao nyingine za kuwawezesha kuanza kujipatia mapato yatakayowezesha kukua na kuwa na Taasisi za kibiashara kubwa zaidi. Kwa hiyo, ufanuzi juu ya vyombo hivi ni muhimu sana.

Katika hatua hii niwapongeze sana *CRDB Bank* ambao wameweka mfumo maalum wa kushirikiana na hivi Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa ili kuviwezesha kuendesha shughuli zao. Wanawasaidia kwa kuwapa mitaji, mikopo, kuwasaidia vifaa na vile vile, kuwawekea usimamizi ambao ni madhubuti sana wa kuhakikisha kwamba wamefanikiwa. Ningombia katika Muswada huu ingebidi tutambue juhudhi kama hizi na tuweke utaratibu wa kuzipa Benki kama hizi *incentives* ili ku-*encourage* Benki nyingine zishiriki katika utaratibu kama huu kama walivyofanya *CRDB Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vyombo vinavyoitwa *Financial Institutions* viwe vya nyumba, viwe vya shughuli nyingine, ni muhimu sana kwa sababu ndivyo peke yake ambavyo vinaweza kumpa mwananchi mkopo bila ya kumdati dhamana ambayo inazidi uwezo wake. Ukienda katika hayo Mabenki makubwa wanakuuliza kama una mali isiyohamishika, kama nyumba. Ukiwaambia unayo, wanataka iwe na thamani mara tatu ya mkopo unaochukua na ukishindwa kulipa, wataiuzza pengine kwa kiasi ambacho wala hakifiki huo mkopo, wanaendelea kubaki na deni. Lakini hivi vyombo kama *SACCOS* na *SACCAS* na Benki Kata zinawawezesha wananchi kuweka utaratibu wao wa kudunduliza akiba zao baadaye kukopa na kwenda kufanya hicho wanachotaka kufanya na kurudisha. Mimi naona ndiyo jawabu la kuwasaidia wananchi ili waweze kupata mikopo bila ya masharti yale ambayo hawayamudu. Ningombia kabisa katika mfumo tutakaoanzisha, wa kusimamia hivi vyombo uhakikishe kwamba hivi vyombo tunavisaidia na hata kama ikibidi Serikali inachukua utaratibu wa makusudi wa kuvichangia ili kuhakikisha kwamba vinaanzishwa, vinakua na vinakuwa imara ili viweze kuwasaidia wananchi.

Sasa nikiangalia katika huu Muswada mara nyingi sana unazungumzia kwamba lazima uandikishwe kwanza ndipo uanze kuchukua fedha kutoka kwa wananchi. Tunapoanzisha *SACCOS* na *SACCAS* tunakwenda kwenye Mkutano tunaitana tunaanza kuchanga pale pale, kazi imeanza na pale ndipo patakapopatikana fedha baadaye ikituwezesha kwenda kuijandisha, ndipo patapatikana fedha ambayo kesho yake pengine tunaweza hata tukaanza kukopeshwa.

Naomba kazi hii ikubalike, maana vyombo hivi ni tofauti na Mabenki. Mabenki wanakuja watu wenye mapesa yao wanachangia kwa kununua hisa na utaratibu mwingine watakaojiwekea, kwa hiyo, wanaweza wakaenda. Lakini sisi wa *SACCOS* na *SACCAS* tunadunduliza kile kidogo tulichonacho na mara kikipatikana tunaanza kazi ya kukopeshwa wakati tunajiandaa kufanya haya mengine ya kuandikisha.

Kifungu cha 17 sehemu ya Pili inasema: “Benki itakuwa na uwezo wa kutoa masharti yatakayozingatia mazingira maalum yatakayokuwepo”. Mazingira maalum ndiyo hayo. Kutambua kwamba pale Kijijini sisi tukianzisha chombo chetu cha Kuweka

na Kukopa tunaanza kukopeshana hapo hapo kwa sababu ndio tumepata kamtaji hako wakati tunatafuta fedha za kwenda kufungua akaunti Benki na kwenda kufanya hizi shughuli nyingine. Lakini suala la usimamizi ni suala muhimu, suala la uongozi wa vyombo hivi ni suala la umuhimu sana na mimi nakubaliana kwamba katika usimamizi tusitofautiane sana na ule utaratibu tuliouweka kwa ajili ya Mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo nitaomba Waziri atufafanulie wakati atakapokuwa anahitimisha hoja yake, ni kwamba kwa mfano hizi *SACCOS* na *SACCAS* ni Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, sasa hivi vinasimamiwa chini ya Sheria ya Ushirika, vinakaguliwa kuwa na Maafisa Ushirika na kadhalika. Sasa uhusiano utakuwaje kati ya Benki Kuu na hivi vyombo ambavyo vinasimamia hizi *SACCOS*, *SACCAS* na hizi Benki nyingine ambazo kwa kweli mfumo wake ni wa kiushirika zaidi kuliko ilivyo kwa hizi Benki kubwa? Maana hata ukaguzi wa *SACCOS* na *SACCAS* unafanywa na Maafisa Ushirika. Sijui kama tunaweza kufanya *at international standard* kwa hivyo vyombo vidogo vidogo. Kama tunataka Maafisa Ushirika wakague *at international standards* itabidi tuhakikishe kwamba wanapata mafunzo ya kuwaambia hiyo *international standard* ni kitu gani. Pengine tungkuwa na *National standard* ambayo inakidhi mahitaji ya kukagua vyombo hivi ili kurahisisha uendeshaji wake na bila kuweka ugumu ambaio sio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengine nafikiri tunayatafuta wenye. Sasa hivi hatuna chombo chochote kinachokopesha kwa ajili ya kujenga nyumba katika nchi hii. Tulikuwa na *Tanzania Housing Bank*, ilipokufa hakijaanzishwa tena chombo cha kutuwezesha kukopa. Nafikiri kwa ajili hii, Serikali ikaamua ianze utaratibu wa kujenga nyumba ambazo zikishakamilika zitauzwa kwa wafanyakazi. Lakini nafikiri utaratibu ule sio utaratibu mzuri sana. Utaratibu ambaio ungetufaa zaidi ni utaratibu ambaio ungejenga nyumba kwa ajili ya wananchi wote na kwa ajili hiyo tunahitaji tuwe na Benki ya Nyumba ama tuwe na Benki za Nyumba.

Sasa nafikiri tungeiomba Benki Kuu iangalie suala hili na ichukue hatua za makusudi za haraka sana za *ku-encourage* kuanzisha Benki za Nyumba ambazo sasa hizo ndizo zitakazotoa mikopo kwa watu wanaotaka kujenga au kwa Makampuni wanayotaka kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza ili wananchi kwa wingi zaidi waweze kupata nyumba. Serikali badala ya kuendelea na utaratibu huu kwa kweli hizi fedha wanazotumia wangeziwekeza katika Benki ambayo itapanua huo uwanja hiyo medani inayotuwezesha wengi zaidi kupata mikopo ya kutuwezesha kujenga nyumba. Maana hiki kikundi cha wafanyakazi ni kikundi kidogo, Watanzania ni milioni 35, sijui wanaotaka kujenga nyumba ni wangapi. Sasa fedha watapata wapi kama Serikali haitusaidii tukajenga nyumba hizi?

Nikikumbuka wakati huo huo kwamba Serikali ilishaahidi kwamba haitaingia katika shughuli kama hizi itaiachia sekta binafsi na itaaniszha Mabenki, kwa hiyo, kufanya shughuli kama hizi. Kwa hiyo, ningeomba hivi vyombo vinavyohitajika vya kumwezesha mwananchi kupata haya maisha bora viwekwe na kama ikibidi turekebishe vyombo vilivyopo ili viweze kutusaidia kufanya kazi hizi. Nimekwishasema kwamba wale ambaio wanashiriki katika suala hili tuanze kutafuta njia za kuwapa *incentives* ili

waweze kuwa ni wadau wanaoshirikiana na Benki Kuu katika kutekeleza mambo haya. Ningombaa sana hili tulishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limenipa matatizo na nimepata maswali mengi sana katika Jimbo langu la Ubungo ni ule utaratibu wa kurasisimisha mali ili uweze kwenda kukopa Benki. Sasa katika baadhi ya maeneo, wananchi wameshapimiwa maeneo yao, wameshapewa kitu kinachoitwa leseni, lakini akienda Benki akipeleka karatasi pale hakikubaliki. Tungeomba hili nalo litazamwe ili kumhakikishia mwananchi kwamba zile ahadi anazopewa na Serikali za kumwezesha kuinua ubora wa maisha yake kweli zinakuwa na maana ile iliyokusudiwa ama vinginevyo wanaona kama vile vinasumbuliwa.

Umeambiwa kwamba hii nyumba yako itarasimishwa na imerasimishwa, umepewa karatasi unakwenda Benki unasema hebu nipeni basi mkopo niende nikaimarishe ile biashara yangu; unaambiwa hapana hatutambui karatasi hiyo. Kwa hiyo, kunakuwepo mambo mawili, tamko la Serikali ambalo linatofautiana na msimamo wa Benki kuhusiana na suala hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja hii, namwomba tu Waziri anisaidie kufafanua yale ambayo sikuyaelewa sawa sawa na ambayo nimemworodheshea. Lakini matumaini yangu ni kwamba kuanzia sasa tutakuwa na utaratibu mzuri zaidi utakaomhakikishia mwananchi kwamba anaweza akapata mkopo wa kuimarisha shughuli zake. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu. Awali ya yote, kwa sababu ni mara ya kwanza kusimama, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa wetu Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake ambao ameuonyesha kwa siku hizi zilizokwishapita. Pia, nitoe shukrani kwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, Mawaziri, Spika, pamoja na Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa na kuingia katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Pia, napenda kutoa shukrani kwa wananchi wangu walionichagua toka Jimbo la Bukombe watu takriban laki nne na zaidi ya asilimia 60 wakakubali kwamba niwe mwakilishi wao katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nami ninaahidi kuwatumikia kwa uaminifu kama walivyoniamini wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri mwenye dhamana aliyetuletea Muswada huu ambao ni Muswada mzuri sana katika awamu hii ya utawala wa Awamu ya Nne. Ninaamini tulipokuwa tunapita kwenye kampeni tuliyokuwa tunayasema, sasa nina imani kwamba tutakwenda kuyatekeleza endapo Serikali yetu na sisi Bunge tutapitisha Muswada huu kama jinsi ulivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuongelea hasa katika mantiki ya Muswada mzima mkianza na *objective* yake. Muswada wetu umesema kwamba unakwenda kuangalia usalama lakini pia unakwenda ku-reduce risks kwa *depositors*. Hapa nilianza

kupata mawazo kidogo kwamba kama kusudi la Muswada huu ni kuangalia usalama na kuhakikishia usalama wa fedha za wananchi wetu, nikawa naangalia pengine sasa hii labda tuiangalie kwa upya sana kwa sababu yako maeneo mengine haya ya Benki, kwa mfano katika Jimbo langu na Wilaya yangu ya Bukombe hatuna Benki. Tunatembea Kilomita 100 kwenda na kurudi 200 na wananchi wetu wanahitaji sana kuweka fedha zao katika Benki. Hii inanipa shida. Ikiwa ni pamoja na Halmashauri zetu za Wilaya, wafanyabiashara, wafanyakazi na wakulima wachimbaji kwa sababu tumezungukwa na madini mbalimbali hasa ya dhahabu katika maeneo yetu. Kwa hiyo, inakuwa ni shida kwa kutokuwa na Benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikaona kwamba pengine sasa uwe ni muda mzuri kwa Mheshimiwa Waziri tunapopitisha Muswada huu tuangalie na maeneo kama ya Bukombe, nilisikia Mheshimiwa Yono alikuwa amelisemasema sana hili, basi tuwe na ulazima wa kuhakikisha kwamba zinakuwepo Benki au Taasisi zinazoweza kusaidia wananchi hao. Kwa sababu siku moja nimekuwa najaribu kuongea na watumishi pale kwenda Bukombe je, ule usalama wa Halmashauri zetu unakuwaje? Mimi nikaona kwa sababu hii tunatoa mamlaka, basi tuwe na nafasi nzuri ya kufanya shughuli hiyo, lakini pia tukikumbuka kufungua Benki katika sehemu ambazo hazina Benki kabisa kama Wilaya ya Bukombe ambayo nafikiri nimesema wakazi wake takribani laki nne ambao ni wengi sana kukaa katika maeneo magumu yenyehali hiyo tunahatarisha usalama wao na kuvutia ujambazi, kwa sababu fedha zao wanahifadhi majumbani kwa kukosa huduma ya kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *section* ya 10 (1) na (4), tulisema kwamba tunapotaka kuanzisha *SACCOS* au mtu anataka kuanzisha *MFC/MFI* kwamba ndani ya siku 90 taarifa zitakuwa zimeshatolewa kwa *applicant*. Mimi hili pia nilianza kuliangalia kwa sababu nakumbuka mwaka 2003 pale Bukombe tulitaka tuanzishe *Bukombe Community Bank* na akaja *consultant* kutoka Dar es Salaam.

Majuzi nilikuwa naongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri akawa anasema zilipokwenda Benki Kuu, hawakupata *feedback* yoyote ile. Nikaomba, labda kupitia mjadala huu pengine Benki Kuu wanaweza wakaona namna ya kutusaidia kwa sababu katika Muswada tumesema ndani ya siku 90 utajulishwa na kama kumekuwa *rejected application* watasema ni kwa nini wamekataa maombi hayo. Kwa hiyo, tujaribu ili kweli wananchi wanaotaka kuanzisha *SACCOS* kama hizi waweze kujua ni kwa nini tumekwama, tumepongukiwa nini ili mambo yetu yaweze kwenda sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *section 17*, wenzangu waliongea kidogo, lakini tunasema kwamba mtaji angalau bilioni tano, ninaamini sisi tunaotoka katika Majimbo na Wilaya ambazo bado ziko Vijijini inawezekana kabisa hali ya kuwasaidia wananchi wetu ikawa ni ngumu sana. Kwa sababu *SACCOS* tunapokwenda kuianzisha uwezekano wa kupata mtaji kama ule na hatimaye tuuite *Financial Institution* kule itakuwa ni ngumu. Mimi labda nikaona hili nalo wajaribu kuliangalia upya ili mtaji utoe nafuu kwenye *SACCOS* tuweze kuimarisha. Je, *SACCOS* tunazozihimiza sasa hivi tunapopita kwenye Mikutano yetu kwa sababu ziko *SACCOS* tunazihimiza, zinaanzishwa na watu wanaanza kukopeshana ili kurekebisha maisha yao. Mimi niombe tu basi tujaribu kuangalia kwa sababu tunahitaji kweli maisha bora kwa kila Mtanzania.

Sisi tumeona kupitia *SACCOS* zetu ni kweli wananchi wetu wanawenza wakafaidika sana. Kwa hiyo, tuwe na usimamizi wa karibu na kuendelea kusaidia mahali ambapo tunaona panahitajika papewe msaada, zaidi sana, nikizidi kusisitiza hasa katika maeneo na Wilaya ambazo hazina kabisa huduma kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *section 23(3)* hapa mimi sina tatizo kabisa katika *separation of power*. Kwa sababu nimeona jinsi inavyokuwa kwamba hiyo *Board of Directors* itakuwa *chaired* na *none executive* mbalimbali *BoT* pia kutakuwa na *internal auditor* ambaye ataripoti katika *committee* ya ukaguzi. Mimi nikaona kwa kweli utaratibu ni mzuri na nikazidi kusema kwamba sehemu kama hii tuikubali na iendelee kufanyika na ninaamini kwamba hata *institutions* zetu zitafanya kazi vizuri. Kweli katika Muswada huu malengo yake ni mazuri sana. Lakini kwa sababu malengo yake ni mazuri, basi tunahitaji tuangalie namna ya kuwawezesha wananchi wetu ili hata waweze kupata mikopo hiyo kwa urahisi sana hasa wanaokaa mbali na Benki. Kwa sababu wakisogezewa huduma hizi na tukalichukua kwa haraka, inawezekana wananchi wetu wakafanikiwa katika shughuli zao za kilimo, uchimbaji na kadhalika.

Nilikuwa najaribu kuangalia nilipokuwa nafikiri kwamba kama ni kilomita 100 kutoka Ushirombo kwenda Kahama ndipo wananchi wetu wakatafute mkopo. Bado katika Jimbo la Kahama na Wilaya ya Kahama na wao wanataka mkopo pale, Benki ilipo msongamano unakuwa ni mkubwa. Kwa hiyo, uwezekano wa wananchi kuhangaika kwenda na kurudi pasipo kukamilisha masharti inaweza zikawachosha na hatimaye wanawenza wakafikia hatua wakaona kwamba hawana msaada. Lakini mimi ninachoamini ni kwamba Muswada wetu ni mzuri na malengo yake ni mazuri, nina hakika kabisa ndani ya miaka mitano wananchi wetu watafurahia na maisha bora yatafanyika kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri. Jana katika kuwasilisha Muswada uliopita alizungumzia kwamba *CRDB* sasa inaweza kuendelea kufanya biashara ya *Microfinancing* kama ilivyo *Commercial Bank*.

Lakini naomba nichangie tena hapo hapo kwamba ni vizuri kama alivyoomba kuunda Taasisi au ki-*subsidiary* cha *Microfinancing* ingekuwa vizuri katika ufuutiliaji wa shughuli za Benki. Kwa sababu watapanua zaidi na lengo ni kuzihudumia hizi *SACCOS*. Sasa kama wana kitengo maalum cha *Microfinance as a subsidiary* watakuwa wanawenza kwenda kila sehemu ya nchi yetu na ndiko tulikoahidi watu huko Vijijini kwamba fedha zitapitia kwenye *SACCOS*.

Udhibiti ni mzuri, sina kipingamizi, lakini kuwe na *flexibility*. Sasa wao *CRDB* ninavyojua wanatoa mikopo ile kwa *SACCOS* bila *collateral*. Lakini katika kutoa mikopo hiyo, wana *retain 25%* ya mkopo ule kwenye akaunti ambayo inaitwa Juhudi na

inapata *interest* ile akaunti. Halafu wanakuwa na *close supervision, close monitoring* na *follow up* kwa maana ya kuzilinda zile fedha. Halafu vizuri zaidi *SACCOS* inamkopesha mtu ambaye anamjua. Miradi kama hiyo imefanyika sehemu nyingi, mimi bahati nzuri nimefanya kazi katika Taasisi hii kwa miaka 22, kwa hiyo, naijua.

Kigoma tulikuwa na mradi kama huu. Tunawakopesha wavuvi wadogo wadogo zaidi ya 600 katika kipindi cha miaka 10. Hatukutumia *collateral*. Tunakwenda Kijijini, Serikali ya Kijiji na sisi tunakaa tunawa-*interview* waombaji, baada ya pale mwombaji anatoka, sisi tunakaa na Serikali ya Kijiji unamwonaje huyu mtu wao wenyewe wanajuana kule. Wanasema aah, hapa ukipeleka fedha ndio umezika.

Through that, ile project ilifanikiwa na ikapewa sifa sana na hata nchi za nje wametualika kwenda kuelezea tumefanyaje. Sasa CRDB moja ya sharti ambalo najua jana ilijibowi tangu mwezi Mei wamepelekewa masharti ya kufanya, kuna sharti moja wanashindwa la kusema lazima wakopeshe na collateral. Wao wanaingia Mkataba wa ubia na SACCOS na hawadai collateral. Lakini BoT tukiweka lazima wadai collateral kwenye SACCOS, basi watakuwa wanakataa indirectly, ku-sunction SACCOS kama kiungo cha wananchi na Benki.

Kwa hiyo, ndio kusema kwamba unawanyima wasikopeshe *SACCOS*. Ndiyo hapo tuwe *flexible* na *control* ibaki vile vile na wao wenyewe labda wahimizwe kuwafuatilia *BoT* waulize Mabenki, wewe bwana umekopesha *SACCOS*, lakini mbona zinafanya vibaya! *CRDB* kwanza ilifanya majaribio Mikoani kwa mfano Morogoro, Dodoma, Iringa na Mbeya wakaona *success 100% repayment*. Sasa wanaupeleka nchi nzima wanakutana na *snag* kama hiyo. Ndiyo maana tunasemea sana kwamba pawe na *cultural change*. Kama tunataka kubadilika kuwaendea hawa watu kuwe na *change* vile hata katika kuwfikiria kwamba sasa hivi *agenda* iliyopo ni ya mtu wa Kijijini.

Tabadilike kimawazo kwamba *agenda* ya sasa hivi katika nchi ya Tanzania ni kumshughulikia mwananchi wa Kijijini ili apate mikopo na sisi kama wanasiaya tumeliimba kwenye kampeni na watu wanangojea matokeo. Naiomba sana Benki au Serikali ilegeze pale ili iwahimize *CRDB* wahakikishe fedha hizi hazipotei kwa kufanya *follow up* ya mara kwa mara na *loan supervision* nzuri.

Katika kukopa sio *collateral* peke yake, inaweza kuwa ni jambo la kulinda fedha zile. Tabia ya mtu ni kitu kikubwa sana (*character*). Katika vigezo vitano vyta ukopeshaji *character* inawekwa namba moja, umjue yule mtu. Ukitumia, una uhakika wa usalama wa fedha yako. Kwa hiyo, hapo tusiogope sana kwenye hizi *Microfinancing* kwamba fedha zitapotea ovyo, *SACCOS* wana wafahamu wateja wao. Mimi nina *SACCOS* zinafanya vizuri katika Jimbo langu la Kilombero, ziko pale Kidatu, Mang'ula, Ifakara, Mlimba na tunazianzisha nyingi tu kwa ajili ya kuendeleza zao fulani au biashara fulani wanayoifanya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofsi*)

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba na mimi nikupongeze kwa kukalia Kiti hicho kwa mara ya kwanza. Pia, naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na timu yake, inaelekea Mkutano huu wa tatu hoja zote na Miswada yote inahusiana na Wizara ya Fedha itashughulikiwa ipasavyo. Kwa hiyo, nampongeza kwa kazi nzuri ambayo anaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha, nimeshiriki sana karika Muswada na kuuboresha na mengi nimeyatoa katika vikao vyetu vya Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini pamoja na hayo, yapo machache ningependa niyaongelee wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee juu ya mikopo ya nyumba. Mchumi akitembea katika Tanzania akaenda Masaki, akaenda Mikocheni, Arusha, Bukoba, akaangalia majengo yote yaliyosimama na akaelewa kwamba majengo haya yamejengwa kwa pesa taslimu, anapata masikitiko makubwa. Anapata masikitiko makubwa kwa sababu katika uchumi pesa hizi ni pesa ambazo hazizunguki. Ni pesa ambazo zimefunganishwa ndani ya matofali, nondo mchanga na kokoto, haziwezi tena kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunaongea juu ya wenzetu, kuhusu ushindani katika masoko ya Afrika Mashariki, tunajiuliza kwanini wenzetu wanasonga mbele haraka? Suala moja ambalo linajitokeza ni kwamba watu katika Tanzania tuna shida ya mitaji. Lakini sehemu nyingine, jibu kubwa la masuala haya ya ukosefu wa mtaji kwa wafanyabiasha wetu, kwa sisi Watanzania, ni kwamba pesa zetu nyingi tumeziweka ndani ya majengo, kwa sababu tuna tabia na hulka ya kusema ukishafikia umri fulani lazima ujenje nyumba yako, uiishi katika nyumba yako mwenyewe. Lakini ukiangalia kushoto na kulia hakuna njia ya kuweza kupata mkopo wa kujenga nyumba hiyo.

Kwa hiyo, unatumia *resources* zako mwenyewe, pesa taslimu ambazo unazo unazitumia kujengea nyumba ya kuishi. Lakini pesa hizi ndizo ambazo ungewekeza ungekuwa umepata mkopo wa kujengea nyumba, ndizo ambazo ungejengea kiwanda kidogo na ukaweza kushindana na wenzako na washindani wengine kutoka nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiasa Serikali iweke chagizo, iyawekee Mabenki chagizo yaweze kutoa mitaji ya *house finance* na yaweze kutoa pesa kama mikopo ya kuweza kujengea nyumba. Nasema Serikali iwasukume kidogo kwa sababu kila Mwekezaji hataki kuwekeza ambapo kile ambacho wachumi wanakiita *pay back period*, muda wa kurejesha zile pesa, unakuwa ni mrefu. Mabenki yatakuwa yanaridhika, yanaonekana kwamba yanakopesha kwa muda mfupi yanapata faida nzuri. Kwa hiyo, hayatapendelea yenyewe kujielekeza katika kukopesha mikopo ya muda mrefu.

Mikopo ya muda mrefu ina-*risks* zaidi, kwa sababu jinsi ambavyo unashubiria kurejesha ambacho umekiwekeza, ndivyo jinsi ambavyo ambacho umekiwekeza kinakuwa kwenye *risks* na unaweza ukakipoteza. Kwa hiyo, nazidi kuiasa Serikali ijitahidi iweke msukumo iyahimiza mabenki yaweze kutoa mikopo ya muda mrefu, *development finance* na *mortgage finance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maneno kwamba Watanzania hatukopesheki. Watanzania tunakopesheka kwa sababu Benki ambazo zimeanza biashara hapa Tanzania, rekodi inaonyesha kwamba wanapata faida kubwa sana ambayo hata mtu mmoja amediriki kuiita *immoral profits*. Angalia kila robo ya mwaka mahesabu ambayo yanachapishwa na Mabenki haya, utakuta yote yanatengeneza faida kubwa sana na hayapotezi pesa katika ile mikopo ambayo wananchi hawalipi. Ukiangalia mahesabu yao, kwa uhakika hawaweki hata tunayoiita *provision for bad debts*. Kama ipo, inakuwa ni ndogo sana. Ni ndogo sana kwa sababu Watanzania wanakopesheka na wanalipa. Kwa hiyo, tuwahimize hawa wenze Mabenki wazidi kuwakopesha Watanzania mikopo ya muda mrefu ya kujengea majumba wakiwa na uhakika kwamba pesa zao zitalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kidogo niongelee juu ya *SACCOS*. Watu wengi wakisimama wanaongelea *SACCOS* kama mkombozi wa jamii ya Watanzania hasa walioko huko Vijijini. Hili ni kweli, *SACCOS* tukiziendesha vizuri, tukiziimarisha zitakuwa mkombozi wa Watanzania ambao wako Vijijini. Lakini tuelewe kwamba hizi *SACCOS* zina *limitations* zake. *SACCOS* zinaweza zikatoa mikopo midogo midogo ya kulipa *school fees* ya vijana wanaosoma, mikopo ya kusaidia miradi midogo midogo ya kushona cherehani, ya kushona *uniform* za watoto.

Lakini *SACCOS* haitaweza kutoa mikopo mikubwa ya kuleta maendeleo na maisha bora kwa haraka. Tunahitaji huduma za kibenki ili kuweza kusonga mbele haraka kidogo zaidi; kwa mfano, miradi ya kununua matrekta. *SACCOS* haiwezi kutoa mikopo ya namna hiyo. Tutahitaji mikopo kutokana na Mabenki ili tuweze kununua vitu kama matrekta, ili tuweze kuendesha viwanda vidogo vidogo katika maeneo yetu, kwa sababu *SACCOS* mitaji yake ni midogo itaweza kusaidia katika mikopo ya kusaidia mambo madogo madogo.

Kwa hiyo, ni muhimu kwamba lazima Serikali isaidie kuhimiza kusukuma na kufanya Mabenki kuweza kusambaza mitandao yake katika maeneo yote ya Tanzania na hasa hasa katika maeneo ya Vijijini. Lakini pia niiase Serikali kwamba iwe na uangalifu zaidi, isaidie *SACCOS* hizi kwa ungalifu zaidi, iweze kuhimiza ukaguzi wa Benki Kata hizi ili hapo tunaposonga mbele wananchi wanavyowekeza pesa zao katika *SACCOS*, isije ikatokea baadhi yake kuanza kuanguka. Zikianza kuanguka na pesa au *deposit* za wananchi zikaanza kupotea, basi imani katika vyombo hivi itatoweza na itakuwa ni vigumu kuirudisha tena na wananchi wataachana na kutumia *SACCOS* hizi. Serikali ijitahidi kutumia vyombo vyake ihakikishe kwamba *deposits* za wananchi zinalindwa na inatoa msukumo kwa wananchi kuendelea kuvitumia na kuvijenga vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo juu ya matumizi ya *cheque*. Tunayo Mabenki yanatoa huduma yana-*checking accounts*, lakini kimsingi watu wengi ambao

tuna-*cheque books* za Mabenki, unakuta *cheque books* hizi zinakuwa ni za kwenda katika Benki na kutolea pesa humo humo ndani ya Benki. Mimi nadhani tunahitaji kuwe na msukumo wa kuweza kufanya wananchi wakaweza kutumia *cheque leaf* kwenda katika shughuli zao za kila siku. Ukienda kwenye Kituo cha *Petrol* uweze kutumia *cheque leaf* yako. Ukienda kwenye duka kubwa, *super market* au duka la vifaa vyatya ujenzi uweze kutumia *cheque leaf* yako. Itasaidia pesa hizi zisichafuke, itapunguza ujambazi, itasaidia katika maeneo makubwa na kuleta maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee suala la *NMB*, katika mjadala wa Benki Kuu ambao tumeumaliza. Katika mjadala huu, inaelekea kwamba kutegemea tu Mabenki ya kigeni hakutatusaidia haraka. Inaeleke kwamba Benki ambayo itatusaidia hasa huko Vijijini ni Benki ya *NMB*. Sasa tunaelewa kabisa kwamba sera ya chombo chochote iwe Kampuni, iwe ni Shirika huwekwa na wanaokimiliki chombo hicho na sio wale wanaokitumia.

Kwa hiyo, ili tuweze kuwa na mamlaka juu ya *NMB*, ili tuweze kuielekeza *NMB* iende Vijijini ikasaidie wananchi wa Vijijini, ni lazima sasa katika uuzaaji wa hisa ambazo zimesalia ambazo zimo mikononi mwa Serikali, Serikali iangalie kwamba hisa hizi zinamilikishwa kwa Watanzania na Watanzania wote katika *style* ile ile ambayo hisa za *CRDB* zilisambazwa.

Hata mimi nasema kwamba hata tumuuzie hisa hizo Mtanzania mmoja au Kampuni ya Kitanzania, nasema sio suala zuri kabisa. Suala ni kuwamilikisha Watanzania walio wengi katika *style*, kama mnakumbuka ambayo *CRDB* ilitumia ili kusambaza katika Mikoa yote na kwa Watanzania walio wengi. Tukishakuwa na hiyo Benki tutakuwa na kauli katika Benki hiyo. Tutaiagiza ifanye kama tunavyotaka iweze kusambaza huduma zake na kuangalia wananchi walio katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nimpongeze tena Waziri wa Fedha kwa kuleta Muswada huu na nataka nieleze kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. RICHARD S. NYAULAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Awali ya yote nimpongeze Waziri kwa kuleta hoja hii Bungeni na kwa michango mbalimbali ambayo imefanyika na Gavana wa Benki Kuu na vilevile nampongeza Mwenyekiti wa Kamati na Mwenyekiti wa Upinzani kwa kuweza kufanua zaidi kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vyatya fedha zimekuwa zikiongezeka kwa kasi kubwa sana katika nchi yetu. Vipo vingi hivi sasa. Tunaweza kuwa na Mabenki pamoja na Taasisi za fedha zinazozidi 36. Lakini sehemu kubwa ya Mabenki haya na Taasisi hizi za fedha zipo Dar es Salaam, zipo Mwanza, Arusha na sehemu chache katika Manispaa zilizopo. Kwa maana hiyo, huduma ya Benki hizi pamoja na Taasisi hazijaenea nchi nzima.

Vilevile natambua kwamba kuna Taasisi nyingi, kama *SACCOS* au Vyama vyatya Kuweka na Kukopa ambavyo vimeanzishwa Mijini pamoja na Vijijini. Kwa hivi sasa

kuna takribani Vyama vya Kuweka na Kukopa kama 12,600. Hivi ni vingi vya kutosha. Kwa hiyo, naipongeza Serikali pamoja na Benki Kuu kuweza kuleta Muswada huu kwa kuwa wadau wanaohusika na vyombo vya fedha wameongezeka kwa kiasi kikubwa sana na kunapoongezeka watu wengi, maana yake ni kuwepo kwa mambo mengi ambayo yanaweza kujitokeza.

Kwa hiyo, kuweka miongozo ya usimamizi wa fedha na Taasisi zake ni kitu cha msingi na kinachohitaji kupongezwa. Kwa hiyo, nawapa hongera sana. Lakini labda nijaribu kufafanua neno usimamizi. Natumaini wote tutakuwa tunaelewa tafsiri ya kusimamia maana yake ni kuzuia mambo fulani fulani yasitokee na vile vile ni kuendeleza mambo ambayo ni mazuri yanayostahili kuendelezwa katika jamii yetu. Kwa hiyo, itakuwa ni vizuri kama mambo yote mawili yatakuwa yanazingatiwa na vyombo vyetu katika hali ya kusimamiwa ili kuhakikisha kuwa fedha ambazo zinawekwa akiba na walalahoi zinatunzwa na zinalindwa. Vilevile kuwe na azma ya vyombo hivi viweze kuleta maendeleo kwa mwanchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchukua nafasi hii kutokana na mabadiliko hayo kuunga mkono Muswada huu na kwa hakika umeletwa katika muda muafaka. Kwa kipindi kirefu Benki Kuu imekuwa ikisimamia Mabenki na vyombo vya fedha vingine. Lakini nikiri hapa kuwa muda mrefu Benki Kuu haikusimamia Vyama vya Kuweka na Kukopa japoikuwa na wananchi wengi wamekuwa wakiweka hela zao huko. Kufuatana na historia ya ushirika katika nchi yetu kumekuwa na matatizo ya kila aina katika kuendesha Vyama hivi.

Kwa hiyo, naipongeza kuwa sasa Benki Kuu imeanza kuweka misingi ya kuweza kusimamia Vyama vya Kuweka na Kukopa. Kwa kuanzia, natumaini kufuatana na Muswada wamesema watasimamia Vyama vya Kuweka na Kukopa vile ambavyo vitakuwa vimefikia sifa ya kuwa kampuni ndogo za fedha, yaani *Microfinance Companies*. Lakini maana yake ni kwamba Vyama vya kuweka na kukopa ambavyo viko Vijijini na ambavyo ni vidogo zaidi bado vitakuwa havisimamiwi na Benki. Hiyo naiafiki kwa sababu Vyama hivi ni vidogo na vimekuwa ni vingi na inawezekana kwamba gharama ya kuweza kuvisimamia kutoka Benki Kuu itakuwa ni kubwa sana.

Lakini vilevile tukizingatia kwamba viko zaidi ya 12,000 maana yake ni kwamba kazi hiyo itakuwa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuweza kuhakikisha kuwa kunakuwa na tofauti kati ya usimamizi wa Mabenki pamoja na vyombo vya Kuweka na Kukopa vyenye sifa ya Kampuni ndogo viweze kusimamiwa na Benki Kuu lakini hizi *SACCOS* zetu au Vyama vya Kuweka na Kukopa viendelee kusimamiwa na Idara ya Ushirika chini ya Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya mpaka sasa Vyama vya Kuweka na Kukopa ingawaje vimekuwa vikisimamiwa na Idara ya Ushirika, bado kumekuwa na matatizo makubwa kwa sababu Idara hizi za Ushirika ni dhaifu sana. Usimamizi wake ni dhaifu na kwa sababu hiyo, hawana uwezo wa kuweza kuvisimamia Vyama vya Kuweka na Kukopa vilivyopo Mijini na vile ambavyo viko Vijijini. Kwa hiyo, ningeomba na ningeishauri Benki Kuu pamoja na Serikali iweze kuimarisha Idara hizi za Ushirika ili

ziweze kusimamia vizuri Vyama vya Kuweka na Kukopa maeneo ya Vijijini pamoja na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 6(2) inatoa adhabu kwa wale ambao watakuwa wanavunja Sheria ya Muswada huu. Inasema kwamba *fine* itakayokuwa inatolewa isizidi Shilingi milioni 20. Sina tatizo na kiwango cha Shilingi milioni 20, lakini nina matatizo kwamba kiwango cha chini hakipo. Inawezekana kuwa tunataka kutoa uhuru kamili kwa Mahakama lakini tumeona vilevile kwamba matatizo mengi yamejitokeza katika uhuru wa namna hii, watu wengi wameweza kulipishwa *fine* ya Sh.10,000/= kwa uhalifu mkubwa. Kama hizi *fine* zikiwa ni ndogo, maana yake ni kuwa watu wanaweza kudiriki na kuendelea kufanya uhalifu na ubadhirifu mkubwa kwa fedha za walalahoi.

Kwa hiyo, nashauri, kiwango cha chini cha *fine* kionyeshwe. Kwa hiyo, mtu akifanya kosa hilo basi kiwango cha chini cha *fine* kinaweza kuwa ni Shilingi milioni 10 lakini kisizidi Shilingi milioni 20. Ibara ya 10(1) katika Muswada, imeweka kipindi cha siku 90 kwa Benki kutoa leseni au kutoa majibu ya leseni kama imekubali au imekataa. Naipongeza Benki kwa kuweka kipindi hiki. Kwa kweli ni kipindi kifupi ukilinganisha na utaratibu na mazoea ambayo tumekuwanayo kwa muda mrefu.

Wachangiaji wenzangu wameeleza kwa kiwango kikubwa sana kuhusu malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza huko nyuma katika kutoa leseni. Lakini maadam *BoT* imeweka kipindi hicho katika Sheria, mimi nawapongeza na kazi kubwa ni kuzingatia kipindi hicho. Vilevile nilikuwa nina imani kuwa kwa kuweka kipindi hicho kitaongeza uwajibikaji kwa Watendaji kazi katika Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17(1) inaeleza kiasi cha mtaji wa Shilingi bilioni tano ambacho kinahitajika kwa ajili ya kuweza kuanzisha Benki. Benki ni Taasisi kubwa, mimi naafikiana kabisa na kiwango hicho. Sasa hivi kiwango kilikuwa ni bilioni moja, lakini uchumi kutokana na kuwa na mahitaji na kiwango cha Shilingi bilioni moja kimeonekana kwamba hakitoshelezi. Kwa hiyo, naafiki kiwango cha Shilingi bilioni tano. Lakini katika kipengele cha Ibara hiyo hiyo 17 imeeleza kuhusu madaraka ya Benki Kuu kuweka viwango vya mtaji kwa Taasisi nyingine. Kinachonishangaza hapa ni kwamba kwa kuwa wameweka kiwango cha Shilingi bilioni tano katika Mabenki kuna matatizo gani kuweka kiwango katika Taasisi nyingine?

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hapa kungekuwa na viwango vilivyowekwa kwa Taasisi nyingine kusudi wale wanaotaka kuanzisha Mabenki au Taasisi hizo, basi waweze kujua kitu gani cha kufanya. Natumaini hiyo itaweza kupunguza urasimu ambao unaweza kujitokeza. Kwa hivi sasa kiwango cha kuanzisha *Community Bank* kimewekwa kuwa ni Shilingi milioni 250. Natumaini ni kiwango kizuri kwa Benki kama hiyo. Lakini kikizidi hapo inawezekana uwezo wa kuanzisha Benki hizi utakuwa ni mgumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba pamoja na kwamba kazi kubwa ya Benki Kuu itakuwa ni kusimamia, lakini vilevile ifanye kazi kubwa ya kuweka mikakati ya kuanzisha *Community Banks* kwa kuwa hizi ni Benki zinazoanzishwa kwa

kuwashirikisha watu mbalimbali yaani jamii yenewe. Zina uwezo wa kuwafikia wananchi wa aina mbalimbali ikiwa ni wale wenye uwezo pamoja na walalahoi. Lakini vilevile zinaweza kusambaa katika nchi nzima. Kama tukizungumzia *Community Banks* ambazo zinaanzishwa kwa ajili ya Wilaya. Maana yake ni kwamba tunaweza kuwa na *Community Banks* zaidi ya 130 katika nchi yetu. Hicho kitakuwa ni kiwango kikubwa sana cha Benki ambazo zimeweza kuenea katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, naomba Benki Kuu ifanye kazi ya kuimarisha Benki hizo. Ningetaka kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Mufindi, Mwanga, Dar es Salaam, Moshi na Mbanga kwa kuanzisha Benki za namna hiyo. Nina imani matunda ya kuweza kuwashirikisha wananchi katika kuanzisha Benki hizo yameshaoneka katika maeneo hayo na natumaini sisi Wabunge wengine tunastahili kuiga mfano huo.

Kwa hiyo, napenda kutoa rai kwa Wabunge wote kuwashirikisha wafanyabiashara mbalimbali, wafanyakazi na kuwashirikisha wakulima katika kuanzisha Benki hizi za *Community*, kwa sababu hizo ndizo Benki ambazo zinahitajika na wananchi na una uhakika kwamba Benki hizi kwa sababu zinakuwa kwenye Makao ya Wilaya itakuwa ni rahisi zaidi kwa kufanya kazi vizuri zaidi na Vyama vya Kuweka na Kukopa ambavyo ni vingi Vijijini.

Kwa hiyo, mwendo wa kutoka Kijijini kwenda kwenye Benki katika kila Wilaya utakuwa siyo mkubwa sana na kwa hiyo, kuwezesha Vyama vya Kuweka na Kukopa kutumia Benki za *Community* ili kuweza kufanyabiashara za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiwa na Benki hizi za *community* ambazo zimesukumwa na kuanzishwa, nina imani kwamba Benki Kuu kama ambavyo inaweza kutoa mikopo kwa Benki nyingine na Taasisi nyingine za fedha, basi *BoT* itakuwa na uwezo wa kutoa mikopo kwenye *Community Banks* ambazo ziko karibu zaidi na wananchi.

Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunahakikisha kwamba tunaimarisha Vyama vya Kuweka na Kukopa visiwe kama ni vyombo ambavyo vinatoa mitaji midogo midogo kama vingeweza kuimarishwa zaidi.

Kwa hiyo, ningeomba utaratibu uwekwe kusudi Benki Kuu ichague Taasisi mbalimbali kama vile *SCALT*, *NMB*, *CRDB* na *SELF* ikiwa ni pamoja na *Community Banks* ambazo zinaweza kufikia *SACCOS* mbalimbali katika Vijiji vyetu. Nina imani kwamba Taasisi hizi zikiimariswa maana yake ni uwezo wa wananchi unaweza kuimarika zaidi.

Lakini vilevile ningeomba Benki Kuu iangalie utaratibu ambao wanaweza kuutumia kwa kusimamia na kuendeleza Taasisi ya *TAMFI* yaani *Tanzania Association of Microfinance* ambayo kazi yake kubwa ilikuwa ni kujaribu kuviimariswa *Microfinance* sehemu mbalimbali na kutoa mafunzo na kuweza kusimamia.

Chombo hiki kwa sasa hivi kimefifia sana na hakioneshi kama kina kazi kubwa sana. Lakini kama kingekuwa kimeimarishwa, nina imani kwamba kingeweza kutumika vizuri sana katika kuendeleza Taasisi ndogo pamoja na *SACCOS* huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 22 inaelezea umuhimu wa Benki Kuu kuidhinisha au kupitisha Mkaguzi wa Mahesabu ambaye anachaguliwa na chombo au Tasisi inayohusika. Nachukua nafasi hii kuipongeza sana Benki Kuu pamoja na Serikali kuweka kipengele hicho kwa sababu itakuwa ni vizuri Mkaguzi anayechaguliwa anakawa ni yule mwenye uwezo na mwenye viwango ambavyo vinahitajika. Kwa kufanya hivyo itakuwa tunajaribu kuimarisha usimamizi wa Taasisi hizo.

Lakini vilevile ningetaka kutoa pongozi kwamba ripoti yake au ripoti ya Ukaguzi itapeleka kwenye vyombo vinavyohusika pia itapelekwa Benki Kuu. Hii itakuwa ni nafasi nzuri kwa Benki Kuu kuweza kuptitia ripoti hizo vizuri na kubainisha mafanikio na matatizo yote na kisha kuchukua hatua zinazohitajika ili kuviimarisha vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kwa kuunga mkono hoja hii ahsante sana.
(Makofî)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu kwa asubuhi hii umekwisha. Nina matangazo machache kwanza kwa Mheshimiwa yoyote ambaye chombo hiki ni chake aje achukue meza kuu baadaye kidogo.

La pili, naomba kuwakumbusha Waheshiwa Wabunge amba wana nia ya kuchangia Muswada huu kuhusiana na Sheria ya Mabenki na Taasisi za kifedha kwamba nafasi bado iko, bado iko fursa ya kutosha kabisa. Kwa hiyo, tufuate utaratibu unaotakiwa ili tuweze kuchangia Muswada huu.

Lingine ni kwamba wachangiaji wetu wa jioni watakaoanza kuchangia atakuwa ni Mheshimiwa Adam Malima - Mbunge wa Mkuranga, Mheshimiwa Nimrod Mkono - Mbunge wa Msoma Vijijini, Mheshimiwa Charles Kajeg - Mbunge wa Mwibara na Mheshimiwa Ponsiano Nyami - Mbunge wa Nkasi.

Baada ya kusema hayo, sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni hii.

(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mheshimiwa Anne S. Makinda) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, bado muda wetu wa kujadili Muswada huu upo. Kwa hiyo, kuna wale amba walifkiria tumefunga, hatujafunga. Bado tuna

lengo la kwamba tuufunge kesho. Kwa hiyo, bado orodha ya wachangiaji inaruhusiwa kuendelea.

Lakini la pili, pale nje kuna maonesho ya Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Waheshimiwa Wabunge, nawashauri kila mtu ajaribu kupata muda wa kwenda kuangalia kwa sababu yana uhusiano mkubwa sana na kazi tunazozifanya kule Vijijini na wengine mnaweza kukuta mengine ni ya Kitaifa.

Mengine ni ya maeneo yenu na mengine yapo tu mnaweza kuwasiliana nao, kwa sababu tunakokwenda ni vizuri tukishirikiana na hizi *NGOs* katika kufanya kazi zetu za Kibunge. Kwa hiyo, mnashawishiwa kwa sababu wana siku ya leo na kesho. Kwa hiyo mkipata muda wowote mnaweza kwenda kuangalia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Adam K. Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kajege na Mheshimiwa Ponsian Nyami, ajiandae. Mheshimiwa Misanga tafadhalii, atafuatiwa na Mheshimiwa Blandes.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake wote wawili pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, lakini vile vile Gavana na Watendaji wote wa Benki Kuu kwa kuleta Muswada huu mzuri ambao umekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niseme tu mapema kabisa kabla sijasahau kwamba naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. (*Makofii*)

(Hapa mitikisiko mdogo wa Jengo la Bunge ulitokea)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, tukuchukulie muda wako kidogo. Waheshimiwa Wabunge, hiki kinachounguruma siyo tetemeko la ardhi. Wanashindilia, unajua tena kuna ujenzi unaendelea hapo. Kwa hiyo, msije mkafikiria ni tetemeko. Kuna yalioyotupata siku moja humu ndani sisi wenyewe. Mheshimiwa Missanga, nakuomba uanze upya. (*Kicheko*).

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, natumia nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada uliopo mbele yetu. Lakini vile vile, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wote wawili, Katibu Mkuu, Gavana wa Benki Kuu na Watendaji wote wa Benki Kuu na wote ambao wamehusika katika kufanya Muswada huu uletwe mbele yetu katika hali ambayo ni ya kuridhisha. Nawashukuru sana na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Singida Kusini, naomba nitumie nafasi hii vile vile kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri ambazo amezifanya toka amechaguliwa na hata kufikia kumaliza zile Siku 100. Kazi nzuri ambayo kwa kweli inaashiria kwamba baada ya miaka mitano Mwenyezi Mungu akimpa afya yeche na Wasaidizi wake, nina hakika Ilani ya Uchaguzi itakuwa imetekelzeza kutokana na msingi mzuri ambao ameweka katika Siku 100 hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu watu wote wanaridhika. Hata rafiki zangu Wapinzani wanaridhika. Siku moja nilikuwa namsikiliza Maalim Seif akisema kwamba “Kwa hili namuunga mkono Mheshimiwa Kikwete.” Kwa hiyo, mpaka Maalim Seif akiridhika, basi nina hakika na wengine nao watakuwa wameridhika na hata katika Magazeti wanasesma sasa aah! kama ni hivyo basi Upinzani Mheshimiwa Rais Kikwete ameshaumaliza. Sisi hatuna sababu tena ya kung’ang’ania upinzani. Ndivyo wanavyosema wanachama wenu. Kwa hiyo, naomba nimpongeze yeche, lakini vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wanafanya mpaka Serikali ya Awamu ya Nne inaonekana inafanya kazi vizuri. Hongereni sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasikiliza wenzangu waliochangia Muswada ule uliopita na vile vile baada ya kuwasikiliza wale ambao wamechangia toka leo Muswada huu ulioko mbele yetu, kwa kweli mengi yamesemwa na ni matumaini yangu kwamba Serikali imesikia, kama tulivyomsikia Mheshimiwa Waziri jana akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama kusisitiza jambo moja tu. Inawezekana lina vipengele, lakini la msingi langu ni moja kwamba baada ya kutoa uhuru kwa Benki Kuu na Madaraka waliyopewa Benki Kuu, mimi nataka niwaombe sana tena sana waangalie namna ya kipeleka Huduma za Benki huko Vijijini. Hilo ndilo langu ambalo nataka nilisisitize nikiunga mkono yote yale ambayo yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge waliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba Jamii au Watanzania walio wengi wanaishi Vijijini. Wananchi wa Vijijini ndio wanahenyeka na kazi za adha na harubu. Lakini vile vile, ni ukweli kwamba wengi wao kule Vijijini hawafaidi matunda ya kazi wanayoifanya, lakini sisi ambao tunapata bahati ya kukaa Mijini ndio ambao tunafaidi zaidi kuliko wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadharia ambayo inasemwa na Serikali ni kwamba wananchi wa Vijijini wasaidiwe, wananchi wa Vijijini wafanyiwe hivi, lakini ukilinganisha nadharia na utendaji halisi, mimi naona kwamba iko *gap* kubwa sana kati ya nadharia inayosemwa na utendaji uliopo kule Vijijini. Wananchi wa Vijijini wana matatizo mengi na ndiyo maana vijana wetu sasa wengi wanakimbilia Mijini kutokana na adha ambazo zipo kule Vijijini na ile hali duni iliyoko kule Vijijini. Wenzangu wengi hapa ni Wabunge wanaowakilisha Vijijini, wanafahamu matatizo tuliyonayo na misukosuko ambayo tunapata kutoka kwa wananchi Wapigakura wetu wakitulalamikia jambo hili na lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tunapokuja katika habari ya Benki Kuu na habari ya fedha, hakuna huduma muhimu ambayo inaweza kumsaidia mwananchi zaidi ya fedha na vile vile habari ya mikopo. Kote duniani wale ambao wameendelea, wameendelea kwa msaada mkubwa sana wa mikopo. Sisi ambao tunajenga nyumba kwa pesa taslim na kununua magari na sijui na vitu gani, wanatushangaa wenzetu wengine tukiwaambia hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu katika hili ni kwamba Benki Kuu sasa kwa kweli iangalie uwezekano na iweke mkakati wa kuwasaidia wananchi walioko Vijijini wapate huduma za fedha na vile vile ndani yake suala zima la mikopo ili iweze kuwasaidia na washiriki kikamilifu katika kupiga vita dhidi ya umaskini kulingana na Sera mbali mbali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kama nilimsikia vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa akijibu hoja mbali mbali, alisema fedha yetu inapungua thamani mara kwa mara. Moja ya sababu ni kwamba *exports* zetu sisi ni chache ukilinganisha na *imports* ambazo tunapokea toka nje. Kama tungekuwa na bidhaa nyingi za kuuza nje, ingechangia au ingechochea fedha yetu ikaendelea kupata thamani. Sasa kama hivyo ndivyo, *exports* ili zipatikane, kwa kweli kuna haja sana ya kumtambua mkulima ndiye ambaye atasaidia kuongeza *exports* zetu ziende nchi za nje na hatimaye fedha yetu iweze kuwa na nguvu inayostahili.

Lakini mkulima huyu kama hapati mikopo, hapati msaada wa hali na mali atawezaje kulima mazao, atawezaje kulima kilimo cha kisasa na akapata mazao mengi ambayo yanaweza kusafirishwa nchi za nje kama vile Kahawa, Alizeti, Pamba na kadhalika? Wakati hatumsaidii na njia moja ya kumsaidia ni hii ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Vijijini kwa mfano, tulipoanzisha ile *NMB* walikuwa na mategemeo kwamba baada ya *NMB* kuanzishwa sasa watakuwa wamepata nafuu ya kupata mikopo. Lakini mimi mwenyewe nimepeleka watu kadhaa *NMB* na wanaambiwa kwamba: “Kama unakaa Kijijini sijui Kilomita 30/40 hatuwezi kukupa mkopo kwa sababu hatuna Watumishi wa kutosha wa kuweza kufuatilia mikopo huko uliko.” Kwa ajili hiyo, wanavijiji wengi hawapati mikopo ya kuwasaidia kuendeleza kazi zao mbalimbali. Kwa hiyo, narudia kusema kwamba wanaofaidi ni wenzetu ambao wako Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kwa kweli lazima ifike mahali iangaliwe upya na jitihada za makusudi zichukuliwe na Serikali yetu, lakini vile vile Benki Kuu itafute namna ambavyo inaweza ikashawishi Mabenki, hizo *Financial Institutions* ambazo tunazzungumzia katika Muswada huu ziweze kupeleka huduma kule Vijijini. Kwa mfano, naomba nishauri mawili:- Mpango wa muda wa kati kwa kweli ni kuangalia uwezekano wa kushawishi baadhi ya Benki kama *CRDB* ambao wameonesha kazi nzuri na uzalendo *NMB* ambao wameonyesha kazi nzuri na uzalendo angalau kuwashawishi hawa waanje na Tarafa. Kila Makao Makuu ya Tarafa angalau kuwe na huduma za Benki ama za *CRDB* au za *NMB* au *Financial Institution* nyine yoyote ambayo

inaweza ikapatikana ipeleke kwa kuanzia katika Tarafa zetu ili baadaye twende kwenye Kata zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *mechanism* gani inatumika? Nasema hiyo ndiyo kazi ya Benki Kuu, isaidie kuona kwamba wanabuni utaratibu, wanabuni mikakati angalau kufikisha huduma hizi katika Tarafa zetu kama mahali pa kuanzia. Lakini wakati jitihada na mikakati hiyo inaandaliwa, liko suala ambalo mimi naona inawezekana nalo kuwa na *Mobile Banks*. Katika nchi za wenzetu suala la kuwa na *Mobile Banks* ni suala ambalo linafanyika na linawezekana kwa utaratibu ambao wanapanga kwa kushirikiana na vyombo vya Usalama. *Mobile Bank* ya CRDB, *Mobile Bank* ya NMB, *Mobile Bank* hata ya NBC inaweza kabisa ikaenda Vijijini kufanya kazi ya kuwasaidia wananchi kuwapa huduma za Fedha ikiwa ni pamoja na huduma za mikopo.

Sasa *Mobile Bank* nayo ina matatizo gani? Magari yapo yanazurura Mjini kule saa zote hayana kazi yoyote. Yakiagizwa yakatengenezwa vizuri na ulinzi ukapatikana, watu wa Benki hao wanaweza wakaenda katika Tarafa zetu mbalimbali wakatoa huduma za Benki, lakini vile vile wakatoa huduma za mikopo. Kwa sababu utaratibu utakuwa umewekwa, wananchi wataambiwa na watahamashiswa kwamba kuna huduma za Benki sasa zinapatikana, tarehe fulani, siku fulani. Hata kama siyo kila siku, inaweza ikawa mara moja kwa wiki, inaweza ikawa sijui mara mbili, mara tatu kwa mwezi, ilimradi wajue tu kwamba kuna siku fulani inakuwepo huduma za *Mobile Bank* ama za CRDB, ama za NMB na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba wakati tukienda huko katika utaratibu wa kupeleka hizi Benki angalau katika Makao Makuu ya Tarafa ambazo bahati nzuri nyingi zina umeme na nyingine ziko njiani kupata umeme, kwa hiyo, mambo kama haya yanawezekana. Sasa wakati jitihada hizi zikifanyika, suala la *Mobile Banks* kwenda Vijijini, inawezekana. Hivi sasa Wizara yetu ya Afya inao utaratibu mzuri tu wa kupeleka *Clinics* kwa njia za *Mobile*. Wanakwenda kwenye Vijiji mbalimbali. Wizara ya Afya inafanya hivyo, akina mama wanafuatwa kule wanapimwa, watoto wetu wadogo wadogo wale wanaangaliwa. Sasa kama Wizara ya Afya inaweza ikafanya hivyo, ikapeleka *Mobile Clinics* katika sehemu mbalimbali, kwa nini Mabenki yetu nayo yasiweke utaratibu wa kuwa na *Mobile Banks* na wakaenda Vijijini wakasaidia kukidhi hayo mahitaji ambayo nayazungumza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado tunasisitiza kwamba wakati wa mpango wa muda mrefu wa kwenda kwenye Tarafa zetu, unaandaliwa lakini hili la muda mfupi yaani la *Mobile Banks* wanaweza kabisa ilimradi washirikiane vizuri na vyombo vya Usalama. Linaweza likapata ahueni. Tukipeleka huduma hizi katika Tarafa, nani atafaidika? Siku zote tumekuwa na tatizo hapa la kulipa mishahara ya Walimu na jitihada za Serikali zilifanya angalau kupeleka mishahara hiyo Vijijini, imeshindikana mpaka sasa Walimu wametakiwa kufungua Akaunti za Benki ambazo ziko Mijini ili kupata mishahara yao.

Lakini kama tutafikisha huduma hizi na utaratibu ukapangwa vizuri, tutakuwa tumetatua tatizo la Walimu kupata mishahara yao angalau katika Makao Makuu ya

Tarafa. Hilo moja litakuwa limemalizika. Vile vile, siyo Walimu pekee walioko Vijijini, wako Watumishi wa Afya, wako Watendaji wetu ilimradi wako Watumishi kadhaa walioko Vijijini wa Serikali Kuu ambao wako kule na wale wa Serikali za Mitaa ambao wanawenza wakanufaika kabisa kwa utaratibu huu wa kuwa na Benki katika Makao Makuu ya Tarafa ikiwa ni pamoja na *Mobile Banks* kwenda huko katika Makao Makuu ya Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile tumezungumzia Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inazungumzia habari ya MKURABITA, habari ya kurasimisha mali. Tayari jitihada zimeshafanyika baadhi ya watu wameshaanza kurasimisha mali zao wameshapata. Lakini wanamtaka mtu atoke kilomita 300/400 mpaka aende kutafuta mkopo kule Mjini.

Kwanza anatumia fedha nyingi, usafiri wenyewe ni wa matatizo, yeze mwenyewe hana pesa ya kumsaidia. Fedha hiyo hiyo unataka ahangaike nayo. Sasa kama utaratibu wa kupeleka *Mobile Banks* au Benki katika Tarafa utakuwa umekamilika, basi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa maana ya kwamba wale ambao tayari mali zao zimerasimishwa wanawenza wakapata mikopo ili kusudi iweze kuwasaidia kuinua uchumi wao na kwa hiyo kupiga vita dhidi ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya tatu, tunazo *SACCOS*. Tunazungumzia *SACCOS*, lakini *SACCOS* kule Vijijini wanatafuta mahali wao nao waweke pesa. Hawana uwezo wa kuweka pesa nyingi na matokeo yake wanakuwa na visenti visenti tu. Lakini kama hizi Benki zina utaratibu wa kwenda kwenye Tarafa zetu na hizi *SACCOS* nazo zinaweza zikapata sasa imani ya kuwa na fedha nyingi zaidi na kwamba wakija wale watu wa Benki, basi ama wanaweka au wanachukua kwa utaratibu ambao utakuwa umewasaidia kupunguza gharama za kwenda Mijini.

Mara nyingi kuna malalamiko kati ya wanachama kwamba *Administrative Cost* zinakuwa nyingi sana kwa miradi midogo midogo hii. Sasa ukimtaka yule Mkuu wa *SACCOS* kila siku aende Wilayani, aende wapi, atakuletea orodha kubwa sijui usafiri, malazi, chakula na mengineyo kiasi kwamba hela yote inakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo nayo inaweza ikasaidia sana namna ya kumsaidia huyu mwananchi au huyu kiongozi wa *SACCOS*. Kwa hiyo, *SACCOS* nao wanahitaji msaada huo wa Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hilo litawasaidia watu wa Vijijini kwa sababu sasa hivi hata hao *PRIDE*, hata hao *SELF* wote wako Mijini. Mtu wa Kijijini hapati. Unakwenda pale *PRIDE* kwa akina mama wa Mjini. Unakwenda pale *SELF*, watu wa Mijini. Sasa huku tunazungumzia kwamba wananchi walio wengi wako Vijijini, tunawasaidia vipi? Ndiyo maana nasema nadharia ni kubwa kwamba wananchi wa Vijijini wasaidiwe, lakini utendaji halisi wa kweli wanaofaidi matunda ya uhuru, matunda mengi ni sisi watu wa Mijini au watu wa Mijini zaidi kuliko na kila kitu. Kuna umeme, kuna *dance*, kuna mipira, kuna nini, yote watu wa Mjini. Sasa matokeo yake

ndiyo maana vijana wetu wanakimbia kule Vijijini angalau na wao waje wafaidi namna fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nisisitize tu moja nalo ni suala la usiri. Katika maelezo ambayo yametolewa hapa, moja ya kazi muhimu inayotakiwa kuzingatiwa na Watumishi wa Benki ni usiri. Usiri wa kutokuvujisha siri za mteja wao ama ni fedha kiasi gani na nini.

Lakini bayo ambalo linasemwa, sina hakika nalo, ushahidi sina lakini linasemwa, bora tuliseme. Kwamba katika hii habari ya ujambazi wako baadhi ya Watumishi wachache ambao siyo waaminifu wanadiriki kushirikiana kumwambia aah, aisee, leo Mr. X hapa kachukua Shilingi milioni tatu, Mr. Y kachukua Shilingi milioni nne. Watumishi wa Benki wanawaambia wale.

Kwa hiyo, wewe ukitoka nje unajiona kwamba uko *safe*, lakini tayari kumbe umeshachorwa. Unaambiwa kabisa kavaa kitenge, kavaa nini, kavaa ghasia gani. Kwa hiyo, ukitoka pale unaingia kwenye gari, wanakufuata wanakwenda kukumaliza. Ni kwa sababu hakuna usiri kwa baadhi ya Watumishi hata kama ni wachache katika Benki zetu hizi.

Naomba Benki Kuu kwa kweli ilifuatilie hili vizuri kuona kwamba Watumishi hawa wa Mabenki au uongozi unahakikisha kwamba kunakuwa na usiri wa kutosha ili kuepusha maisha ya watu, vinginevyo hata kwenda kuchukua pesa nyingi sasa itakuwa wasiwasi na matokeo yake ni kwamba tutaogopa kuweka fedha Benki, tutaanza kurudi tena katika utaratibu ule wa zamani ambao zinakaa kwenye godoro au zinakaa kwenye mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nisisitize suala ambalo wenzangu wamesema la Benki ya Nyumba na Benki ya Wakulima. Kwa kweli suala la kuwa na Benki ya Nyumba tena baada ya ile Benki ya Nyumba ya Kwanza mambo yake kuharibika, ni muhimu sana. Niiombe sana Serikali kwa kweli na kwa sababu hili limo na limezungumzwa hata kwenye Ilani ya Uchaguzi.

Basi niiombe sana Serikali walipe kipaumbele ili kusudi Benki hizi ambazo zimezungumzwa kwamba zitawasaidia wananchi mojawapo ikiwa Benki ya Nyumba, Benki ya Wakulima ambayo itawasaidia wakulima katika pembejeo, itawasaidia wafugaji kupata pesa za kununulia dawa na kadhalika. Zifunguliwe mapema iwezekanavyo ili kusudi kuepusha matatizo ambayo yanaweza yakatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kukushukuru, narudia kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri ambayo inafanya. Nina hakika sisi Wabunge na wananchi wote kwa ujumla tunaiunga mkono na tutaisaida ili kusudi itimize azma ambayo wamelenga kuitekeleza katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Nne. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii. Awali ya yote naunga mkono hoja hii na nasema kwamba Muswada huu kwa kweli umekuja wakati muafaka kwa kuwa nikiusoma, nikilinganisha na Muswada ambao umepita, kuna marekebisho makubwa sana na mimi kama Mwanasheria, Sheria iliopita ya nyuma ilikuwa inanipa shida. Sasa huu kwa kweli umekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, ninayo machache ya kuchangia. Kwanza kabisa, niwapongeze sana Watumishi wa Benki zetu ambao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana. Watumishi wengi wa Benki kusema kweli ni waaminifu. Ni kwa bahati mbaya anatokea mmoja tu, lakini mmoja asiharibu sifa ya Watumishi wengine. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ambalo nitalisema, pamoja na Muswada huu mzuri lakini vile vile Benki Kuu yetu iangalie maslahi ya Watumishi wa Benki. Maslahi ya watumishi yamekuwa hayaridhishi, ni madogo, mishahara yao ni midogo. Watumishi hawa wanatunza fedha nyingi sana tena kwa uaminifu.

Ninashauri kwamba ifike wakati hawa Watumishi tuache kuwatia kwenye majaribu. Uwepo utaratibu mzuri wa kuwakopesha mikopo yenyé masharti nafuu sana kazini kwao na vile vile hawa Watumishi waandalifi mishahara mizuri, ndipo tutaweza kuondokana na hii hali ya kutiliana mashaka na watu kuwatia kwenye vishawishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikisoma Muswada huu, nilipitia kifungu cha 6(1) kinazungumzia adhabu kwa mtu ambaye atafanya shughuli za kibenki bila kuwa na leseni. Hiki kipengele kwa kweli ni kizuri sana kwa sababu lazima tuwe na udhibiti wa vyombo vyetu vya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia adhabu hii inayotolewa, ni adhabu ambayo inaachiwa mwanya mkubwa sana kwa yule mtu ambaye atakuwa anasimamia haki, Hakimu au Jaji. Inasema kwamba: “Adhabu isizidi faini ya Shilingi milioni 20 au kifungo kisichozidi miaka mitano.” Mimi bado narudia kusema kwamba pamoja na Utawala Bora ambao tunauzungumza kila siku, lakini hawa Waheshimiwa Mahakimu au Majaji ni binadamu.

Utawala Bora bado haujaenea vizuri sana kwenye vyombo vyetu vya Mahakama. Kumwachia nafasi kubwa namna hii mtoa haki sio jambo zuri kwa sababu Sheria hairuhusu jambo fulani lifanyike na mambo fulani yasifanyike. Sasa ukimpa nafasi kwamba Mheshimiwa huyu anaweza kutozwa kiwango kisizidi milioni 20, basi unawenza kukuta mtu amefanya kosa lile lile na kubwa sana, huyu akatozwa Shilingi laki moja, huyu akatozwa Shilingi elfu hamsini, huyu akafungwa siku moja, mwagine labda miaka mitano.

Sasa mimi ninapendekeza kwamba tuwe na *minimum Sentence*, tuseme kwamba Sheria iwe wazi kwamba ni kifungo ambacho hakitapungua miaka mitano lakini

hakitazidi miaka 20, kwamba mtu akitiwa hatiani, basi *discretion* ya Mheshimiwa Hakimu au Jaji iwe kati ya hicho kipindi.

Vile vile, hata kwenye faini ionyeshe kabisa kwamba ni kati ya Shilingi milioni 10 hadi milioni 20. Inaweza kuwa Shilingi milioni 15, milioni 12. Lakini tusiache mwanya mpana namna hii wa kuiweza kuleteleza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *concern* yangu iko kwenye kipengele Namba 8(1)(c). Kwenye kipengele Namba 8(1)(c) inazungumzia kwamba *Chief Executive Officer* na Maofisa wengine ni kwamba wanawajibika kupeleka *documents* zao Benki Kuu ili Benki Kuu iweze kuwafanya tathmini (*Vetting*). Lakini Sheria inasema wapeleke majina pamoja na anuani.

Sasa mimi hapa nashangaa kwamba ukijua jina la mtu fulani na anuani yake, kweli inatosha huyu mtu kumfahamu vizuri. Ninaona hapa kuna mapungufu makubwa. Ili kumfahamu mtu ambaye ni mtendaji wote tunafahamu kwamba anatakiwa awe na *CV* iliyokamilika. Kwenye *CV* tunajua kabisa kwamba amesoma wapi, ana elimu gani, vyeti vyake aambatanishe ikiwezekana na picha zake na vile vile hata nakala za *Passport* tuweze kujua kama huyu ni raia wa Tanzania au ni mtu wa nchi gani. Kwa hiyo, napendekeza kwamba hapa taarifa hizi hazitatosha. Anuani na jina haitoshi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kipengele Namba 12(1)(b) inaeleza ni watu gani wasioruhusiwa kushika uongozi kwenye Benki. Kipengele Namba 12(1)(b) kinazungumzia watu gani ambao wanakatazwa kushika uongozi katika Benki. Sina matatizo na kipengele (a), lakini matatizo yangu yapo kwenye kipengele (b) na hasa mistari miwili ile ya mwisho.

Kipengele (b) kinasema kwamba: “Mtu hataruhusiwa kushika nafasi kwenye Benki kama aliwahi kuondolewa kwenye uongozi wa Benki na Benki Kuu.” Sasa, hii yenye tu haitoshi, kwa sababu kipengele (a) na (b) kinaeleza kabisa kwamba huyu mtu labda ataondolewa kama si mwaminifu, pengine amekuwa *judged bankrupt*.

Lakini hii tulioongeza hii inaleta mwanya mbaya sana watu kuwanyima haki ya kufanya kazi kwa sababu haielezi huyu mtu aliondolewa na Benki Kuu kwenye kazi za Benki kwa sababu zipi. Sababu tunayoijua ya msingi ni mtu kutokuwa mwaminifu, labda uwizi na masuala mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukiacha nafasi hii, kuna hatari ya Benki Kuu kuwa *Ma-dictator* na hii imeishajitokeza kidogo kwenye Benki yetu hii. Unakuta mtu alikuwa ni *Director* wa *Banking Supervision* wa Benki Kuu, anahoji ajira ya *Managing Director* wa Taasisi ya Fedha ya Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, akishahoji kwa kutumia kipengele kama hiki, anamuandikia barua kwamba hafai kukaa kwenye nafasi hiyo yaani kuwa *Managing Director* wa Benki hiyo. Wanamuondoa kwenye nafasi hiyo bila kueleza sababu ya

msingi ni ipi na muda si muda nafasi hiyo inatangazwa huyo huyo *Director* wa Benki, *Supervisor* wa Benki Kuu ndiyo anaomba hiyo kazi na anaajiriwa, anakalia hicho kitit.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba mfano ninao na ninaweza nikatoa mfano hai ni wapi imetokea. Kwa hiyo, ningeomba kabisa kipengele hiki kiondolewe kwa sababu kitanyanya watu wengi sana, kwa kuwa kinawapa madaraka watu waweze kunyanya viongozi wa kwenye mabenki mengine madogo. Mtu kama atakuwa ana tuhuma basi zithibitishwe ili aweze kuondolewa madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa sana ya mabenki ni kutoa mikopo, kupokea ripoti pamoja na kukopesha. Waingereza wanasema kwamba: “*A loan is recovered when it is made,*” kwamba, mkopo unarejeshwa tangu siku ile unapotengenezwa. Ukitengeneza mkopo leo hii utajua kabisa kwamba huu mkopo unarejesheka. Lakini ukitengeneza mkopo unaweza ukasema, huu kurudisha hapa ni majaaliwa. Mikopo mingi sana ya mabenki yetu imekuwa ni mikopo ambayo ukiangalia kwa haraka haraka ni kwamba haiwezi kurejesheka. Hailipiki kwa sababu usimamizi umekuwa ni mbovu, siyo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anakuwa *Credit Officer*, anaenda ku-survey security ya mtu anasema, huyu mtu anastahili kupewa milioni 150 au 200. Hata nyumba yenye we ukimuliza iko mtaa gani hajaiona! Sasa pamoja na mkopo huu na riba yake, tunategemea kabisa kwamba mkopo hauwezi kurejesheka hata kidogo. Kwa hiyo, naomba katika Muswada huu basi Benki Kuu ijikite kabisa kuangalia kwamba mikopo inarejesheka kwa urahisi hasa pale inapotengenezwa. Tusingubiri mkopo uharibike, hapo ndiyo inakuwa mkopo mchafu, tunaanza kupiga kelele kukimbilia mahakamani, tunaogopa *court injunctions*. Makosa tuyaa ngalie kuanzia kwenye benki zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa hapo hapo kwenye masuala ya mikopo, utakuta kwamba benki zetu zimeshindwa ku-*delegate*, kutoa mamlaka kwa matawi ya kule mikoani kushughulikia mikopo. Mimi ninatoka Wilaya ya Karagwe, utakuta pale Karagwe anakuja mfanyakia shara anaomba mkopo, anajaza fomu. Sababu ya kuomba mkopo anataka kufanya biashara ya kahawa au labda mahindi na hayo mahindi yana msimu wake labda miezi miwili au mitatu. Ana-process mkopo unatoka Karagwe unakuja mpaka Dar es Salaam. Mpaka uje kurudi tena Karagwe huo msimu wa mahindi ulishaisha siku nyingi sana na ameingia gharama ya kulipia zile fedha za michango na unakuta hana faida na huo mkopo. Ningeshauri Benki Kuu iweze kutoa mamlaka japo kwa kiwango fulani cha fedha ili matawi ya benki zetu hizi yaweze kutoa mikopo kwa haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nigosie suala la *commissions* ambazo benki zinatoza. Utakwenda benki moja au benki nyingine unataka u-credit akaunti ya mteja, mteja wa benki hiyo hiyo, lakini unaambiwa ni lazima ulipe *commission* labda ya shilingi kama elfu tano. Lakini ukienda benki nyingine hiyo *commission* haipo. Sasa nadhani hapa kwa sababu sisi Watanzania wote ni walalahoi, uwezo wetu ni mdogo, nashauri Benki Kuu iliangalie hili la kutozana *commission* maana zinakuwa nyingi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la *SACCOS*. Bila kuzikopesha *SACCOS* zetu tutakuwa hatuwezi kufaidi huduma za benki. *SACCOS* nyingi zinaomba mikopo kupitia kwenye benki, lakini wanaambiwa kwamba ni lazima wawe na *security*. Lakini ukiangalia kwenye *SACCOS* watu walioko kule ni akinamama ambao uwezo wao ni mdogo sana, pengine anaiza vitumbua, maandazi au vitenge. Sasa huyu *security* ataipata wapi? Atapata wapi nyumba ili awe na hati ya nyumba? Naomba *SACCOS* zetu zikopeshwe bila kuangalia *security*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalisema hilo kwa sababu *SACCOS* ndiyo uti wa mgongo. Bila kuwa na *SACCOS* benki zitabaki kuwa za watu wenye fedha nyingi sana na matajiri. Makabwela, akina *yakhe* tutabaki kuwa watazamaji na washangiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kurudia kwamba naunga mkono Muswada huu na nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofî*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie. Kwa mara ya kwanza leo nitachangia kwa kifupi kwa sababu Muswada wenyewe ni mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuunga mkono, tofauti na ilivyokuwa jana. Lakini nitaje mawili, matatu yanayogusa vifungu vya 4 hadi 5 na vifungu vya 31 hadi 35. Katika ukaguzi wa mabenki pamoja na taasisi nyingine zinazohusiana na vyombo vya kifedha kuhusiana na utendaji wao wa kazi pamoja na mambo mengine. Nadhani *BOT* ijitahidi sana iwe na wakaguzi ambao watakuwa na uelewa wa hali ya juu au unaolingana na wale watu ambao wanakwenda kuwakagua. Ninasema hivi kwa sababu kuna mahali fulani niliwahi kuona yule anayekaguliwa ana ujuzi na uwezo wa hali ya juu na vifaa vya hali ya juu kulikoni yule anayemkagua. Pia, yule anayekaguliwa ana elimu ya hali ya juu na vyombo vya kisasa na vya hali ya juu na teknolojia mpya, kulikoni mtu anayemkagua. Matokeo yake yule anayekagua ndiyo anafundishwa kwamba ingetakiwa ufanye moja, mbili, tatu. Tunakwenda wapi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetoka hapa Tanzania, siyo kwingine. Ndiyo maana nashauri hawa wataalam wa *BOT* kwa sababu wanafanya kazi za fedha zile zile na katika mabenki mengine na taasisi nyingine nao wanafanya kazi hizo hizo, lakini kama watakuwa wamebweteka mahali fulani wanaweza wakajikuta wanapokwenda kuwakagua wenzao wanakuta wenzao wako juu zaidi kuliko wao na kwa hiyo wataibiwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna muda ambao umewekwa kwa benki au taasisi katika kutoa taarifa au katika kutekeleza maagizo ambayo watakuwa wamepewa na Benki Kuu, imetajwa tu hivyo. Kwa kadri Benki Kuu itakavyokuwa imeona, nadhani ingekuwa ni vizuri kama ungetajwa muda ili hao wakaguzi wa benki watakapokwenda wajue kabisa kwamba katika muda tutakaopewa wa kurekebisha mambo hayo au maagizo tuliyopewa utakuwa ndani ya muda huu na siyo zaidi ya hapo na baada ya hapo wawe *penalized*. Hiyo itawabana, vinginevyo itakuwa ni ngumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo udanganyifu mwingi katika uwekaji wa mahesabu kwenye taasisi hizi za vyombo vya fedha upo mwingi kwa sababu binadamu ameumbwa katika asili ya kutaka apate. Kwa maana hiyo, mahesabu ya taasisi hasa za binafsi huwekwa mara mbili. Kwanza ni mahesabu ambayo ni bubu yaani yale ya udanganyifu na pili ni mahesabu ya kwao ambayo ni ya kweli. Kwa mfano, niliwhali kwenda mahali fulani nikataka kununua kitu fulani, hawakunifahamu. Wakaniambia kitu hiki unachotaka kununua ni shilingi 70,000/= bila *VAT*, lakini ukitaka na *VAT* ni shilingi 105,000=/. Nikawaambia nanunua pamoja na *VAT*, wakanishangaa. Wakanitazama wakasema: "Mmh, wewe ni mpelelezi!" Sasa na mimi nikawashangaa! Wewe umeniambia ukitaka kununua na *VAT* ni shilingi 105,000=/, bila *VAT* shilingi 70,000=/, mimi nakwambia nanunua pamoja na *VAT* unaniambia mpelelezi, maana yake nini? Wakasema: "Unakuja kutuchunguza, ondoka." Nikaondoka, sikununua. Ilikuwa ni kama wiki mbili zilizopita.

MBUNGE FULANI: Wapi?

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Dar es Salaam. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, inaonyesha wazi wazi kwamba hata kama kuna ukaguzi kwa mfano wa *TRA* kwenda kuwakagua watu, wateja wao watawaonyesha vitabu vya ajabu ajabu na vitabu vya fedha zao wameficha, ndiyo maana nashauri hata *BOT* wanapokwenda kukagua vyombo hivi wajue kutakuwa na mahesabu ya kweli ambayo ni yao na mahesabu ambayo ni ya kuidanganya *BOT*. Hapo panatakiwa wajuzi zaidi wa *BOT*, wakijua utendaji wa kazi wa mabenki unavyokwenda hawatadanganya. Wakiwa na watu ambao wanafanana na mimi hapa, watadanganya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo, kwa ujumla naomba wajaribu kutazama kwani riba ni kubwa mno na wala haijali uwezo wa nani anakopa. Mtu mwenye uwezo akikopa riba yake ni hiyo hiyo na hata yule ambaye hana uwezo, uwezo wake ni wa chini, naye riba yake ni hiyo hiyo. Nashauri watu wa chini na pengine wakulima mjaribu kuwapangia *special rate* ambayo wanaweza kulipa hiyo riba, ile ambayo ni ya chini, ili na wao waweze kuinuka isifanane na ile ya wale ambao tayari wana uwezo. Hapo ndipo tutakuwa tumejaribu kupunguza au pengine kuja kufuta umaskini ambao tunajaribu kuukazania kuuondoa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekaji fedha wengi katika mabenki, riba ambayo inatolewa licha ya kusema tu kwamba ni kubwa, lakini faida wanayoipata, wengi wanapata faida ndogo. Ndiyo maana unakuta watu wengi wana pesa zao katika majumba yao, hawana ule *morale* wa kwenda kuweka fedha benki kwa kujua kwamba anapoweka Benki, ile faida anayokuja kuipata mwishoni ni kidogo. Kuna haja gani ya kupeleka huko na kila siku kuhangaika kwenda kupanga foleni ndani ya benki kuchukua au kuweka?

Mheshimiwa Naibu spika, pengine hatapata matatizo hayo tu anapokwenda kuweka fedha zake benki, wakati mwingine majambazi wanaweza kumvamia akiwa ndani ya benki. Sasa jaribuni kurekebisha ili wawekaji wawe na *morale* wa kuweka. Jaribuni kutujengea yale mazingira ya kuwafanya watumishi, wakulima wa kawaida na

wafanyabiashara wa ngazi ya kawaida nao waweze kuona benki ndiyo mahali pekee panapofaa kutunza pesa kwa kuwawekea faida nzuri na hata mazingira mazuri hayo ya ulipaji wa riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wengine walivyochangia, ni vizuri hizi *SACCOS* muone ni jinsi gani mtakavyoweza kuwakopesha na pia kuangalia mazingira gani ili fedha hizo ziweze kutunzwa, maana wananchi wengi wameanza kuelewa umuhimu wa *SACCOS*, lakini pengine mtaji wao ni mdogo na bado wanapata matatizo katika kukopeshwa. Ninaomba benki zinazohusika kuitia Benki Kuu mjaribu kutuwekea mazingira ya kuweza kuwasaidia hawa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, leo ni mara yangu ya kwanza tangu nimeingia Bunge hili ndani ya miaka 10 iliyopita kuchangia kwa ufupi sana. Muswada ni mzuri, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia maneno mawili au matatu kuhusu Muswada huu ambaao ni mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na kuwa mwanamke wa kwanza kufanya hivyo katika nchi yetu. Pia, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wale wa zamani kwa kurudi hapa Bungeni na kuwakaribisha wapya kwa makofi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siwasahau wapigakura wangu huko Musoma Vijijini. Wao kwanza nawapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini pia kuwapa pole hasa wanaoshi pale *Buhemba Gold Mines* ambapo kila wakati kuna ugomvi mkubwa kati ya wawekezaji na wananchi wanaochimba dhahabu kidogo kidogo. Ningependa kuwaahidi na kuwa-assure wapigakura wangu kwamba nitafanya juhudzi zote kuhakikisha ari mpya, kasi mpya hii pamoja na nguvu mpya inaelekezwa pale ili kumaliza matatizo ya Buhemba, *once for all*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leo siyo kazi ya kuhusika na mambo ya madini, nadhani tushughulikie suala muhimu zaidi hili la *Bank and Financial Institution, Act*. Hii sheria niseme ni nzuri sana, ninaiunga mkono mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yale nitakayosema ni *technical* yaani mambo ya undani ndani, ya kisheria ambayo nadhani nimefanya *schedule of amendments* ili waweze kuyaangalia kwa makini kuona kama tunaweza kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo ningependa kuongelea ni kuhusu Muswada wenyewe kwa umbali wake. Sheria hii inasema itakwenda mpaka Zanzibar. Itatumika hapa na pia itatumika Zanzibar. Kwa kizungu inasema *it-extend to Zanzibar*. Inamaanisha nini? Zanzibar wana sheria yao ya makampuni, kama vile Kenya ama Uganda ina sheria zao za makampuni. Kwa hiyo, Zanzibar kimuundo wa kampuni ambayo itakuwa ni benki ni tofauti na muundo wa benki ambayo imeanzishwa chini ya Sheria ya Kampuni ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ninaloliona, hofu ninayoiona kwenye Muswada huu, ukiona kila *page* unazungumzia juu ya *Companies Ordinance Cap 212*. Sheria ambayo tumeifuta sisi Bungeni hapa mwaka 2002, tukatunga Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Nadhani pengine ni utata mdogo tu, lakini ni kioja! Huwezi kuwa na Benki ya Tanzania inayoundwa chini ya utaratibu wa *Companies Ordinance* au *Companies Act*, halafu hiyo hiyo benki nyininge inaundwa Zanzibar inakuwa ni Benki ya Zanzibar chini ya mfumo mwengine, halafu unasema: “Sheria ya hapa ndiyo itadhibiti sheria ya Zanzibar.” Sielewi maana yake ni nini! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nawasemea Wazanzibari, mimi siyo Mzanzibari lakini ni Mtanzania. Maana yake ni nini? Wewe umeanzisha kampuni yako Zanzibar na hiyo kampuni pengine inaitwa *Mkono Bank Limited Zanzibar*, chini ya mfumo wa *Companies Decree* ya Zanzibar, halafu ukapewa leseni na Benki Kuu. Siku Benki hiyo ikifilisika utatumia sheria gani? Utatumia sheria ya kwetu Bara ama ya Zanzibar? Muswada huu una utata huo, nadhani utatuletea matatizo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mwanzo kabisa tungoanisha hizi sheria mbili. Sioni ni kwa nini tuwe na Sheria ya Kampuni Zanzibar na Sheria ya Kampuni Tanzania, lakini Sheria ya Benki ni moja, sioni maana yake! Kuna tatizo gani? Huwezi kuanzisha benki bila kuwa na kampuni. Sheria ya Muflisi ya Makampuni ni moja, iko kwenye *Companies Act*, utaratibu mzuri kabisa. Ukiona Muswada huu unavyosema kwamba kama benki imefilisika basi achana na utaratibu huo wa kampuni, nenda kwa Muswada huu utapata jibu. Haiwezekani kabisa! Sheria ya *insolvency* ni ngumu sana, haiwezi kukarabatiwa ama kudhibitiwa na karatasi ama *page* tatu kama tunazoziona hapa. Sioni kwa nini ile Sheria ya *Company* isingewekwa hapa moja kwa moja, ile Sheria ya Kampuni ya Kufilisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo la maana ya *Banking Business*, biashara ya benki ni nini? Ninavyojuu mimi, biashara kuu ya benki ni kuchukua *deposit*, unachukua fedha *on deposit*. Kwa hiyo, mtu ye yote anayefanya hiyo biashara ya kuchukua fedha *on deposit* na akiambiwa nipe hela yangu iliyowekwa pale ni lazima hiyo benki imrudishie. Ukiona Muswada huu, nakuja sehemu ya kwanza, inatoa ufanuzi kuhusu biashara ya benki na ina-cover mpaka *Cooperative Society* mpaka vijijini.

Kwa hiyo, Sheria ya Muflisi ya Benki na Sheria ya Muflisi ya *Cooperative* yote imeoanishwa hapa. Wanasema hii ndiyo itadhibiti utaratibu wote wa kufilisi benki iliyo kubwa na benki iliyo ndogo. Lakini utaratibu huo hautajwi ni upi, utaundwa baadaye na madaraka hayo amepewa Gavana wa Benki afanye hivyo. Sasa hapa moja kwa moja unapingana na sheria kama tano. Moja ni sheria ya kwetu, moja ya Zanzibar, moja ya *cooperatives*, moja ya *banking* na moja ya *bankruptcy*. Zote zimebekwa kwenye kapu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, isingekuwa vizuri tukafanya utaratibu ili kuangalia upya? Muswada huu unaweza kwenda kama ulivyo, lakini baadaye tulete marekebisho Bungeni kuona ni vipi tunaweza kukarabati usituletee matatizo huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, sheria hii inazungumzia mambo ya *core-capital* na wametoa *definition*. Ninavyojua, hii *section three* ama ibara ya tatu ya Muswada huu ingeboreshwa zaidi kama tungesema *ordinary shares* ni sawa sawa na *common stock*, naona kuna *confusion* hapa. Unazungumza juu ya *ordinary shares*, hapo hapo wanasema ni *common stock*, hivyo vyote ni kitu hiki kimoja. Marekani ndio wanaita *common stock*, hapa tunaita *ordinary shares*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani lingekuwa ni jambo la busara kuangalia upya eneo hilo la *definition* ya *core-capital* na *banking business*. Lakini kwa kutaka kujua urefu na upana wa mabadiliko haya, nimeandaa *schedule of amendment* tutaiona kama tunaweza kuifanya kazi leo ama itapelekwa mbele kwa uchunguzi zaidi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kupoteza muda mrefu, isipokuwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyeleta Muswada huu kwa kazi nzuri aliyoifanya pamoja na maofisa wa Benki Kuu hususan Gavana wa Benki na kile kitengo cha *Bank Supervision* ambacho kimefanya kazi nzuri ya kuandaa Muswada huu ingawa una upungufu, lakini huko mbele nadhani tunaweza kuutengeneza ukawa mzuri sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na machache niliyosema, naunga mkono Muswada huu mkono mia kwa mia. (*Makofit*)

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza viongozi wetu wa juu, Mheshimiwa Rais, Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa kwa uongozi wao mzuri tangia walipoingia madarakani. Nina hakika utendaji wao mzuri umewaacha vinywa wazi hata wapinzani ambao walikuwa hawaamini kama kasi yao na *speed* yao itakuwa ya namna hiyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mwibara kwa kunichagua niwawakilishe katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile, kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu ambao unalenga kuimarishe Sekta ya Fedha na Uchumi kwa ujumla, ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuondoa umaskini uliokithiri katika jamii yetu. Nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, nimepata fursa ya kupitia Muswada huu kwa kina na kuufahamu barabara. Pale nilipotaka maelezo, Wizara ya Fedha na Benki Kuu walinipa maelezo ya kutosheleza na hivyo kuona

kwamba Muswada huu unatosheleza azma yetu ya kuimarisha Sekta ya Fedha na Uchumi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii vile vile kuwashukuru Gavana, Waziri wa Fedha na watendaji wao wakuu walioshiriki kuandaa Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni. Kwa hakika wamefanya kazi nzuri na hivyo wanastahili pongezi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unalenga pamoja na mambo mengine kupunguza gharama za ukopaji wa fedha katika hii Sekta ya Biashara yaani kupunguza gharama ya riba kwa sababu Sekta ya Fedha ikishaimarika ina maana kwamba inaondoa *risk* zilizomo katika uchumi wetu na hivyo kufanya riba kuwa ya chini.

Muswada huu vile vile unajenga mazingira mazuri ya kibiashara katika Sekta ya Fedha ili kushawishi ushiriki mkubwa wa mabenki kutoka nje na ndani na hivyo kuongeza ushindani mkubwa katika Sekta ya Fedha na hivyo kufanya gharama za ukopaji wa mikopo ama upatikanaji wa mikopo kuwa wa nafuu na mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Muswada huu utapunguza kwa kiasi kikubwa sana *risk* kubwa ambazo Mabenki mengi na wawekezaji kutoka ndani na nje wamekuwa wanaogopa kuingia katika sekta hii kwa sababu ya hizo *risk*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi Muswada huu unalenga kuyashughulikia yale yote tunayoona kwa sasa hivi kama ni kikwazo kikubwa cha kufanikisha uendelezaji wa sekta ya fedha na hasa upatikanaji wa fedha na mikopo ambayo inaweza kufika mpaka vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa upande wangu naunga mkono Muswada huu na nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, tuunge mkono Muswada huu ili tuweze kuimarisha uchumi na tuweze kuondoa umaskini ambao umekithiri katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa namna hiyo napenda kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. (*Makofii*)

MHE. ADAM K. A. MALIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutimiza siku 100 katika madaraka. Naomba nikubaliane na Mheshimiwa mwenzangu aliyesema jana kwamba nyota njema huonekana asubuhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kazi nzuri mno inayofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kiasi kikubwa inatokana na ushirikiano na umahiri na *supporting*

role nzuri ya msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitambue kazi nzuri sana na ya kujivunia ya viongozi wetu hawa wakuu wawili. Lakini pia niwapongeze Mawaziri na Manaibu wao na watendaji wakuu wa Serikali na Wizara. Lakini nitakuwa siwatendei haki ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ambao wanahakikisha Serikali haipati muda wa kusinzia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya kwanza kabisa ni mafanikio ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kama Rais na halafu pia ni mafanikio yetu sote na ishara kwamba mambo mazuri kwa Mtanzania yanawezekana kila mtu akitimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipata nafasi ya kuujadili Muswada huu katika ngazi ya Kamati ya Fedha na Uchumi na ninaweza nikaliambia Bunge lako kwamba Waziri wa Fedha na watu wake ni watu ambao ni mahiri sana na hivyo napenda nimpongeze yeye na Manaibu Mawaziri wake, Gavana, watendaji na wataalam wote wa Benki na wa Wizara ya Fedha waliowasilisha Muswada huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niseme yafuatayo, awali ya yote naomba niseme naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tunajadili Muswada wa *BOT* tulisema mionganoni mwa majukumu ya *BOT* ni kusimamia shughuli za kibenki na Taasisi za fedha. Tumeweka misingi ya Benki Kuu kusimamia shughuli za Taasisi hizo ili zifanye kazi kwa kuitikia sera ya Taifa ya fedha ambayo yenewe inaitikia misingi ya sera kuu ya uchumi ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama wawakilishi wa Watanzania wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba Benki Kuu na Taasisi inazozisimamia zinatekeleza majukumu yake katika namna ambayo malengo Makuu ya maendeleo ya uchumi wetu na uwezeshaji wa Mtanzania hauwatazami tu wale watu wachache labda akina Selelii na akina Chegeni, lakini pia iwatazame akina Jongo na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba mimi ni mchumi na ninapenda kukuhakikishia kwamba Tanzania yetu ina wataalam wachumi wengi sana ambao mimi nikijilinganisha nao, nakuwa kama kipanya tu kidogo anayetafuta kujificha, mapaka mabonge yakiingia. Tuna *professors*, tuna wataalam wakubwa sana wa uchumi. Maana yangu ni kwamba nataka kusema nini, Tanzania ina mipango mizuri, ina rasilimali nzuri, ina utawala wa kidemokrasia, ina uwajibikaji wa mfano kabisa wa wawakilishi wake wanaoteuliwa na wananchi na uwajibikaji wa wale wanaoteuliwa na Mamlaka. (Makofi)

Kwa hiyo, sasa wakati wa kujivunia mipango mizuri umekwisha na sasa mimi naomba nishauri Bunge lako kwamba tuwaombe wataalam na wachumi hawa mahiri mno

sasa watuelekeze kwenye utekelezaji wa msingi wa mipango hiyo. Mtazamo huu ambao ni *general overview* unalenga kunikisha wapi? Huu ni Muswada wa mfumo wa Mabenki na Taasisi za Fedha wa Tanzania (*The bank and financial system*) ya Tanzania. Kimsingi nchi zilizoendelea zimetegemea sana mchango wa mfumo huu katika maendeleo yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu na Taasisi za fedha huko nyuma ulichangia sana kuzorotesha maendeleo yetu kwa kuwakopesha wasiokopeshka kwa kushindwa kufuutilia madeni, kwa sera mbaya za *borrowing rate* na *interest rate* na pia kwa kuidhinisha fedha kwenye maeneo ambayo kimsingi ilikuwa hayana tija. Ukosefu wa hatua za kisheria na za kinidhamu ulipelekea kwamba mfumo huo wa Benki uliwatahirisha wachache na ukawaendeleza umaskini wengi katika Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba kusema ni kwamba watu wanajifunza kwa makosa yao. Nchi kubwa kama Japan tunavyofundishwa kwenye uchumi tunaambiwa kila siku kwamba Japan ni katika nchi ambazo *Banking system* yake ilipata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *Banking system* ya Japan leo inajivunia kwamba ina *contribution* kubwa ya Mabenki kutoka nje (*capital from outside*), lakini yenye we Japan ina mabenki yake na taasisi za kifedha kubwa ambazo zinazingatiwa kama mhimili wa uchumi wa Japan.

Maana yake ni kwamba kuna maeneo mengine ambayo huwezi kumwambia *Standard Chartered* aende lakini sheria inamruhusu kufanya kazi zake za kibenki ndani ya Tanzania. Kwa hiyo, tunachoomba ni kwamba sheria hii iangalie na Benki Kuu ifanye mkakati wa makusudi kabisa wa *ku-promote* maendeleo ya *Baking sector* ambayo yanamu-*involve* Mtanzania mwenyewe. Hatuwezi kuingia katika *Banking sector* ya mabilioni ya fedha, nina hakika tukimsikia Abdulkarim Shah ame-*invest* kwenye Mabenki yenye mabilioni ya mahela tutaanza kujiuliza. (*Makofî*)

Lakini Benki ambazo zinapenda kufanya shughuli zake kwa lengo la kupeleka maendeleo ya Mtanzania, yale ambayo sisi tulikwenda kwa wananchi kuwaomba kura na kuwashakishia ni Benki ambayo inamwezesha Mtanzania kuwa na mtaji mdogo wa kuuzungusha na kurudisha pesa za mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba Benki Kuu na Serikali izingatie kwamba mfumo huo wa Mabenki ndiyo unaopelekea kukidhi malengo ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabenki tuliyokuwa nayo ambayo yamezaliwa kutohaka na sheria hii ya *BAFIA* ambayo tunataka kuiondoa sasa ya mwaka 1991 imetuonyesha njia, zimetuonyesha namna Mabenki yanapokuwa *privatised* na *managed* vizuri yanachangia katika uchumi. Lakini bado kabisa sheria hizi kama zinalenga kuwanufaisha Watanzania wote basi mwendo bado mrefu. Hata hivyo ninaamini kabisa kwamba hii *Banking and Financial Institution Act (BAFIA)* ya mwaka 2006 inaweka

mazingira ya kufanikisha hayo kama wale wataalam niliowataja wenyе sifa kemkem wataacha kuridhika na Miswada na semina na kongamano na wataanza kuwa na tathimini za utekelezaji wa sera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mungu atanijalia uhai na Ubunge, mimi nitasimama hapa mbele yako tena ndani ya mwaka mmoja na nitaomba kuwa uliza maswali yafuatayo wataalam wa Benki Kuu. Bunge la Jamhuri ya Muungano limeridhia Muswada huu kwa kutambua kwamba vipengele *section No.5, section 24* inaielekeza Benki Kuu na zinaiwezesha kusimamia uanzishaji wa taasisi na huduma za kibenki ambazo zinawalenga Watanzania wa chini, swali langu nitakaporudi mbele yake litakuwa kwao, je, utekelezaji wa sheria hii umechangia kwa kiasi gani kwa maendeleo ya Mtanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za nadharia na maneno hazitoshi. Katika kuwakabidhi majukumu haya mazito Benki Kuu, pamoja na kuwarahisishia Mabenki na Taasisi za fedha, utekelezaji na uendeshaji wake pia tuwaombe watuletee taarifa za maendeleo zenye mahesabu ambayo ni *quantified* wanasema kwenye *economics* kwa maana kwamba waje watuambie kwamba sera zile zimechangia kwa upande wa pato la mwananchi wa kawaida wa chini limekua kwa kiasi fulani iwe *quantified* wasije wakatuambia tu kwamba Mabenki yamechangia kiasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wake tunaambiwa sheria imewezesha uchumi wa Tanzania kukua kwa kiasi kadhaa na miaka hii iliyopita kila inapota ripoti Benki tunaambiwa kwamba uchumi umekuwa sana *which is fine*. Lakini kama Mabenki yanaongeza *deposit* tuseme labda kutoka bilioni 25 hadi bilioni 100 hiyo *figure* inatuambia kwamba *fine* Mabenki yameongeza rasilimali au *whatever* lakini *what if depositors* wametoka 15,000 wamekwenda 15,200 hiyo inatuambia ni *depositors* wale wale ambao wameongeza uwezo wao. Sasa tunachotaka kutoka Mabenki haya ni kwamba pamoja na kukua kwa Mabenki na sisi tunawezesha uwezekano huo katika sheria hii basi tunapenda kama Wabunge kwamba iwe inaonekana pia katika maendeleo ya kiuchumi wa Watanzania walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kulisema hilo niseme kwamba sheria hizi ziwe zinakidhi pia maendeleo ya Kisekta. Ukiangalia Mabenki haya labda yanapenda kwenda kwenye sekta ambazo ni za hela ya chapu chapu lakini inahitaji uwekezaji na mikopo mikubwa ya Mabenki ielekee katika kilimo. Sasa mimi siwezi kuwaambia Mabenki wakopesha kwenye sekta ya kilimo lakini naomba Wizara ya Fedha na Benki Kuu ifanye mkakati wa makusudi kabisa na ifanye utafiti wa kina kujua nchi zingine zimeweza kufanya hivyo na sisi Tanzania tupitie njia gani ili wakulima waweze kunufaika na huduma za sekta ya Benki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kusema tu kwamba uzuri wa sheria kama nilivyosema siyo mijadala ya Bunge na makongamano. Uzuri wa sheria narudia uko kwenye utekelezaji wake unaoleta maendeleo ya kweli kwa wananchi wote. Kama tulivyoihakikishia *BOT* na Serikali kwamba Bunge lako litafutilia kwa makini utekelezaji wa majukumu makubwa tuliyowapa basi na kwa Muswada huu Bunge lako

pia liombe pia kupewa taarifa za kina za mchango wa sekta ya fedha na Taasisi zake kwa maendeleo ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kusema kwamba nina amini kabisa kwamba Muswada huu umekuja wa wakati, ni wa kitaalam na kwa kiuchumi, ni Muswada mzuri sana na unaendana na malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne. Lakini utekelezaji pia unataka wote tuutazame kwa macho mawili, mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. (*Makofit*)

NAIBU SPIKA: Kama nilivyosema wengi walikuwa hawajaingia, Muswada huu unamalizika kesho jioni kwa hiyo, watu wasije wakafikiri wamechelewa kuomba kwa hiyo, wanaweza kuendelea kuomba kuchangia. Halafu kama nilivyoeleza pia kwamba kesho kuna maonyesho tena kwenye viwanja vya Bunge ni maonyesho ya *NGOs* mbalimbali ambazo zinahusika sana na huduma za jamii na maendeleo katika Majimbo yetu. Kwa hiyo, kwa wakati wenu mnaweza kwenda kuona. Wanaanza asubuhi, wanafunga saa 11.00 jioni. Kama sasa wamefunga, kesho ndiyo siku yao ya mwisho. (*Makofit*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa na mimi nianze kama walivyoanza wenzangu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumaliza siku zake 100 za kwanza kwa mafanikio makubwa. Lakini pia nichukue hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa kasi kubwa aliyoionesha kwa siku 100 za kwanza na kwa kweli tuombe Mungu ziendelee. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Manaibu wake kwa kazi nzuri sana walifanya katika kuandaa Miswada hii miwili ule wa kwanza na wa leo kwa kweli imekuja kwa wakati muafaka na kwa kweli inakidhi haja zote za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Lakini kuna mambo ambayo naamini lazima wenzetu wa *BOT* wayaangalie kwa kina hasa itakapofika wakati wa utekelezaji wa sheria hii tuliyonayo hapa mbele yetu.

Ni kweli kabisa benki na Taasisi za fedha katika historia zinachangia sana katika uchumi na katika *political influence for a centuries* kwa miaka yote benki na taasisi za fedha ni za muhimu sana katika uchumi. Lakini kuna mambo ambayo ningeomba wenzetu wa *BOT* najua kazi kubwa walijonayo *BOT* ni *ku-maintain stable monetary system* lakini lazima wa *promote competitive banking system*, lakini kuna suala *consumer rights*. Najaribu kujiuliza kila siku hivi hawa wateja ni nani anawa-*protect* ningeomba *BOT* itusaidie kwamba nani anawa-*protect* analinda haki za *consumers*. (*Makofit*)

Lakini pia kuna mambo ambayo ningependa *BOT* wayaangalie kwa kina, duniani ukiangalia kuna *bank crisis* zinatokea kila kukicha. *Bank crisis* hizi zinasababishwa na *risk involve* katika biashara ya *bank*. Tunapoongea *risk* hapa utakwenda kwenye *liquidity*

risk, credit risk na interest rate risk. Sasa *BOT* wanafanyaje ili hizi *risk* zisiweze kuleta matatizo katika *banking system* katika nchi yetu. Ukienda katika historia *US saving and loan crisis* ya mwaka 1980's mpaka mwaka 1990's ililetu matatizo makubwa sana katika uchumi wa Marekani, *Japanese Banking crisis* ya 1990's kuna *bankrupt occurred* wakati *great depression* lakini pia hivi karibuni *recent liquidation by the Central Bank of Nigeria*, Mabenki 15 yaliyokuwa *liquidated*. Sasa mambo haya *BOT* isipoyaangalia yatakuwa ni hatari kubwa kwa uchumi wetu wa Tanzania.

Kwa hiyo, lazima Benki iangalie tena suala la *level* ya *interest rate* na *Central Bank Action* katika kuleta haya mambo yasitokee. Sasa ndiyo kazi ya *Central Bank*.

Lakini pia ukiangalia ibara ya 16 mpaka ya 24 wamepandisha mtaji kutoka biliioni moja kwenda biliioni tano. Kwa kweli hili mimi nimelipongeza sana. Lakini kama ushauri ningeomba *BOT* iangalie uwezekano wa kuzifanya Benki wawe na *Deposit insurance* ili ikitokea Benki *ime-fail* wale *depositors* wasipate hasara, *insurance* ndiyo iweze kulipa. Hili naona la muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Lakini pia ninaamini hakuna Serikali yoyote ambayo ingependa *bank system* yake ina *fell*. Sasa kwa sababu hakuna Serikali ambayo ingeweza kuona *bank system* ina *fell* ni vizuri sasa watu wa *BOT* ni wakati wa kuitekeleza hii sheria wawe makini sana wanawenza kusababisha Benki kufeli. Lakini pia tuangalia *perception* ya watu kwenye Mabenki yetu, watu wengi wanaangalia Mabenki kama yako kwa ajili ya kutafuta faida tu hayako kwa ajili ya kuendeleza nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnakumbuka huko nyuma kabisa Marekani wakati wa Rais Andrew Jackson suala la *bank* ilikuwa ni *issue* ya kampeni kwamba hata ye ye Rais wakati ule alikuwa anaona Mabenki kazi yao ni kuhangaika na faida tu hayahangaiki na kuendeleza watu. So ikawa *issue* ya kampeni.

Kwa hiyo, ningependa sasa na sisi siku moja katika historia tukaanza *issue* ya kampeni ikawa ni *performance* haitatusaidia. Kwa hiyo, lazima *BOT* tumewapa kila walichokihitaji kwenye sheria ya *BOT* lakini pia Muswada huu tuliwapa nguvu kubwa kusimamia Mabenki haya na Taasisi za fedha ili ziweze kufanya vizuri ili uchumi wetu uweze kukua.

Lakini kuna mambo ambayo ninaamini kwa kweli hizo *banks by definition* ya *bank* pamoa na *Financial Institution* hizi *formal one* kwa kweli haziko kwa ajili ya watu maskini, usitengee *Barclays Banks* wataenda Kasulu *no way*, hata kama tumewapa leseni, usitegemee *Standard Chartered* watakwenda Nkasi haiwezekani, haitatokea. Sasa lazima Benki Kuu ifanye jambo moja. Jambo moja la kufanya lazima tuanzishe *very strong Macro finances. Macro Finances* ndiyo zitakazowaokoa watu wa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Benki Kuu itusaidie sana. Kwa kweli hili suala la *Macro Finances* tulipe kipaumbele kuanzia kwenye *ku-train* watu ambao watalielewa jambo vizuri ya *Macro Finances* ili kweli wataalam hawa waje wasaidie nchi hii kuinua watu wa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kama tutaanzisha *Macro Finances* nina hakika tutaweza kuwasaidia wakulima wetu, tutaweza kuwasaidia wale wavuvi wangu wa Kibirizi wataweza kusaidiwa kama tutaanzisha *Macro Finances*. Lakini tusipoanzisha *Macro Finances* mimi sioni ni Benki gani, Benki ziko pale ni kwa ajili ya matajiri jamani. *Middle class* na kwenda juu ndiyo wenye fedha kwenye Mabenki haya. Mtu maskini sioni kama atawenza ku-meet vigezo vya kupewa mikopo na Mabenki haya makubwa.

Kwa hiyo, ningeomba sheria hii imekuja ni nzuri sana inakidhi haja na kwa kweli hii sheria ni mkombozi. Lakini niombe *BOT* itusaidie sana ili Mabenki yetu yaweze kuwa na kazi siyo kutafuta faida pia yafanye kazi ya kuhakikisha uchumi wa nchi unakua lakini pia na wale maskini tuwatafutia utaratibu ili nao waweze kufaidi hizi Taasisi na Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi naungana na wenzangu na naunga mkono hoja hii. Imekuja kwa wakati, ninaamini itatuokoa kutoka hapa tulipo sasa. Naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. PHARES K. KABUYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuzungumza machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maneno mengi huwa nashindwa kuelewa, waswahili wanasema ada ya mja ni kunena, lakini muungwana ni vitendo. Nadhani ukiona mtu anasema maneno mengi ambayo kazi yake ni kuunda misamiati huyo mtu ana matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu sasa hivi imepania kuondoa umaskini lakini najiuliza maskini wenyewe wanaeleweka? Mimi maskini nawaweka katika madaraja yafuatayo, kuna maskini hohehahe, kuna maskini sana na kuna maskini wa kawaida, maskini hohehahe ukitoka hapa nje tu unakumbana nao nao ni *beggars*. Mbona hatuanzi na hawa? Ni maskini gani tunaotaka kuwaondolea balaa ya umaskini, unaacha maskini omboombao mlangoni unakwenda kuondoa umaskini kwa watu wa Kagera hii kweli utawenza wewe? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuenze na hawa wa milangoni wako maskini amba wanauzu kuni na kubeba magunia ya mkaa hawa ndiyo tunaotaka kuanza nao, je, tuna mipango gani na hawa maskini? Halafu wako maskini wanaolima kwa jembe la mkono, hawa ndiyo mimi ninaoangalia kwamba tunganeza na hawa.

Halafu mimi nisingemsifu Waziri Mkuu na wala nisingemsifa Mheshimiwa Rais, nataka hawa waniambie bwana Rais wetu amefanya kazi na Waziri Mkuu wetu amefanya kazi. Yesu wanamwambia wewe ndiyo mtukufu anaseme wewe wanena, wacha watendewa waseme sisi humu tukisifusifu tumeukata angalau. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Mabenki hakuna Benki ya maskini duniani. Maskini hawajaanzisha Benki, Mabenki ni ya matajiri. Kazi ya Benki ni kukusanya fedha za matajiri na kuzilinda na lazima kuwepo na masharti kwamba wewe unayekopeshwa

uhakikishe fedha hiyo utairudisha na uwe na *mortgage*, huweki kitu huwezi kurudisha kitu kiende, ukifa kitu kiende. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa huyu *beggar* unataka aende Benki, ni Benki gani ya *beggar*? Watu wa Benki mtawapa kazi ngumu. Hizi hela ni za akina Kabuye na wenzake si hela za kugawagawa tu, lazima watu watimize masharti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo huko viongozi wetu walipata shida kwenye Vyama vya Ushirika. Wanakuja ooh, bwana vyama vya ushirika, Waziri Mkuu amesema kopesha wapeni mabilioni, vyama vimekufa na Mabenki yamekufa. Kwa hiyo, mimi nafikiri hawa kitakachowaondolea umaskini si Mabenki, Mabenki ni ya walionacho. Utapendezwa kweli fedha yako unataka kuagiza magari Dubai uambiwe kwamba Benki imefilisika kwa sababu wamekopesha maskini hivi mtaelewana na Meneja? (*Makofi/Kicheko*)

Sasa la kufanya Serikali yetu inao mzigo wa kuwafanya hawa maskini wakopesheke. Lazima kwanza tuwfanye wakopesheke, tufanye kazi kiuchumi bwana, tumesoma *economy*, Benki gani ya maskini anakwenda anazoa fedha bila hata *mortgage*, bila chochote hiyo itakuwa ni Benki sijui! Tuwfanye kwanza wakopesheke na njia za kuwafanya kukopesheka zipo, tuna maskini Wafanyakazi wa kima cha chini waajiri wao wawe ndiyo wa kuwasimamia hawa. Lakini leo kuna mahali pengine walimu wanalia hawajapata mkopo hata wa kujenga nyumba, wafanyakazi wengi wanalia waajiri wao wapo ambao ndiyo wa kuwafanya wakopesheke ndiyo wa kuweka mgongo kwamba kopesheni watumishi wangu. Lakini hii ya blaa blaa tutasifiana hapa bado nchi itaendelea hivyo hivyo. Wakulima kuna mahali pengine ambapo mashamba yana thamani kama kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, toweni hati watu wamiliki hayo mashamba, hizo hati waweze kuziweka kule ili waweze kupata mkopo, ndiyo kuwaweza wakopesheke. Nasema hivyo kwa sababu mashamba ya watu wengine hayana thamani. Sasa hao leo wamehamia hapa shamba likichoka yuko huko. Sasa kama benki inasema inakukopesha, umemkopesha yuko hapa ni Msukuma, kesho anapeleka ng'ombe Mbarali atampata wapi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tufanye wakopesheke, tuwape kilimo cha kuaminika, umwagilaji watu wa benki wajue kwamba kweli huyu amepanda mazao yataiva. Unakopesha mtu wa mazao, kesho yanakauka. Leo hii waliokopa, hivi benki watafanyaje kama kweli wamekopesha wakulima. Lazima tuwe na mtindo wa kuhawakikishia wakulima kwamba wanapolima wanavuna. Nchi haiwezi kuwa na mabwawa? Mbona mkoloni alichimba mabwawa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaaminishe wawe na kazi ya kuzalisha siyo bahati nasibu. Huyu Mungu wetu wa Afrika tunampa kazi kubwa. Mazao ya wananchi yapate bei, mtu kama ana kahawa zake anajua kweli zimepamba, hata Meneja wa Benki akija akaona anasema kweli wewe unaweza ukakopeshwa na anajua bei ipo. Lazima atamkopeshwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mazao haya bei watakuambia bwana duniani bei imekufa. Lakini ukienda Uganda, namshukuru sana Mheshimiwa Spika, aliniteua kuandamana Rais katika ziara ya Mtukufu Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waganda walikuwa wamesema lete kahawa kwa bei nzuri hawa Waganda wana soko gani la dunia? Lazima tuhangakie watu wetu. Mimi nataka maendeleo bwana hata kama yanaletwa na bepari. Mimi kuuza kahawa Uganda nini, ni pesa, kwani wewe unayemng'ang'aniza hapa umenilimia, umenipa jembe. Wewe unapomkata mshahara, wewe saidia sijui nchi ipate ushuru, wewe unapopata mshahara mbona hujahurumia nchi. Mkulima ndiye unamng'ang'aniza shilingi 2/= wakati kuna hela anayetaka aende achukue. Mnasema lete kahawa. Lakini hapa kahawa haina bei hawa wanaauza wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu tuwatafutie bei ya mazao wawze kustahili kukopeshwa, tuwasaidie namna hiyo. Vyama vyao vya ushirika tuviimarishe. Vyama vilivyokufa kama watu walikula hela ya wakulima wafuatiliwe waadhibiwe na kama vyama vimefilisika kwa njia ya *transaction* ya kawaida basi hivyo vyama visafishwe na Serikali ili viweze kwenda hivyo ndivyo vilikuwa vinakopesha wakulima, mbolea, madawa, sasa vimekufa. Wewe unasema mabenki yakopeshe hawa walalahoi. Benki ni ya mlalahoi ndugu yangu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuchosha, lakini naomba niseme kwamba benki zetu nazo ziwe tayari kukopesha wale wanaokopesheka bila mizengwe. Nao wana matatizo ya hapa na pale, urasimu ni mwangi sana utafikiri pesa wanazingojea zitoke mbinguni. Pesa ziko hapa lakini unakwenda, unakwenda, unakwenda mpaka unachoka. Halafu kuna rushwa. Siyo wote kama walivyosema, lakini wapo. Watu wengi wanashindwa kulipa mikopo, wanaambiwa bwana tutakupa laki sita. Lakini mbili ni zetu. Umekopa laki sita lakini wewe utsalipa laki sita, wakati umetoka na unne. Hiyo nayo ni matatizo, rushwa imo si wote lakini imo. Kuna mmoja alikopa laki sita, akaambiwa mbili zetu, sawa akapeleka laki nne. Wakati wa kulipa akalipa laki nne, hizi nyingine akasema lipeni na ninyi wa Benki si ndiyo mlikula. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikawa kasheshe, kwa hiyo, tunaomba na ninyi muwe safi kabisa. Kwa kweli mtu mtoa rushwa mtu wa benki hawezi kuwa na njaa jamani. Ndiyo maana angalau ninyi kamshahara ni kazuri kidogo, siyo kama mwalimu, ili msiwe na mambo ya kuchafua chafua benki. Kwa hiyo, hiyo nayo inatakiwa na riba. Riba ni kubwa, kwa kweli riba ni kubwa angalieni msiwe na uchu wa kutajirika haraka haraka. Punguzeni riba. Halafu na ile *interest* mnazowapa. Wewe unataka riba kubwa lakini aliywewka amana unampa *interest* kidogo maana yake nini. Nani atalaeta hela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu tulikuwa na *fixed account* unasema nita-fix kwa miezi sita niwe nakula hiyo *interest* hela yangu ibaki. Lakini *interest* ya shilingi 2/= nani atakupa hela yake milioni 5 kuja kupata laki mbili. Kwa hiyo, lazima muwe na vivutio vya kuweza kusaidia watu wavutiwe. Hii miezi mingapi hatujapata magari, kama kungelikuwa na *interest* ya shilingi fulani mtu unaweka kule tumilioni twako unanunua gari na kengine kanabaki. Lakini shilingi 2/= nani atakubali. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, lazima mfanye kazi kama watu wa benki msaidie, mvute watu waweze kuja. Kwa hiyo, narudia kufanya *summary* kwamba kwanza tuwafahamu hao maskini tunaotaka kuwaondolea umaskini ni nani na wako wapi. Tujue ni jinsi gani tunawenza tukawasaidia. Lazima wakati mwingine tutumie ukali. Hawa maskini kuna wengine hawajui kama ni maskini na kuna wengine hawajui kama wakiendelea kuwa maskini watakufa, hawajui. Ni sawa na mtoto mdogo amekamatwa mepigwa na malaria, yeye kumpa kidonge lazima umlazimishe ushike na pua ili ameze. Ukitsema kwamba umeacha kumeza dawa nitakuacha ufe. Huyo hajui kufa huyo. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, lazima wakulima wetu tuwe na mipango na mikakati Serikali ipo, wewe unashinda unazurura, unazurura katika nchi ya nani. Huku watu wanashinda na bao, bao kila siku. Unakula wapi, unalala wapi. Lazima tuwe na mipango ya kusaidia nchi hii. Halafu tufahamu watu wetu. Mimi niko hapa nina watoto 7 kila mtoto anayemaliza shule nenda kalime, unalima wapi, mimi nina hekta tatu atalima wapi. Wajukuu zangu wakimaliza shule nenda kalime, wanalima wapi, lazima Serikali iwe na mipango. Hao wanaothamani wakulima wanalima wapi? Nenda mkalime, Mhaya ana hekta moja, watoto 10 nenda mkalime wapi. Matokeo yake wanakwenda kuzurura. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana itajaa, lazima tuwe na mipango. Tufanye mambo ya kisayansi. Wakati mwingine tunajifanyia vitu vya hovyo hovyo tu mimi nawaambieni. Haya sitaki kusema mambo ya ulinzi lakini wengine majambazi tunawatengeneza wenyewe. Tunatengeneza mgambo dunia nzima wanajua kushika bunduki. Hujui wanamgambo wanaishi wapi, wanafanya nini, sasa wakichukua benki ooh, wametupiga. Wewe umewafundisha, hujui wanakaa wapi. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa tunakazana watoto wamalize *Form Four* huna mpango nao. Hivi mimi nitamaliza *Form Four* niende kijijini tu kuozea kule na wewe ule, ukae kwenye mataa. Mimi ninywe maji yenye hatari. Ooh, msije mjini, nani atakudanganya. Wewe ndiyo ukae kwenye maji mazuri, mataa, mimi Kabuye nikae huko porini. Tutabana hapa hapa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga hoja mkono. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabuye, umekaribisha watu wote waliokuwa nje, wamerudi ndani ya ukumbi. (*Makofi/ Kicheko*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada ambao umewasilishwa mbele yetu. Napenda nimpongeze Waziri wa Fedha pamoja na wale wote ambao wamemsaidia katika kuufikisha Muswada huu mbele yetu ili tuweze kuujadili. Muswada ni mzuri ni Muswada ambao una makusudio ya kuweka utaratibu na usimamizi wa mabenki na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata hofu sana wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha akihitimisha hoja juu ya Muswada uliokuwa umewasilishwa wa Benki Kuu. Alielekeza ni namna gani au aliwatoa hofu Wabunge waliokuwa na wasi wasi juu ya kutetereka kwa sarafu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwatoa hofu Wabunge kwa kuwaambia kwamba ni lazima tuzalishé zaidi ili kuifanya fedha yetu iweze kuwa na nguvu. Lakini hofu niliyonayo ni kwamba fedha itaimarika vipi wakati hatuwekezi katika uzalishaji. Tumekuwa mara nyingi tunaelekeza nguvu zetu na fedha chache tulizokuwa nayo katika vitu ambavyo haviwezi kusaidia kuongeza uzalishaji. Nadhani sasa hivi ipo haja kubwa sana tukabadiishi mwelekeo tukaenda kuwekeza katika kilimo ambacho kitasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na hasa kama tutatilia mkazo katika mazao ya biashara ambayo tutaweza kuuza nje na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumza kuhusu mikopo, nami sitapenda kutofautiana nao. Najua umuhimu na haja ya kupata mikopo ili kuweza kuongeza tija. Lakini ili tuweze kupata mikopo ni lazima kuwepo na kile ambacho tunaenda kukopa. Kwa ujumla tabia zetu kama Watanzania kwa ujumla wetu hatuna tabia ya kuweka akiba. Sasa ni lazima kwanza tubadilishi tabia zetu za kujiwekea akiba ili kiwepo hicho ambacho tutaenda kukopa. Vinginevyo kutakuwa hakuna kitu cha kwenda kukopa. Mabenki haya yanajiendesha ni pamoja na kuweka akiba zetu katika mabenki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia sasa hivi mabenki tuliyokuwa nayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa ni mabenki ambayo yanatoa huduma kwa wafanyabiashara wakubwa. Wafanyabiashara wakubwa wakubwa ndiyo wanaonufaika na mikopo inayotolewa na mabenki yetu. Ipo haja sasa hivi ya mabenki haya yakabadilishi mwelekeo na yakaweza kusaidia makundi mengine na yenye yake weza kunufaika na huduma zinazotolewa na mabenki na taasisi za fedha. Pamoja na hatua nzuri ambazo sasa hivi zimeshaanza kuchukuliwa. Lakini zimeelekezwa katika makundi ya wachuuzi peke yao. Mikopo inayotolewa sasa hivi haikidhi na wala haitoshelezi na wala haitaleta mabadiliko na kuwaleta maendeleo hawa wanaokopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo imewalenga wafanyabiashara wadogo wadogo. Mikopo inayotolewa haikidhi na wala haitoshelezi. Leo mtu anakopa shilingi laki tano. Shilingi laki tano siyo mtaji wa kufanya biashara katika nchi hii kwa sasa na kwa thamani na bei ya vitu kama tunavyofahamu. Kibaya zaidi huyo anayekopa shilingi laki tano, anapewa muda mfupi sana wa kurejesha fedha hizo. Kwa maana nyingine mfanyabiashara mdogo huyu, kijana ambaye anataka kujikwamua anakuwa muda wake wote anazunguka, anahangaika, anaifanya kazi benki badala ya kujiletea yeye mwenyewe maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna mpango wa kutolewa mikopo hiyo midogo midogo ya shilingi laki tano na kuendelea. Lakini marejesho yake ni baada ya siku 30. Lakini ukija kutazama yale marejesho na fedha waliochukua ni kwamba kijana huyu kwa muda wa miezi 6 alikuwa akiifanya kazi benki na siyo kwa sababu ya kujiletea yeye mwenyewe maendeleo na pengine inafikia mahala kwamba na mkopo

wenyewe anashindwa kuulipa. Nafikiri ipo haja sasa hivi mabenki yetu yakatazama upya ni namna gani wanaweza kuwasaidia hawa wafanya biashara wadogo wadogo ambao wamewalenga sasa hivi. Siyo wadogo wadogo peke yake yao pia wawatazame wafanya biashara wa kati.

Lakini pamoja na kutazama makundi haya ya wafanyabiashara peke yake hatutaweza kwenda mbali kama hatutawaangalia wakulima wetu. Ipo haja ya makusudi kabisa ya kuangalia ni namna gani tutawasaidia wakulima wetu waweze kusaliza ili tuweze kuongeza Pato la Taifa. Ni eneo pekee na kila siku tumekuwa tukiimba kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo nchi hii. Sote tunaamini kwamba nchi yetu ni nchi ya kilimo na siyo nchi ya viwanda pamoja na kwamba bado tunaendelea kuwekeza katika viwanda ambapo havisaidii na tumetelekeza kabisa kilimo. Ipo haja ya makusudi kabisa sasa hivi kuangalia ni namna gani tutaweza kuisimamia sekta hii ya kilimo ili kweli ilete maana ambayo tumekuwa tukiizungumzia kila siku kwamba ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kwanza tuwasaidie wakulima wetu kujua mahitaji yao na namna gani tunaweza kuwasaidia. Leo mkulima bado anaendelea na kulima kilimo kile kile cha miaka 70 iliyopita na wala hakijabadilika kwa sababu hawezi kupata msaada wa kuweza kubadili hali yake ya kilimo. Mkulima wetu wa kawaida leo hawezi hata kukopa trekta ya mkono. Trekta ambayo haifiki hata shilingi milioni 4, lakini kwa mkulima wa kawaida achilia mbali huyu ambaye analima mazao ya chakula. Nichukulie mfano mkulima wa tumbaku ambaye pato lake kwa kawaida huwa ni kubwa lakini bado hana uwezo wa kununua au kukopa trekta ya mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea na kilimo ambacho wote tunafahamu hakitaleta mabadiliko wala hatutasukuma maendeleo ya nchi hii. Ni lazima tutazame upya suala zima la kilimo na namna gani mabenki yetu yatasaidia katika kukisukuma kilimo ili kiweze kuwa na tija na kutuletea faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za mabenki ni huduma ambazo sasa hivi zinapatikanika mijini. Hata watu wetu watakapokuwa tayari kuweka akiba zao na fedha zao waliyokuwa nayo hawajui ni mahala gani wazipeleke fedha zao. Huduma za mabenki zimekuwa ni adimu sana zinapatikana katika miji tu na pengine zinaishia katika makao makuu ya Wilaya. Ni lazima tutazame ni namna gani tunaweza tukawaafikia watu wetu kule vijijini ili waweze kuziweka akiba zao katika benki ziweze kusaidia mzunguko wa fedha na kuweza kuleta tija badala ya kuendelea kufukiwa ndani ya mashimo na kuwekwa ndani ya vibuyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda nami niungane na ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Missanga katika pendekezo lake kwamba ipo haja ya kutazama upya tena kama tulishindwa kwa nini tulishindwa. Lakini haja ya kurudisha *Mobile Bank*, ni lazima sana katika nchi yetu. Pamoja na hili wimbi la ujambazi wa sasa hivi kitu ambacho mimi binafsi naamini kabisa siyo tishio. Tutaweza kulidhibiti. Ni lazima tuangalie kwamba tunafikisha huduma za kibenki kwa watu wetu wote mahala walipo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewapunguzia usumbufu wananchi wa kufuata huduma za mabenki mbali na pia kuwaondolea ile hatari *risk* ya kubeba kiwango kikubwa cha

fedha ama kwenda benki ama kutoka benki. Ni lazima tuhakikishe kwamba huduma za benki zimesambaa na zimewafikia watu wetu wote.

Mimi naamini na ipo haja kabisa ya kuziimrisha benki zetu za ndani ambazo kwa sasa hivi zimejithidi kusambaza mitandao yao na kufika sehemu nyingi za nchi hii na wala tusiweke mategemeo yetu na matumaini kwa mabenki yanayotoka nje. Tumeisha jifunza ni namna mabenki yetu ya ndani yalivyoweza kusambaza huduma zake katika nchi hii tofauti na mabenki yenyenye majina makubwa yaliyotoka nje ambayo yamejikita katika miji mikubwa.

Kwa mfano, *Standard Chartered* wako katika miji michache sana katika nchi hii. Lakini unapozungumzia *NMB* imefika kila mahali. Ni vema sasa tukaangalia kwa makusudi kabisa kuziimrisha benki hizi za ndani ambazo zinaweza kufika kila mahala ili ziweze kusaidiana na kuziimrisha *community Banks* na *SACCOS* zetu ambazo zitatoa huduma kwa watu wetu katika maeneo yote ya nchi hii. Kwa kufanya hivyo, ninaamini kabisa kwamba kwa kupitia mabenki tunaweza kutoa chachu ya maendeleo ya nchi yuetu.

Baada ya kusema hayo Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hofu moja tu ambayo nitapenda niondolewe masharti mashaka kama nitakuwa sahihi au siyo sahihi. Nimepata kusikia kwamba unapotaka mikopo ya fedha za kigeni (*dollars*) riba yake ni ya chini mno. Wanasema kwamba ni wastani wa asilimia 6 hivi riba yake. Lakini unapotaka mkopo wa fedha za Kitanzania riba yake inakaribia au inazidi asilimia 16. Tofauti hii kama kweli ipo ni dhahiri kwamba wanaonufaika ni wale ambao wanahitaji fedha za kigeni na pengine hizo fedha zinazochukuliwa hazirudi nchini na mikopo hiyo inalipwa kwa fedha za ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakopa, wanapewa fedha za kigeni kwa riba ndogo na Mtanzania anayetaka mkopo kwa fedha za Kitanzania kwa ajili ya kuleta maendeleo ndani ya nchi yake anatozwa riba kubwa. Kama hili ni kweli nitapenda na nitaishauri Benki Kuu ijaribu kuliangalia suala hili na kuweza kurekebisha dosari. Sasa hivi mtazamo na mwelekeo uwe ni wa kumsaidia Mtanzania kwanza. Baada ya kusema hivyo, napenda kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi nami nichangie Muswada huu uliyo mbele yetu ambao unaitwa *The Banking and Financial Institutions Act of the 2006*. Muswada huu umezungumziwa na walionitangulia na wote wameunga hoja mkono na mimi naunga mkono Muswada huu. Haya tunayoyasema ni ya nyongeza na ya usafanuzi ili Muswada huu utakapokuwa umepita, Muswada usaidie kusukuma maendeleo ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya dunia ya leo yanategemea uwezo wa kupata mtaji na uwezo wa kutumia *information technolegy*. Vitu hivyo viwili ndiyo vinatutofauti kati ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea na sisi katika mambo haya mawili bado tuko nyuma sana ya kwamba ni watu wachache ambao wana fursa ya

kufikia vyombo veya fedha wanavyoweza kuvitumia katika kutatua matatizo yao binafsi au hata katika kuhakikisha ya kwamba wanapanua shughuli zao ili kuweza kuajiri ama kujenga ajira kwa watu wengine.

Kwa hiyo, ni matumini yangu ya kwamba huu Muswada unatuwekea mazingira ambayo yatahakikisha kwamba watu wengi wanafikiwa na huduma hizi. Kwa maana hiyo basi, ni vema kama alivyosema Mheshimiwa Adam Malima, ifike mahali tuandalie ni taasisi ngazi za fedha na benki zipi zipi zimeanzishwa na zinahudumia watu wa aina gani. Upo uzoefu tunaouona ya kwamba ukiangalia idadi kubwa ya vyombo veya pesa viro miji mikuu na hasa Dar es Salaam.

Kwa hiyo, mimi nataka nipendekeze tangu mwanzo, nimeunga mkono nikiwa na matumaini ya kwamba benki hizi na taasisi hizi hazitawahudumia tu wale walioko Dar es Salaam kwa sababu inakuwa vigumu wananchi wa Tandahimba, wananchi wa Ukerewe, wananchi wa Mafia, wananchi wa Namtumbo na wote kufikia benki hizi kupitia Dar es Salaam. Ndiyo maana imekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wetu kuweza kutafuta mitaji wao wenyewe. Badala yake wamekuwa wakihangaika kuwakimbilia Wabunge wao na unakuta na Mbunge naye anagawa mpaka anafika mahali hana chochote. Kumbe badala ya kuwasukuma kwenye taasisi ambazo kweli wangepata mitaji mikubwa na kuondokana na umaskini. Tunabaki kuzungushiana umaskini na kulalamikiana.

Kwa hiyo, mimi ningependa kwa kweli bennki hizi na taasisi hizi zielekezwe katika maeneo yote ya nchi hii na maeneo ambayo yanaweza yakaleta maendeleo kwa haraka zaidi hayako mijini. Mijini mara nyingi ni utumiaji. Lakini uzalishaji mkubwa uko katika maeneo ya pembezoni mwa nchi hii ambaa ndiyo wale wasiofikiwa na taasisi hizi. Nitawapa mfano tu, mvuvi wa Kojani au mvuvi wa Mafia au mvuvi wa Ukerewe. Hawa wakiwa na mahali ambapo wanapata fursa ya kupata mitaji kwa haraka, wanaweza kurudisha mkopo wa milioni 3 katika kipindi kisichozidi miezi mitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo tunayo uhakika na ndiyo maana mimi naomba hizi taasisi zifike huko ili tuweze kurudisha au mkulima wa korosho akiwezeshe, anaweza akawa na zao kubwa la korosho na korosho ni zao lenye thamani ambayo haiwezi kupimika kwa biashara ndogo ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niongezee, mara nyingi tunatunga Sheria. Lakini hazifuatiwi na uhamasishaji au maelezo ya umma kuhusu hizi sheria tulizotitunga. Hii ni kati ya Sheria ambayo inapaswa isambazwe kwa haraka na katika lugha ya Kiswahili.

Mimi napata shida katika Miswada kama hii kuiweka katika kiingereza wakati watumiaji hawajui kiingereza, kwa hiyo, hata ukimpa hawezi akajua ni jinsi gani atakavyonufaika na hizo Taasisi zinazoanzishwa, swali. Kwa nini umoja wa Afrika na Bunge la Afrika limeweka lugha ya Kiswahili rasmi na sisi tunashindwa kutafsiri Miswada muhimu kama hii katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ombi langu ukishapita tu Waziri muhusika atafsiri haraka iwezekanavyo ili watu wote wa nchi hii wajue fursa

iliyopo inayotokana na Muswada huu. Kazi iwepo katika mafungu yanayotengwa katika mabenki kuwepo na fungu la maelezo kuwawezesha wananchi wetu kufahamu namna ya kuyafikia mabenki haya na taasisi zinazohusika. (*Makofi*)

Lingine ambalo napenda niliongeze hapa, tunapata matatizo ya kukopesha wananchi kwa sababu hatujafanya kitu ambacho kinafanyika kwa mataifa ambayo yamezoe kutumia benki. Mataifa mengine yanatumia benki huwezi kutumia pesa na ukikutwa unapesa nyingi watakushangaa hata dola mia moja ukiwa Marekani unaenda kwenye *Super Market* umenunua kwa dola mia moja watakutizama kwanza wamezoea kutumia senti ndogo ndogo kubwa wanatumia karatasi za benki. Sasa unaweza kufanya hivyo kama unakitambulisho ama anwani, je, wananchi wetu walio wengi wanakitambulisho na anwani?

Kwa hiyo, ndio maana mabenki na taasisi zinapata kigugumizi nikishampa huyu aliyejua mbele yangu kwenye *desk* langu hapa nitamtafutaje, *address* aliyonipa ni sahihi. *Address* sahihi ni kitambulisho na tunaweza kutumia hata namba zetu za kupigia kura kuwa ni namba za kututambulisha kwa kuanzia, halafu tukaongeza na namba nyingine mpaka tukafika mahali tukawa mwanachi wa Tanzania anaweza kujitambulisha ya kwamba ukinitafuta kwa namba fulani ndio mimi na mtu mwengine akasema kweli ama taasisi nyingine kama ni wilayani ama kijijini wakasema kweli tunamtambua kwa namba hii. Sisi ni nchi ambayo tuna watu wengi wageni tusipokuwa na vitambulisho, hatutaibiwa hata na watu wengine wanatoka nje wanavuka mipaka anakopa mapesa mengi, kuiba watakuja kuacha, hii kasi mpya na ari mpya wanajidanganya, haikomi hawa Rais na Waziri Mkuu nadhani hawategemei kukoma, hawa wanaendelea ukiwaangalia machoni mwao unaona hawa ni watu wakuendelea tu. (*Makofi*)

Sasa watakwisha, lakini kama hatuna vitambulisho watu watakopa bila ya kuwa na anwani na kuwa na kitambulisho cha kumtambua huyu ni Mtanzania anayo haki ya kukopa. Kwa hiyo suala la vitambulisho lisifikiriwe ni kutambulishwa kama walivyokuwa wanatambulishwa watu katika ukoloni ama manamba, ni utambulisho wewe upate haki ya kusema wewe ni Mtanzania, kwa maana hiyo hata ukienda benki unaweza kutumia kitambulisho chako kuwe kukutambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilisisitize hapa ni suala la *money laundering* sina uhakika kama hii sheria inatutosha ama lazima isisitizwe zaidi katika taratibu kuzuia *money laundering* benki zikianzishwa ili kusafisha pesa chafu, ndio *money laundering*. Sasa tusije tukakuta taasisi na mabenki yanaibuka kumbe ni katika kusafisha pesa zilizochafu zinazotoka nje ya nchi na zinazoibiwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kusema tufuate mfano wa China, mabenki haya kuyaanzisha tu hivi jumla jumla hayatusaidii, lakini wa China wenzetu tunahata benki za *construction and building*, mtu ambaye kazi yake ni *contractor* ana benki yake kwenda kukopa na kwa sababu ni rahisi kujua anakofanya kazi inampa uwezo, kwanza tunahitaji kuwapa *contractor*, *ma-engineer* na watu wengine uwezo anaenda kukopa kwenye *construction and building bank*. Wakulima wanakuwa na benki yao kwa sababu mahitaji yao ni tofauti na hawa watu wa *construction*, nyumba

wanakuwa na benki yao, wanawake wanakuwa na benki yao, nataka nirudie wanawake kwa maana namna ya kuweka na kupata pesa katika nchi hii kwa wanawake bado iko katika ngazi ambayo inahitaji kuzingatia masharti maalum kwa hiyo hili ni lazima liwepo mabenki mbalimbali kukidhi mahitaji. Vijana wana benki yao, kwa sababu vijana hawaaminiwi, anamuuliza wapi, umefanya kazi mara ngapi, wakishambana hivyo hawampi mkopo, iwepo benki maalum ya vijana ili tuweze kuwasaidia vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi baada ya kusema hayo ninaunga mkono na mtakia Waziri kila la heri katika kusimamia na pamoja na watu wake ndani ya Wizara hiyo na watakapoanza wahakikishe hizi benki zinafika Ukerewe. (*Makofi*)

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, awali ya yote naomba nimshurkuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa uhai na kuweza kunirudisha tena katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, la pili nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri anayoifanya yenye maendeleo na yenye ari aliyoitamka katika kampeni zake. Pia kumpongeza Waziri Mkuu kwa kazi anayoifanya ambayo inatia moyo na ari kwa wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijakupongeza wewe kupata Unaibu Spika, kwa kuweza kuwa Naibu Spika wa kwanza mwanamke hongera sana na kuwapongeza Wenyeviti wote pamoja na Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha, mama Zakia Meghji na ninampongeza kwa dhati, nina imani kuwa kazi aliyoipata ataifanya kwa kasi na kwa ari mpya na maana ya kumpongeza hivyo pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa sababu naelewa kuwa waswahili wanasema nani kama mama na hakuna kama mama na kasi tunaiiona. Kwa sababu katika muda wetu huu wa Bunge hili, katika Mkutano wa Tatu, Mheshimiwa Waziri ametuletea mambo mazuri sana, na imani alipoingia katika Wizara hiyo alijua vipi atawenza kuwasaidia Watanzania na katika kutafuta ufumbuzi wa kuweza kuwasaidia ndio haya ambayo ameyafanya yameweza kufika katika Bunge letu kwa haraka sana. Tukiangalia Muswada huu ambao ametuletea ni Muswada ambao wa ukombozi wa wananchi kama na sisi wenyewe tutahitaji kufanya kazi kwenu. Kwa sababu huwezi ukawasaidia wananchi bila ya kuweza kuwasaidia katika mikopo maeneo mbalimbali, lakini wameliangalia hili kwa kina zaidi na ndio sababu ya kutuletea kwanza, na imani wananchi wengi watafaidika na Muswada huu ambao umetufikia.

Pamoja na hayo naomba nichangie katika sehemu ya kwanza kuhusu masuala ya mikopo na riba, masuala ya mikopo na riba hapo nyuma ilikuwa ni kitu ambacho kinawasumbua sana wananchi. Sisi ambao tunakwenda katika ziara kwa wananchi wetu tunawaita kwenye mikutano na kuwaambia wajunge katika vikundi, lakini wanajiunga kwenye vikundi wapi wanapata mikopo, wanaweza wakaenda mtu kwenda kuchukua mkopo, anaambiwa lazima apeleke hati ya nyumba, ye ye mwenyewe anaomba mkopo, hiyo hati ya nyumba anaipata wapi, isitoshe mwininge anaenda kuomba mkopo ye ye

mwenyewe atoe shilingi 500,000. Yeye anataka kuomba mkopo wa shilingi 500,000 tena, kwa hiyo, mimi nina imani Muswada huu utawasaidia sana Watanzania, lakini bado tunaomba Serikali iweze kuangalia mabenki yetu, riba inakuwa kubwa sana, riba inakuwa kubwa hata wale wanaokopa wanashindwa kukamilisha mikopo yao, matokeo yake wanapata matatizo makubwa sana, kwa hiyo bado tunaomba Serikali iangalie kuhusu suala la riba, likishaangaliwa kuhusu suala la riba wananchi wataweza kukopa.

Mheshimiwa Naibu spika, mabenki mengi yanazungumzia kuwa wanapesa benki, lakini watu hawaendi kukopa, hakuna mtu anayeweza kwenda kukopa milioni mbili akalipa milioni tatu au milioni tatu na nusu.

Kwa hiyo, anajikuta anapata hasara yeye, tunaomba wapunguze riba, watakpopunguza riba zao wananchi wataenda kukopa kwa wingi sana, lakini kitu ambacho cha ajabu hata kwenye biashara tu akili timamu unaweza ukapata shida huwa unahela ndani watu hawahitaji kuzichukua lakini bado wewe unaendelea kukaa nazo hutumii utaratibu wowote wakuweza kuwasaidia wananchi ili waweze kukopa na wewe uendeshe katika biashara yako. Lazima hili waliangalie kwa kiasi kikubwa zaidi kuwa wananchi pamoja na kuwa tutapitisha Muswada bado riba zikiwa juu hawatoweza kwenda kukopa, hilo ni moja wapo. Lakini kuhusu suala la mikopo watu wengi wanaopata shida kuhusu mikopo ni wanawake na vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wengi ni watu ambaو wanaaminika na ni watu ambaو wana moyo wa kufanya kazi na wanarudisha mikopo kwa haraka sana, lakini wanaopata shida ni wao naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia wanawake waweze kupewa kipaumbele sana kwa sababu naona wako Waheshimiwa wengine wananiangalia hapa Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, anageuka kabisa na kunitazama, mimi ninachosema kwamba wanawake wapewe kipaumbele ili waweza kukopeshwa, asilimia kubwa ukiangalia kwa wafanyabiashara wengi sasa hivi ni wanawake na wanamitaji makubwa. Kwa hiyo tunaomba hawa waweze kusaidiwa kwa kiwango kikubwa sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hazara Pindi Chana, unapita kati ya msemaji na Spika, endelea Mheshimiwa Aziza.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuendelea kuongea, bado vijana tunamshukuru Mheshimiwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema atawasaidia wanawake na vijana ili waweze kuepukana na matatizo ya ajira. Suala la vijana, ni suala zito zaidi, vijana hawana ajira, vijana wako wengi zaidi kuna usemi uanosema vijana ni sawa na bomu ambalo limefunikwa majani, siku majani yale yakifunuka, hilo bomu litalipuka sana. Lakini na imani Muswada huu utawasaidia sana vijana, vijana wako ambaو wanaaoajiriwa katika Serikali na wako ambaو waliojiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya wale ambaو walijiajiri wenyewe, nasema kwa dhati kuwa wengi wanapata shida sana hawana nafasi zingine za kufanyabiashara, maeneo ambayo wanayokaa kufanyia biashara na wakatozwa ushuru,

bado wanasumbuliwa na wako ambao tayari wameshakopa mikopo katika benki, wengine wanaenda *PRIDE, FINCA* lakini sasa tayari mtakapo wasumbua wanahamishwa maeneo waliyokuwepo vijana na wakinamama hasa wale mama ntilie wanahamishwa maeneo wanayofanyia biashara kwa muda hivi saa ngapi watarudisha ule mkopo ambao waliookopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake unamrudisha nyuma kimaendeleo na kuweza kumsababishia arudi katika hali ya umaskini, hiyo ni kitu ambacho kinasikitisha kwa kweli tunaomba vijana na akinamama waweze kuangaliwa ili waepukane na matatizo kama haya na wao wanufaikie na mikopo ambayo inayotolewa na benki zao.

Lakini bado wako wafanyakazi, wako wafanyakazi wengine wa Halmashauri, mfano kama Sikonge siku ya wanawake duniani nilikwenda nikawaomba na wao watoe mawazo yao, nini wanaona katika wanawake kinaweza kikawasaki. Wako waliosema sisi ni wafanyakazi wa Halmashauri, lakini hatupati mikopo sasa hivi tumeshaandika barua zetu kwa kuombwa tukopeshwe lakini hatukuopeshwi, suala hili la wafanyakazi kutokupata mikopo peke yake ni moja ambayo ya kishawishi kuwashawishi ili waweze kuomba rushwa, kama kuna uwezekano wa kuwakopesha kwa nini tusiwakopeshe, ili na wao wajiedeleze katika maisha yao ya kifamilia, mimi nilikuwa naomba tuangalie na watendaji wetu pengine tukiwakopesha itatusaidia zaidi waepukane na vishawishi vingi vya rushwa. Bado wafanyakazi waweze kujiunga na wao *SACCOS* nimeona juzi katika *TV, TRA* wamejiunga *SACCOS* ile ni mojawapo ambayo itawasaidia wafanyakazi waweze kuepukana na masuala mbalimbali ya vishawishi na kama wakiomba mikopo basi na wao waweze kusaidiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea kuhusu masuala ya wakulima, wakulima wetu wa Tanzania wengi wanatumia jembe la mkono, huwezi kumkopesha mkulima ambaye anategemea mvua, halafu mvua inakuwa hainyeshi, ni sawa lakini mkulima huyu huyu kama tutamwezesha aweze kupata mikopo ili aweze kupata pembejeo zilizokuwa imara atalima bila ya matatizo yoyote, jembe la mkono halitoweze kumfikisha popote lakini bado tumsaidie aweze kukopa angalau basi aweze kupata hata trekta. Kilimo cha kutumia mkono kwa kweli wakulima wetu wanahangaika sana na asilimia kubwa kwa sababu hawakai wakapiga mahesabu, lakini akipiga mahesabu muda alioutumia pesa ambazo alizompa kama ni mkulima au ni ye ye mwenyewe kulima na mapato ambayo aliyoyapata, kwa kweli utajikuta amepata mapato madogo sana mwengine. Illa kwa wale ambao wana uwezo wa kuweka wakulima wanaoenda kuwalimia, ambao wanalima mashamba makubwa sana, kuna wale wakulima wadogo wadogo wanapata shida sana, hii ni moja wapo ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu, lakini bado si lazima kila mmoja awe na trekta lake, kuwe na utaratibu kama ni wa Serikali au wa watu binafsi wa kuweza kuwakodisha matrekta yale ili yaende kuwalimia katika mashamba yao, kwa sababu sio rahisi kila mmoja awe na uwezo wa kukopa trekta. Kuwe na utaratibu wa kuwakopesha ili waweze kwenda kuwalimia wananchi wale wabaki na kazi ya kupanda akitoa eka moja kwa shilingi 50,000 itamsaidia zaidi kuliko ye ye kila siku awe anakwenda na kurudi shamba ambayo bado itamrudisha nyuma hata huu mkopo utamsaidia aweze kukopa kulipa masuala ya trekta na kutafuta mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi ya kuchangia kwanza ningependa kuanza kwa kuipongeza Serikali yetu nikainza na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kasi ambayo ameanza nayo ambayo kama wengi wetu wameona na wamesema kwa kweli inakidhi na inaridhisha kabisa na inaendana na jinsi ambavyo amekuwa akiahidi kwenye kampeni. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia kwa kweli shughuli zote za Serikali hapa Bungeni kwa uimara kabisa na kwa kweli mimi nilikuwa simfahamu kwa karibu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nilidokezewa tu kwamba ni mfuutiliaji na katika kipindi hiki kifupi kwa kweli nimeridhika kwamba kweli mzee wetu huyu anaiweza hii kazi nampongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake na watendaji wote wa benki ambao wameleta Muswada huu mzuri kwenye hiki kipindi ambacho kwa kweli ni cha muhimu sana kuwa na Sheria itakayotuwezesha kutekeleza azma yetu kwanza ya kulinda maslahi ya nchi lakini kadhalika kwenda na dunia ya sasa ya utandawazi ya sayansi na teknolojia. Kwa ujumla Muswada ni mzuri na ninaunga mkono mia kwa mia. Kuna maeneo machache tu ambayo ningependa kuyazungumzia kama nyongeza.

Kwanza ningependa kusisitiza suala la kulinda maslahi ya nchi hasa kuzuia utoroshaji wa pesa nje ya nchi, kifungu namba 7(3) kinasema kwamba benki ikimaanisha Benki Kuu inaweza ikatoa kibali kwa mtu au benki kwa maana ya *Financial Institution* kama ilivyoandikwa kwenye sheria kufungua au kufanya biashara zake nje ya nchi. Sasa kwenye mazingira kama hayo nina wasiwasni na usimamizi utakaokuwepo, kwanza uwezo wenyewe wa benki kuu kusimamia *transaction* zitakazokuwa zinafanyika kati ya benki iliyoko hapa nchini na sehemu ya benki ambayo iko ya nje ya nchi yetu, kwa sababu katika mazingira ya nchi mbili tofauti kutakuwepo tofauti za kisheria lakini pia kutawepo na tofauti ya *currency* zitakazo kuwa zinatumika na hata gharama ya *supervision* watu kwenda kukagua benki ambayo iko nchi nyingine sidhani kama watu wa *BOT* wanawenza wakaruhusiwa kirahisi kama ambavyo inaweza ikatarajiwa. Kwa hiyo, nilifikiri eneo hilo ni vizuri tukatafuta namna ya kuliimarisha zaidi au walau kuwa na namna fulani ya kuhakikisha kwamba halitumiki kama mwanya wa kufanya biashara ambazo sio nzuri ikiwemo aliyosema sasa hivi Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, suala la *money laundering* inatumika sana pale ambapo kunakuwepo na mahusiano ya benki moja na nyingine ambazo ziko kwenye nchi mbili tofauti.

Lingine ni kuhusu shughuli za benki kwenye maeneo ya vijiji, wachangiaji wengi wamezungumzia kuhusu benki kufanya shughuli zake kuwafikia wananchi ambao hasa ndio tunaotaraji kwamba wanahitaji msaada wa kibenki, kwa bahati mbaya benki nyingi tulizonazo zinapenda kufanya shughuli zake mjini na zimekuwa zikifanya hivyo kwa sababu mbalimbali lakini kubwa zaidi ni kwamba wanapenda faida ya haraka haraka na hiyo inajidhihirisha ukiangalia financial statement zao kwa mujibu wa sheria ya benki ya mwaka 1995. Wanatakiwa kutoa *Financial Statement* kwenye vyombo vyahabari na

ukiangalia benki hizi zinafanya vizuri sana kwa maana kwamba wanapenda kufanya kazi katika maeneo ambayo wapo sasa.

Kwa hiyo, umuhimu wa kuzingatia huduma kwa wananchi walio wengi hawauzingati sana, sasa nilifikiri ni vizuri tukawa na msisitizo wa kisheria na wa kisera wa kuwasilitiza hawa wenyе mabenki waweze kufungua matawi zaidi vijijini au benki za kizawa (za Kitanzania) nyingi ziweze kuanzishwa ambazo zitakuwa zinahudumia wananchi walioko vijijini, na hapa ninamaanisha kwamba ni vizuri tukawa na vipengele kwenye sheria ambavyo vinatoa aidha, tofauti kati ya muomba leseni wa nje na muomba leseni Mtanzania ambaye tunategemea kwamba kama anayeomba leseni ni Mtanzania basi tutaangalia anakaa wapi, anategemea kufanya shughuli zake wapi na endapo hiyo benki inataka kuanzishwa sehemu ambayo haina benki kwa mfano tunataka kuanzisha *Kahama Development Bank* au Benki ya Wananchi wa Kahama, tunategemea katika mazingira hayo muomba leseni yule masharti yake walau yawe na unafuu fulani ukilinganisha na muomba leseni wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *interest rate*, wengi wamelizingumzia lakini ni vizuri na mimi nikalizingumzia kwamba *interest rates* zinatozwa na benki ni kubwa sana na kwa bahati mbaya wengi wa wenyе benki wamekuwa wana-product zenye kufanana. Sasa hivi karibu kila benki unakuta inatoa *salary loans* au mikopo kwa wafanyakazi walioajiriwa na *interest rate* zinafanana kati ya 20% mpaka 23%. Wakati ukiangalia vitu vingine ambavyo vinahusiana na *interest rate* kama gharama au tuangalie kwa mfano *inflation, deposit rate* vyote hivyo vinakuwa viko chini sana, sasa nilifikiri ni vizuri *interest rate* ziangaliwe kwa kupitia mfumo hasa wa kisheria na Benki Kuu iingilie kati kwenye eneo hili kwa sababu hawa wenyе benki wafanyabiashara wataangalia zaidi faida kuliko huduma na kwa upande wao haitakuwa tatizo sana kama wanawenza wakapata wateja wa kutosha wanaowenza kuwakopesha kwa hiyo asilimia 20 au zaidi ya *interest rates*.

Eneo lingine ni kuhusu msisitizo kati ya huduma na faida, benki nyingi tulizonazo, nyingi zinajitika zaidi katika kutafuta faida na wala si kutoa huduma na suala hii ipo hasa kwenye benki ambazo ni za nje zimepata leseni kufanya kazi hapa nchi kibiashara, ndio unakuta vijijini hakuna benki, watu wa vijijini hawapati nafasi ya kupata huduma za kibenki kwa sababu benki hizi zinakuwa haziko *interested* kwenda kule. Sasa nilifikiri hapa ni vizuri tukapata pia msukumo wa kisheria au wa kisera ambao utasimamiwa na Serikali. Kwanza mkakati kwa mfano wa *MKURABITA* ni vizuri ukawa *speeded up* ili kwamba wananchi watumie rasilimali walizonazo kuweza kukopesheka.

Pia ni vizuri kukawepo namna ya kuyashawishi mabenki haya yatumie rasilimali walizonazo wananchi kama ardhi, mashamba au mazao ya kudumu kama kahawa na mazao mengine kama migomba ambayo kwa kweli unaweza ukawa una uhakika kwamba katika kipindi cha miezi mitatu, minne ambacho mtu yule kakopa, shamba lile litakuwepo, mazao yale yatakuwepo na shughuli anayoombea kuifanya itakuwepo kwa hiyo, atawenza kulipa. Kwa sasa hivi kwa sababu mabenki hayako *interest* na hayajasukumwa kufanya hivyo hilo eneo bado limeachwa na wananchi wetu vijijini wanaendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu suala la *DIB* kifungu namba 38 kinachozungumzia kuwepo kwa *DIB* kirefu chake ni *Deposit Insurance Board*. Eneo hili ni muhimu sana lakini nilifikiri kukawepo kipengele cha saba baada ya kifungu cha 38(6) kinachosema kwamba *financial institution* au benki ambayo itashindwa kutoa michango yake kwenye *DIB* iweze kuwa na hatia ya kuweza kufutiwa hata leseni, kwa sababu kwa sasa hivi *penalt* ya asilimia moja sijui nukta tano ambayo itakuwa *charged on daily bases* lakini haijaweka *limit* kwamba hiyo *interest* au hiyo *charge* itaendelea kuwepo kwa muda wa siku ngapi au kwa muda wa miaka mingapi kama benki ile ambayo haijapelaka michango yake *DIB*. Kwa hiyo, nilifikiri ni vizuri kukaongezwa kipengele kwamba endapo hiyo michango ina *outstand* kwa muda fulani, basi benki ile iweze hata kufutiwa leseni kwa sababu kwa namna moja au nyininge itakuwa imekiuka msingi muhimu kabisa wa *ku-protect depositors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine nilichopenda kuzungumzia ni kifungu Na. 39 (2) na (3) ambacho kinasema mwananchi, *customer* ambaye ana akaunti benki akijua kwamba benki ile iko kwenye *process* ya kuwa *liquidated* au *ime-declare* kwamba inafilisika, anaweza aka *lodge* madai *DIB*, kifungu kidogo cha tatu kinaleza kwamba mwananchi yule anatakiwa ku-*prove* kwa *DIB* kwamba ye ye ana akaunti katika benki hiyo na anakiasi fulani cha pesa kwenye hiyo akaunti na kadhalika. Ombi langu au ushauri wangu hapa ni kwamba kipengele hicho kwa kweli kinaleta matatizo sana kwa wateja wa kawaida wa benki, kwanza ni wachache amba wanatunza kumbukumbu za amana au *deposits* zao kwenye benki *on daily basis*.

Kwa hiyo, waki-*declare* kwamba kwa mfano mimi nina akaunti *CRDB* au *Exim Bank* wakasema kwamba benki hiyo ina matatizo inakuwa siyo rahisi kujua kwamba *on that particular day* nina shilingi ngapi? Kwa sababu unawenza ukawa ume-*issue cheque* hazija-*clear* na mambo kama hayo. Sasa nilifikiri Benki Kuu kwa kuwa wao wana-*supervise* wakatumia rekodi ambazo wanawenza wakazipata kutoka kwenye benki ile kuweza kutumia kama *evidence* au *proof* ya kwamba watu fulani wanaamana kwenye benki hiyo na hivyo *balances* zao kwenye *accounts* zao zilikuwa ni kiasi fulani kwa siku hiyo na hivyo waweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumwomba mwananchi wa kawaida kwamba *approve* kwamba ana *amount* kiasi fulani kwenye benki *as of that particular day* nafikiri hii italeta tatizo kwenye utekelezaji na kwa kiasi fulani wananchi watashindwa kupata haki yao ambayo hasa ni pesa zao watakazokuwa wameziweka kwenye benki hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nimalizie kama nilivyokwisha kusema kwamba nawapongeza sana Wizara ya Fedha kwa kuleta Muswada huu amba kwa ujumla wake una madhumuni mazuri kabisa na pia naomba niseme naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani muda uliobakia hautoshi sisi kuendelea, lakini kama tulivyosema mpangilio wetu wa kazi ni kwamba Muswada huu

unapaswa kuisha kesho jioni, kwa hiyo, msifikiri kwamba mmechelewa kuomba kuzungumza, bado hamjachelewa tutaendelea nao kesho.

Sasa nina tangazo hapa kwamba asubuhi Mheshimiwa Spika alikuwa ametangaza kwamba kesho tarehe tano Kamati ya Kanuni za Bunge ingekaa kwa ajili ya kufikiria majina ya Kamati pamoja na mabadiliko ya Wizara yaliyotokea. Sasa kwa sababu ya maandalizi yale inabidi wanaoandaa waingie kwenye *instrument* ya Wizara zile kujua kwamba kila Wizara imepewa kazi gani ili tuweze kupanga vizuri. Kwa hiyo, maandalizi hayo bado hayajakamilika, kwa hiyo, Kamati hiyo itakutana kabla ya kipindi cha bajeti Dar es Salaam. Kwa hiyo, kesho hakuna Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nimeeleza pia kwamba *exhibition* wanaendelea na watafunga kesho, kwa hiyo, mnaalikwa kwenda kuangalia.

Baada ya kusema hayo sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.30 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano
tarehe 5 Aprili, 2006 saa tatu asubuhi)*